# Nipashe

Jumatatu Februari 4, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579832

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Mwanafunzi darasa la nne adaiwa kujinyonga

UKURASA 2




UKURASA 13

# Jaji atoa angalizo sakata la kikokotoo

UKURASA 21

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**WAZIRI MPINA ATANGAZA KUIFUMUA SHERIA YA UVUVI**

SERIKALI imeamua kuifumua Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009 ili kuondoa vikwazo vya kibiashara na uwekezaji katika...

UKURASA WA 4

**ASKOFU SASA AWAFUNDA WANASIASA KUHUSU JPM**

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Philadelphia Gospel Assembly, linalohudumu katika Bara la Afrika, Dk. Yohana Masinga, amewasihi wanasiasa wa Tanzania...



## Kiama waliokopa mabilioni ya TIB

UKURASA 2



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, akibadilishana mawazo na Corotrida Kokupima, baada ya kufunga kikao kazi jijini Dodoma, kujadili mbinu mpya za kukabiliana na mauaji ya vikongwe pamoja na kujijengea uelewa wa mkakati mpya wa kutokomeza mauaji ya wazee nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mikataba mibovu nishati, madini kutikisa Bunge leo

UKURASA 2

**MICHEZO** FIFA YALETA NEEMA SIMBA, YANGA SC UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Kiama vigogo waliochukua mabilioni benki ya serikali

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limetaka vigogo wote waliokopa mabilioni ya shilingi katika Benki ya Uwekezaji (TIB) na kushindwa kurejesha fedha za umma, wachunguzwe na watakaothibitika kufanya udanganyifu, wafikishwe mahakamani kwa Sheria ya Uhujumu Uchumi.

Deni la mikopo chechefu ya TIB ni Sh. bilioni 251.89, kwa mujibu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) iliyoeleza kuwa hali hiyo imeanza kuathiri utendaji wa benki hiyo.

Kutokana na hali hiyo, Bunge limeazimia serikali na benki hiyo wachukue hatua stahiki kwa wadaiwa sugu wote kwa kupiga minada dhamana za wadaiwa hao, kwa kuwa wanafahamika na dhamana zao zinajulikana.

Mwenyekiti wa PAC, Naghenjwa Kaboyoka, akiwasilisha taarifa ya shughuli za kamati yake bungeni jijini Ddooma mwishoni mwa wiki, alisema benki hiyo imeelekezwa kutoa notisi ndani ya mwezi mmoja kwa wadaiwa wote kulipa madeni yao kwa mujibu wa mkataba.

"Ili kuondoa dhana kuwa mikopo inayochukuliwa kutoka benki za umma haipaswi kurejeshwa, serikali kwa kushirikiana na TIB na vyombo vingine vya dola, wafanye uchunguzi wa wakopaji wote na wale watakaothibitika kufanya udanganyifu, iangaliwe uwezekano wa kutumia Sheria ya Uhujumu Uchumi kuwashtaki mahakamani,"alisema.

Kaboyoka alisema kamati yake imefanya uchambuzi wa wadaiwa sugu katika kundi hilo na kubaini mikopo mingi ilichukuliwa na watu

INAENDELEA UK.8

# Mikataba mibovu nishati, madini kutikisa Bunge leo

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MJADALA mkali kuhusu sekta za madini na nishati unatarajiwa kuibuka leo bungeni jijini Dodoma, wakati kamati mbili za Bunge zitakapowasilisha ndani ya chombo hicho taarifa za shughuli zake kwa mwaka 2018.

Masuala kama viwango vikubwa vya tozo za kodi na ushuru vinavyowachochea wafanyabiashara wengi kukwepa kulipa tozo hizo na mikataba mibovu ya sekta ya madini, huenda vikaibuka katika mjadala huo.

Vilevile, mikataba mibovu ya sekta ya nishati hasa inayolihusisha Shirika la Umeme (Tanesco) na shirika hilo kuripotiwa kupata hasara ya mabilioni, kunatarajiwa kuwa hoja za baadhi ya wachangaji.

Ratiba ya mkutano wa 14 wa Bunge ulioanza Jumanne iliyopita, inaonyesha kwamba, leo kamati hiyo itawasilisha taarifa ya shughuli zake kwa mwaka 2018.

Januari 22, mwaka huu, wakati wadau wa sekta ya madini walipokutana na Rais John Magufuli jijini Dar es Salaam, walimweleza utitiri wa tozo, ushuru na kodi ulivyo changamoto kubwa katika biashara na sekta ya madini.

Wadau hao walimweleza Rais Magufuli kwamba tozo kubwa na nyingi zilizowekwa katika madini, hasa dhahabu, zimesababisha wachimbaji wadogo, wa kati na wafanyabiashara wengi kukwepa kuuza madini yao katika utaratibu rasmi.

Hoja hiyo inatarajiwa kuibuka leo bungeni, wakati wa mjadala wa

INAENDELEA UK. 8



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akiagana na mgeni wake Waziri wa Kilimo na Masuala ya Ardhi wa Misri, Dk. Ezzaldin .O. Abusteit, baada ya kumaliza mazungumzo yao Ikulu Zanzibar jana. Anayefuata ni Balozi wa Misri nchini, Gaber Mohamed. **PICHA: IKULU**

**WANATAKIWA HARAKA:**

1. WASAIDIZI WA WATOTO SHULENI
2. WAPISHI:

Shule ya nursery na primary iko kigamboni, kibugumo inatafuta wadada wa kusaidia watoto, usafi wa ofisi na kusindikiza watoto kwa school bus asubuhi na jioni.

**Kiwango cha elimu: Form four** and above
Pia inatafuta **wapishi wenye uzoefu** wa miaka mingi kupika mashuleni.

Uwe na uwezo wa kuhamia kigamboni kwa ajili ya kazi.

**Kama uko tayari piga simu no: 0627301010 kwa maelezo ya kufikisha Maombi yako.**

# Mwanafunzi darasa la IV adaiwa kujinyonga

**Na Enock Charles**

MTOTO wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Msewe jijini Dar es Salaam, Daniel Mussa (10), anadaiwa kukutwa amejinyonga chumbani kwake nyumbani kwao Kimara Kona jijini.

Tukio hilo lililotokea Januari 30, limethibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Jumanne Muliro, aliyedai uchunguzi wake bado unaendelea ili kubaini chanzo halisi cha tukio hilo.

"Kuna mambo matatu hapo; kajinyonga, kafa au kauawa? Sisi bado tunachunguza ili kujua ukweli," Kamanda Muliro alisema.

Alisema hakuna mtu wanayemshikilia kutokana na tukio hilo, lakini wanafanya uchunguzi kwa watu wa karibu na mtoto huyo wakiwamo wazazi na ndugu zake.

"Sisi (Jeshi la Polisi) tunapochunguza, ninyi (waandishi wa habari) husema tunawashikilia, tunahoji watu wa karibu baba, baba mdogo na wengine ili kupata ukweli wa tukio," alisema.

Nipashe ilimtafuta Mwalimu wa Taaluma wa Shule ya Msingi Msewe, Mathias Shayo, ambaye alidai kuwa walipokea taarifa kutoka kwa mama wa mtoto huyo kuwa amefariki dunia kwa kujinyonga.

"Mama yake ndiye alitoa taarifa ya kujinyonga kwa mwanafunzi wetu, ila sababu za kujinyonga, sisi hapa shule hatuzijui," mwalimu huyo alisema.

Bibi wa mtoto huyo aliyejitambulisha kwa jina la mama Lindi, akizungumza na Nipashe jijini mwishoni mwa wiki, alidai kuwa, kabla ya kukutwa na umauti, mtoto huyo alikula na kwenda kulala na baadaye saa 11 jioni alikutwa amejinyonga chumbani kwake.

"Aliporudi shule alikula chakula, akaenda kununua ubuyu, halafu akarudi akawa anasafisha kabati, baadaye alienda kulala. Baada ya muda kidogo, nilipewa taarifa kuwa Dan amejinyonga," mama Lindi alidai.

Bibi huyo alidai: "Nimemlea Dan tokea akiwa mdogo sana, kwa kweli tulimpenda sana, ila ndiyo hivyo tena, hatuna namna."

## HABARI KITAIFA

# Waziri Mpina atangaza kuifumua Sheria ya Uvuvi

**Na Mwandishi Maalum**

SERIKALI imeamua kuifumua Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009 ili kuondoa vikwazo vya kibiashara na uwekezaji katika sekta ya uvuvi.

Pia kwenda na kasi ya mabadiliko ya Serikali ya awamu ya tano inayolenga kujenga Tanzania ya viwanda, kuwatetea na kuwalinda wanyonge.

Akizungumza katika uzinduzi wa ukusanyaji maoni ya wadau kuhusu rasimu ya Sheria ya Uvuvi na Sheria ya Ukuzaji viumbe kwenye maji jijini Dar es Salaam, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alitaja sababu nyingine zilizosababisha kuwapo mabadiliko hayo.

Sababu ya kwanza pamoja na kutoa ulinzi madhubuti wa rasilimali za uvuvi, kuongeza uzalishaji na kuwa na masoko ya uhakika sambamba na kudhibiti utoroshwaji na uingizaji holela wa mazao ya uvuvi nchini.

Aidha, Mpina alisema sheria hiyo mpya inatakiwa iendane pia na mabadiliko na matumizi ya sayansi na teknolojia katika uvuvi na ukuzaji viumbe kwenye maji ili kwenda sambamba na mahitaji pamoja na kuwapo mwamko mkubwa wa ufugaji wa samaki kwenye maji uliojitokeza miongoni mwa wananchi.

Alisema pamoja na rasimu ya sheria hizo mbili pia Serikali iko kwenye hatua za mwisho za kuzifanyia marekebisho Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Namba 29 ya mwaka 1994 na Kanuni zake za mwaka 2009 na Sheria ya Bahari Kuu Cap 388 na Kanuni zake za mwaka 2007 na 2016.

Hivyo Waziri Mpina aliwasihi wananchi kutoa maoni yasiyofungamana na upande wowote na kuacha tabia ya kila mmoja kuvutia upande wake ili kuwezesha kutunga sheria madhubuti.

Aidha Waziri Mpina alieleza utajiri wa kipekee wa rasilimali za uvuvi nchini ikiwamo kuwa na eneo kubwa la maji lenye kilomita za mraba 346,337 sawa na asilimia 36.7 ya eneo lote la nchi, fukwe ndefu na za kuvutia, kuwapo kwa samaki na viumbe vingine ambavyo vimetoweka na vingine vikiwa kwenye tishio la kutoweka duniani.

Pia kuwapo kwa mito, mabwawa na maziwa yenye sifa za kipekee ikiwemo Ziwa Victoria ambalo ni la pili kwa ukubwa duniani na Ziwa Tanganyika ambalo ni la pili kwa kina duniani na la kwanza kwa ujazo wa maji duniani.

Alisisitiza kuwa wakati nchi inakwenda kutunga sheria hiyo mpya ya uvuvi, ni muhimu kama Taifa kujiuliza maswali kadhaa ikiwamo matumizi sahihi ya rasilimali hizo.

Uchangiaji rasimu hiyo uliwahusisha wachakataji wa samaki, wauza zana za uvuvi, wafugaji wa samaki kwenye maji, wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, wawakilishi wa vyuo vikuu na viongozi wa dini.

Wakizungumzia mapungufu ya sheria hiyo baadhi ya wadau wa wavuvi walisema sheria imekataza matumizi ya taa za sola, jenereta pamoja na utitiri wa leseni hali iliyochangia wavuvi wengi kushindwa kutekeleza kikamilifu majukumu yao.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mahmoud Mgimwa, aliipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kubuni wazo hilo na kusisitiza kuwa wao kama Bunge wako tayari kushirikiana na Serikali katika kubadilisha sheria zote zinazokwamisha juhudi za kujenga Tanzania ya viwanda, huku akisisitiza wadau kutumia vizuri fursa hiyo na kwamba wasijitoe katika uandaaji wa sheria hizo mpya.

Katibu Mkuu Uvuvi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Rashid Tamatama, alisema atasimamia kikamilifu uratibu wa zoezi zima la ukusanyaji maoni ya wadau na kwamba timu ya wataalamu wa wizara hiyo itaenda kila mahali walipo wadau.

# Repoa yashauri ukuaji uchumi

**Na Frank Monyo**

TAASISI ya Utafiti ya Repoa imetajwa kuwa taasisi bora ya utafiti Afrika kwa mara ya tatu mfululizo, baada ya kupanda nafasi moja juu katika ubora wa taasisi za utafiti barani Afrika, huku ikiishauri serikali ukuaji uchumi.

Kwa mwaka huu taasisi hiyo imeshika nafasi ya 11 kati ya taasisi 600 za barani Afrika na mwaka jana ilishika nafasi ya 12 kati ya taasisi 300, katika ukanda huo na kwa upande wa Tanzania imeshika namba moja kwa mwaka huu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Repoa, Dk. Donald Mmari, alisema ubora huo umetambuliwa katika matokeo ya Ripoti ya Utafiti wa kutathmini taasisi zinazotoa mchango kwa serikali na jamii katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa duniani uitwao The Global Go To Think Tank Index (GGTTI) 2019, ambao umeitaja Repoa kama taasisi bora ya tafiti zenye matokeo chanya kwa taifa.

Tathmini hiyo hufanyika kila mwaka chini ya mradi wa Think Tanks and Civil Societies Program (TTCSP) wa Chuo Kikuu cha Pennsylvania cha Marekani.

INAENDELEA UK. 8



# TGNP yataja dawa mauaji ya watoto

**Na Yasmine Protace**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP Mtandao) kwa kushirikiana na wadau wa haki za wanawake, haki za watoto na usawa wa kijinsia, wametoa salamu za rambirambi kwa familia iliyopoteza watoto mkoani Njombe, kutokana na matukio ya mauaji yakiyohusishwa na imani za kishirikina.

Kadhalika, limetoa ushauri mbalimbali kwa lengo la kukomesha mauaji hayo. Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, walipotoa tamko dhidi ya mauaji ya watoto hao.

"TGNP Mtandao, kwa kushirikiana na wadau wa haki za wanawake, watoto na usawa wa kijinsia tunatoa salamu za rambirambi kwa familia zilizopoteza watoto mkoani Njombe kutokana na matukio ya mauaji yanayohusishwa na imani za kishirikina," alisema.

Aliongeza: "Vitendo hivyo havikubaliki katika jamii kwa kuwa ni kinyume cha azimio la ulimwengu juu ya haki za binadamu la mwaka 1948. Kifungu cha 3 kinachotamka kwamba kila mtu ana haki ya kuishi, haki ya uhuru na haki ya kulinda nafsi yake. Na ni kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) Ibara ya 14 imetamka juu ya haki ya kuishi sambamba na Sheria ya Haki ya Kuishi ya mwaka 1984."

Alisema jamii inawajibu wa kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia, hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto na. 21 ya mwaka 2009 na mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA), unaolenga kupunguza kiwango cha ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika jamii yetu kwa asilimia 50 ifikapo 2022.

Aliongeza kuwa matukio kama hayo yamesababisha vifo vya wananchi (wanawake, wanaume, wazee na watoto) wasio na hatia kama vile mauaji ya vikongwe, watu wenye ualbino na sasa yanafanyika kwa watoto ambao hawana ulemavu.

Kwa mujibu wa Liundi, TGNP Mtandao inatambua jitihada za serikali ngazi ya wilaya, mkoa na taifa katika kukabiliana na suala hilo na kamati ya kuchunguza mauaji hayo imeundwa na kwao wanaona ni jitihada nzuri pamoja na kwamba upelelezi unaendelea. Aliongeza kuwa TGNP inashauri kamati iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe ilete majibu haraka iwezekanvyo, na taarifa ya uchunguzi ifanyiwe kazi kwa wakati ili kutokomeza kabisa mauaji hayo.

Pia serikali na vyombo vya dola visimamie kikamilifu Sheria ya Kudhibiti Uchawi na. 12 ya mwaka 1998, ambayo imeainisha adhabu kwa watu wanaoendesha vitendo vya kishirikiana vinavyoweza kudhuru wengine.

Aidha, wanalitaka Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola kuhakikisha watoto wanakuwa salama kwa kuimarisha ulinzi katika maeneo yote yanayotajwa kuwa sio salama katika Mkoa wa Njombe ili kuhakikisha watoto wanahudhuria masomo kikamilifu. Liundi aliongeza kuwa wanataka jamii kutoa ulinzi wa mtoto kwa sababu ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha ustawi wa watoto.

Vilevile, serikali na wadau kuzijengea uwezo kamati za ulinzi wa watoto ili kutimiza majukumu yao ikiwamo kubaini maeneo hatarishi katika kijiji/ mtaa na kupanga mikakati ya kupunguza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

# Askofu awaasa wanasiasa kutombeza Magufuli

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Philadelphia Gospel Assembly, linalohudumu katika Bara la Afrika, Dk. Yohana Masinga, amewasihi wanasiasa wa Tanzania kuacha kubeza juhudi na mafanikio ya Rais John Magufuli na badala yake ameshauri wamuunge mkono.

Moja ya mambo ambayo Askofu Masinga ametaka yaungwe mkono kwa vile yana maslahi mapana kwa taifa ni ujenzi wa reli ya kisasa, mradi wa umeme stieglers gorge na uamuzi wa Rais Magufuli wa kununua ndege zinazomilikiwa na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL).

Akizungumza jana katika hafla maalumu ya kuchangia ujenzi wa kanisa jipya litakalokuwa na uwezo wa kuingiza watu 3,000 kwa wakati mmoja, Dk. Masinga alieleza kushangazwa kwake na viongozi hasa wanasiasa kubeza juhudi hizo.

"Mimi nashangaa baadhi ya viongozi wa kisiasa wamekuwa kinyume cha mafanikio hayo yanayoletwa na Rais wetu (Magufuli), hapa kinachohitajika siyo kubeza, bali wanahitajika kuunga mkono juhudi hizo ambazo kila Mtanzania hivi sasa anafurahia na kunufaika," alisema.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Magufuli amefanikiwa kuimarisha nidhamu, uadilifu na uwajibikaji ndani ya utumishi wa umma pamoja na kukemea uzembe na kujenga ari ya kufanya kazi.



Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo Chadema (Bavicha), Wilaya ya Shinyanga Mjini, Samson Ng'wagi, akiwatia moyo wabunge wa chama hicho, viongozi na madiwani wasitetereke kukipigania chama na maslahi ya wananchi licha ya muswada wa Sheria wa Vyama vya Siasa kupitishwa na Bunge. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Sheria kali majangili wa vitoweo yatakiwa

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa** IRINGA

SERIKALI imeshauriwa kuzipitia upya sheria zilizowekwa kwa majangili wanaojihusisha na vitoweo katika hifadhi ili ziwe na nguvu badala ya kuishia kulipa faini ndogo.

Katibu wa Jumuiya ya hifadhi ya Wanyamapori Mbomipa (WMA), Joseph Kisanyage, alisema kuwa sheria zilizopo zinaruhusu ujangili kuendelea. "Faini zinazopigwa na mahakama kwa ajili ya wanyapori ni ndogo na mtuhumiwa anaona ni bora kulipa faini na kuendelea na ujangili wa vitoweo," alisema.

Aliongeza: "Unaenda na jangili mahakamni unarudi naye katika basi umempeleka kabisa na nyama za porini, lakini faini anayopigwa ni ndogo inakatisha tamaa."

Kasanyage alisema mtu mmoja ambaye alivua samaki tenga 10 alipigwa faini ya Sh. 6,000 jambo ambalo haliwezi kumaliza tatizo la ujangili wa vitoweo. Alisema endapo sheria hizo zikiongezwa makali majangili watakuwa wanaogopa hata kwenda kufanya ujangili kwa kuwa ataogopa kupigwa faini kubwa ama kwenda jela.

Alisema majangili hao hawaogopi kufanya ujangili wa vitoweo kwa kuwa wanajua faini yake ni ndogo, huku wakijiingizia fedha.

Kasanyage alisema ujangili wa tembo umepungua, lakini bado kuna changamoto ya ujangili wa samaki na asali unaendelea.

"Zamani ilikuwa ukiwinda swala unakula wewe na familia yako, lakini kwa sasa wanafanya biashara mtu anapiga nyati anakwenda kuuza, anakwenda kutafuta tena mwingine tusipoangali wanyama wataisha."

Aidha, alisema ujangili wa wanyama kama tembo hakuna kwa sasa kutokana na jitihada mbalimbali zilizowekwa za kudhibiti tatizo hilo.

Alisema hata ukienda katika hifadhi utaona wanyama kama tembo kwa ukaribu wakiwa na watoto wao ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Kisanyage alisema kupitia ujirani mwema uliopo wamekuwa wakishirikiana na Hifadhi ya Taifa Ruaha katika kulinda hifadhi ili rasilimali hizo ziwe na manufaa katika nchi. Aliongezea kuwa: "Jangili hawezi kuja moja kwa moja na kuingia hifadhini bila kushirikiana na mtu hapa kijijini kutokana na ulinzi ambao tumeuweka akija jangili lazima akamatwe."

# Mpango waja kudhibiti vifo kinamama, watoto

**Na Elizabeth Zaya**

MUUNGANO wa Utepe Mweupe na Uzazi Salama (WRATZ), umezindua mpango mkakati wa miaka mitano wa kupambana na vifo vitokanavyo na uzazi kwa kinamama na watoto.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mpango huo jijini Dar es Salaam, Mratibu wa Taifa wa WRATZ, Rose Mlay, alisema lengo la kuzindua mpango huo ni kuhakikisha kinamama wajawazito wanaendelea kuwa salama wakati wa kujifungua.

Mlay alisema pamoja na mambo mengine, pia wanataka kuhakikisha wanakomesha kabisa vitendo vya ukatili hasa kwa wanawake pamoja na watoto. "Tunataka kuangazia zaidi kwa kuhakikisha kina mama wanakuwa salama wakati wa kujifungua, lakini pia wanapata vifaa vyote vinavyohitajika wakati wa kujifungua pamoja na huduma bora, watoto wachanga nao tunataka wawe salama,"alisema Mlay na kuongeza:

"Tunataka wanawake waonyweshe upendo wakati wanajifungua, wapate huduma zinazowafurahisha, yaani wakienda katika kituo cha afya, wakute huduma rafiki zenye ukarimu kwao. Wapo kinamama ambao wanajifungua kwa mara ya kwanza kwa hiyo ni lazima wapatiwe huduma bora, wanahitaji uangalizi wa karibu."

Mlay alisema jambo jingine ambalo wamelenga katika mpango huo ni kupiga vita watoto wadogo kuozwa na kunyimwa haki zao za msingi.

"Pia tunataka hizi ndoa za watoto wadogo zikomeshwe kwa sababu unapomwozesha mtoto wa miaka 14 au 15, inapofika katika hatua ya kubeba ujauzito na kujifungua, anapata tabu sana na hata wakati mwingine anafariki, tunaomba msaada katika hili tuwaokoe hawa watoto," alisema Mlay.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Muungano huo wa Utepe Mweupe, Lulu Mwanakilala, alisema zipo hatua mbalimbali ambazo zimeanza kuchukuliwa na serikali katika suala la kuboresha uzazi salama japokuwa kunahitajika zaidi jitihada zaidi katika kuboresha sekta ya afya hususani katika kuongeza wataalamu wa uzazi.

Alisema kuna umuhimu wa kuhakikisha kunakuwa na vituo vya afya katika kila sehemu vyenye vifaa, huduma bora pamoja na wataalamu wa kutosha ili kuondoa vikwazo vyote katika suala la uzazi.

"Mkazo zaidi unahitajika, kwa ulimwengu wa sasa hatuhitaji kuona hata mwanamke mmoja anapoteza maisha wakati anajifungua, tunafahamu jitihada kubwa inayofanywa na serikali katika kuboresha suala la uzazi salama, tunaamini itazidi kulipa kipaumbele suala hili kwa sababu hata hivyo tumekuwa tukifanya kazi kwa karibu sana Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu na amesaidia sana kwa kweli," alisema Lulu Mwanakilala.



Katibu wa CCM Mkoa wa Morogoro, Shaka Hamdu Shaka akizungumza katika mdahalo wa wazi wa vijana uliozungumzia uzalendo, uongozi na hatima ya taifa letu uliofanyika mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Kebwe Steven Kebwe na kushoto Mjumbe wa NEC, Ruta. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Upatikanaji wa taulo za kike changamoto

**Na Beatrice Shayo**

WANAFUNZI wa kike hasa walioko katika maeneo ya vijijini bado wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa taulo za kike, hali ambayo imesababisha wengine watumie magunzi ya mahindi kujisitiri.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mratibu wa kampeni kwa ajili ya kumsaidia mtoto wa kike, Miriam Mauki, alisema:

"Tulikuwa tunawauliza huwa wanafanyaje wanapopata hedhi, msichana mmoja, akasema huchukua magunzi baada ya kumaliza kuvuna na kuyahifadhi na wanapokuwa kwenye hedhi huchukua taulo na kuviringisha katika gunzi na kuiweka sehemu ya siri kujisitiri."

Alisema mbali na msichana huyo kutumia magunzi ya mahindi, wapo ambao wamekuwa wakiazimana nguo za ndani jambo ambalo ni hatari kwa afya.

"Tulipoenda Wilaya ya Karatu tuliona watoto wa kike wakiwa hawawezi kukimbia vizuri, badala yake wanajikunya ndipo tukagundua kuwa watoto wengi hawana sidiria na hii inawanyima kujiamini," alisema.

Mauki alisema wameamua kuanzisha kampeni ya siku 40 kwa ajili ya kupata taulo za watoto wa kike pamoja na nguo za ndani kama chupi na sidiria, baada ya kuona watoto wengi wa kike wanapata changamoto za kujisitiri kwa kuwa hali hiyo husababisha wengi wao kukosa umakini na kujiamini wanapokuwa darasani.

"Girls Initiative ni taasisi isiyo ya kiserikali ambayo inalenga kumfikia mtoto wa kike kwa kumwezesha kifikra, kijamii na kiuchumi kupitia mafunzo na mbinu mbalimbali za kuweza kumkomboa mtoto wa kike katika changamoto anazopitia," alisema Mauki.

Naye mhamasishaji wa kampeni hiyo, Sadaka Said, alisema kampeni hiyo ambayo imelenga kuwafikia watoto wa kike nchi nzima, itasaidia kupunguza mimba za utotoni.

Mtaalamu wa Mahusiano, Reeves Ngalemwa, aliwaomba watu kujitokeza kuchangia kampeni hiyo ambayo unaweza hata kutuma Sh. 1,000 kwa Tigo Pesa kupitia simu yako ya mkononi kwa namba 0677069428 ambayo imesajiliwa kwa jina la Christom Solutions.


ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

**MAKAO MAKUU**
**Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole**
**S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania**
**Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu na 19(2) (a) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414)**

TAARIFA inatolewa kwa umma kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu (Karatu WSSA) ("Mwombaji") kwa ajili ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Karatu. EWURA inakaribisha maoni au pingamizi kutoka kwa wananchi juu ya maombi hayo. Maelezo ya Mwombaji ni kama yalivyotolewa hapa chini:

**1: Jina na Anuani:**

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu,
S.L.P 376,
Karatu - Arusha,
Tanzania.

**2: Maelezo ya Leseni:**

Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Karatu.

**3: Chanzo cha Maji na Miundombinu**

Chanzo cha maji kinachotegemewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu ni Kisima cha Bwawani chenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 720 kwa siku. Miundombinu ya uzalishaji na uhifadhi maji ya muombaji, inajumuisha, tanki moja (1) lenye mita za ujazo 225 na kituo kimoja (1) cha kusukuma maji (pumping station) . Vilevile, muombaji ana mtandao wa majisafi; wenye urefu wa kilomita 2.9 kwa bomba kuu la kusafirisha maji, kilomita 13.3 kwa bomba kuu la kusambaza maji, kilomita 2.3 kwa mabomba ya maunganisho ya wateja yaliyotengenezwa kwa malighafi mbalimbali (GS, HDPE na PVC), kiwango tofauti (PN10 na PN 16) na vipenyo tofauti tofauti (DN25mm mpaka DN150mm) na vituo 14 vya kuchotea maji. Aidha, muombaji hana mfumo wa kukusanya wala mitambo ya kusafisha majitaka.

**4: Umiliki**

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mtu yeyote mwenye kukusudia kuwasilisha maoni au pingamizi juu ya maombi tajwa hapo afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia siku ya kuchapishwa kwa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi hayo zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote kwa maombi ya maandishi kwa anuani iliyooneshwa hapa chini:

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji,**

XXXXXXXX

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Simba mkijipanga Taifa nafasi robo fainali ipo

**KWA** mara ya pili mfululizo wawakilishi pekee wa Afrika Mashariki na Kati kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wamepoteza mechi ya pili ugenini baada ya Jumamosi kukubali kichapo cha mabao 5-0 dhidi ya Ahly ya Misri.

Simba imepoteza mechi hiyo ikitoka kupokea kipigo kama hicho ugenini dhidi ya AS Vita ya DR Congo wiki mbili zilizopita. Kwa matokeo hayo Simba inaendelea kubaki katika nafasi yake ya tatu ikiwa na pointi tatu, huku Al Ahly ikiendelea kukaa kileleni mwa Kundi D ikiwa na alama saba wakati AS Vita ikishika nafasi ya pili ikiwa na pointi nne baada ya juzi kulazimishwa sare ya mabao 2-2 nyumbani dhidi ya JS Saoura ya Algeria inayoburuza mkia na alama mbili.

Kwa namna mtiririko wa matokeo hayo yanavyopatikana inaonyesha wazi njia pekee ya kuweza kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ni kushinda nyumbani na kwenda kung'ang'ania angalau sare ugenini.

Kwa kuwa kinara Al Ahly ambao wameshacheza mechi mbili nyumbani, zote wameshinda na kupata sare moja ugenini dhidi ya JS Saoura nchini Algeria wakati AS Vita ikishinda moja na sare moja nyumbani, lakini pia ikipoteza ugenini dhidi ya Wamisri hao.

Hivyo wakati huu Simba ikirejea kujiandaa kuikaribisha Al Ahly Jumanne ya Februari 12, mwaka huu, haitakiwi kufanya makosa katika mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Taifa.

Kwa kuwa kushinda mechi hiyo ya nyumbani kabla ya kuifuata JS Saoura nchini Algeria Machi 9, si tu itakuwa imejiweka katika nafasi nzuri bali pia wachezaji watakuwa wamejiongezea morali kuelekea mechi hiyo ya ugenini.

Tunaamini kama Simba itaichapa Al Ahly na kisha kwenda kulazimisha sare ama kupata ushindi ugenini dhidi ya JS Saoura shughuli itakuwa nyepesi Uwanja wa Taifa dhidi ya AS Vita katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi Machi 16. Tunafahamu Simba imefanya makosa makubwa sana kuruhusu mabao mengi (kumi) ugenini dhidi ya AS Vita na Al Ahly, lakini inaweza kufuta makosa hayo na kurejesha matumaini endapo nayo itahakikisha inamwotea mpinzani wake mmojawapo hapa nyumbani kwa ushindi mnono.

Pia, hata kama haitapata ushindi wa kishindo kama huo, lakini ikahakikisha inashinda mechi zote za nyumbani na kwenda kupigana kiume ugenini dhidi ya JS Saoura na kupata angalau sare itakuwa na nafasi kubwa ya kutinga robo fainali.

Kikubwa kwa sasa ni benchi la ufundi Simba kuwajenga wachezaji kisaikolojia waamini inawezekana kushinda mechi zake zote zilizobaki mbili za nyumbani na moja ugenini. Kama Al Ahly na AS Vita zimeweza kushinda kwao kwa nini Simba ishindwe kuutumia vema uwanja wake wa nyumbani ikiwa mbele ya mashabiki wake?

Nipashe hatuoni sababu ya Simba kushindwa kutumia vema uwanja wake wa nyumbani na kisha kwenda kushinda ugenini dhidi ya JS Saoura nchini Algeria.

Kwa upande wa mechi ya ugenini dhidi ya JS Saoura tunaamini inawezekana kwa sababu tayari Simba imeshacheza dhidi yao hapa nyumbani na kupata ushindi wa mabao 3-0.

Hivyo, licha ya kwamba Waarabu hao wanaonekana sasa kubadilika na watakuwa nyumbani, Simba wataingia uwanjani wakijiamini jambo ambalo linaweza kuchangia kupata ushindi. Kwa kutambua Simba inapeperusha bendera ya nchi katika michuano hiyo, Nipashe kama wadau wakubwa wa michezo, tunaitakia maandalizi mema na hatimaye kupata ushindi katika mechi zake tatu zilizobaki, mafanikio yakianzia dhidi ya Al Ahly Jumanne ya wiki ijayo. Kila la Kheri Simba.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com

BUSARA

KUONGELEA / MAENDELEO

**HAYAWI, HAYAWI, SASA YAMEKUWA!! HAPA NCHINI TUMEFIKA MAHALI AMBAPO WANANCHI WALIO WENGI WANAZUNGUMZIA MAENDELEO ZAIDI KULIKO KUCHIMBANA, KUKASHIFIANA, KUANGUSHANA NA KUPAKANA MATOPE. KWA KIASI KIKUBWA, KINACHOZUNGUMZWA SASA NI KAZI TU! TUSHIKE UZI HUO HUO.** NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

## Karia iangukie Chadema, usiliingize soka katika siasa

**MOJA** kati ya vitu vyenye nguvu ya umma duniani ni soka na siasa. Vitu hivi viwili vina uwezo mkubwa wa kuhamasisha watu wengi kwa muda mfupi tu.

Soka na siasa ni vitu viwili tofauti ambavyo kuna wakati vinafanya kazi pamoja kwa ajili ya kuhamasisha watu na kuwaleta pamoja, kujenga mshikamano na amani.

Lakini kwa namna yoyote ile soka na siasa havipaswi kulinganishwa kwa mfanano wowote ule kwa sababu kazi ya vitu hivi viwili huwa ni tofauti.

Lakini hivi majuzi Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania, Wallace Karia, aliwaonya wajumbe wa Mkutano Mkuu kuacha tabia za 'U-Tundu Lissu' kwenye soka akisisitiza hatowavumilia wenye tabia hizo.

Maneno hayo yameonekana kuwachefua baadhi ya watu na haswa Wanachadema wenyewe na viongozi wao.

Katika ufafanuzi wake Karia alisema hakuwa na nia mbaya, lakini kama maneno hayo yamewakera watu, basi anaomba msamaha.

Alisema alimfananisha Michael Wambura kuwa ana tabia za Ki-Tundu Lissu kutokana na kuzunguka kwenye vyombo vya habari kuikashifu TFF, kama ambayo Lissu anavyofanya huko nje ya nchi.

Tayari Chadema imemtaka Karia kumuomba radhi Lissu ambaye ni Mbunge wa Singida Mashariki na Mwanasheria Mkuu wa chama hicho, bila hivyo wametangaza moja ya mambo watakayofanya ni kuhamasisha wanachama wake kutoshiriki shughuli za TFF.

> **Tayari Chadema imemtaka Karia kumuomba radhi Lissu ambaye ni Mbunge wa Singida Mashariki na Mwanasheria Mkuu wa chama hicho, bila hivyo wametangaza moja ya mambo watakayofanya ni kuhamasisha wanachama wake kutoshiriki shughuli za TFF.**

Mimi nadhani Karia angeepuka jambo hili kwa kuchagua maneno ya kuongea. Wakati mwingine unatakiwa kuongea kimafumbo zaidi kuliko alivyokuwa wazi, kwa kuwa ninaamini Chadema kama vilivyo vyama vingine nao ni wadau wakubwa wa soka hapa nchini.

Karia angetafuta misamiati, nahau na mafumbo kulizungumzia jambo hili ili kutoleta mkanganyiko kama ambao tayari umeshatokea.

Ukiangalia kwenye mitandao ya kijamii, tayari jambo hili limekuwa kubwa, kila mtu anazungumza lake, kitu ambacho hakikuwa cha lazima sana na hakileti afya kwa soka letu.

Karia angeweza kabisa kumzungumzia moja kwa moja Wambura na si kumchanganya ama kumfananisha na mtu mwingine ambaye hausiki na soka.

Kama nilivyosema soka lina nguvu na siasa nayo ina nguvu, hivyo kila upande ukitaka kuvuta itakuwa tatizo katika soka letu.

Kutoshiriki shughuli za TFF unaweza kulichukulia kama ni kauli nyepesi, lakini ukiitazama kwa undani ina maana pana sana.

Chadema inaweza tu kuwashawishi wanachama na mashabiki wao wasihudhurie kwenye michezo inayosimamiwa nayo, ikiwamo timu ya Taifa, kitu ambacho kusema kweli hakitokuwa kizuri kwa mustakabali wa taifa letu.

Tunataka soka letu na timu yetu ya taifa iwalete pamoja Watanzania wote bila kujali itikadi zao za siasa, vyama, dini, rangi au kabila.

Kwa hili lililotokea, inabidi pande hizo mbili zifanye mawasiliano na kulimaliza jambo hili kwa mustakabali wa soka la Tanzania.

Soka litaendelea pale Watanzania wote watakapokuwa kitu kimoja bila kuwekeana vinyongo, hivyo chondechonde Karia mambo ya Ngoswe muachie Ngoswe mwenyewe, soka letu usiliingize huko kabisa, ukihitaji siasa achia ngazi nenda kapambane huko, lakini si kupitia mlango huo.

## BARUA/MJADALA

# *Pongezi Majaliwa ujenzi wa mji wa serikali Ihumwa-Dodoma*

*TUNAANZA kwa kutoa pongezi kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwa kuwabana wazembe wasiofuatilia majukumu yao.*

*Tunachukua nafasi hii kummwagia sifa nyingi Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Majaliwa kwa hatua yake mwafaka aliyoichukua mnamo siku ya Alhamisi Desemba 27, 2018, pale alipofanya ziara ya kushtukiza eneo la Ihumwa, kukagua ujenzi wa mji wa serikali.*

*Katika ziara ile Mheshimiwa Majaliwa hakusita kuonyesha kukerwa na utendaji kazi usioridhisha kwa baadhi ya makandarasi waliopewa kazi hiyo muhimu kwa taifa.*

*Je! Unaweza kuamini mkandarasi kulalamikia ukosefu wa tofali, nondo? Lalamiko hili ni aibu. Nchi, kama nchi haina uhaba hata kidogo wa saruji na nondo. Ni uongo tu wa makandarasi hao na ni aibu kwao.*

*Lakini pia jambo hili la utendaji dhaifu wa mradi huu ni lazima liwaangukie moja kwa moja baadhi ya mawaziri, makatibu wakuu, mkuu wa mkoa wa Dodoma na mkuu wake wa wilaya, wafuatilie.*

*Labda tu tuseme hii ni hujuma ya wazi dhidi ya viongozi wetu wakuu wapendwa na serikali. Mheshimiwa mkuu wa nchi, ametangaza rasmi atahamia Dodoma Januari 2019. Mtakuwa wapi nyinyi mawaziri wazembe pale Dk. Magufuli atakapowaweka kwenye mtego?*

*Ni ukweli usiopingika kwamba baadhi ya watendaji, mawaziri na makatibu wakuu hapo nyuma walikuwa hawajatembelea 'site' zao, yaani walikuwa 'hawazijui.' Sasa hivi ni aibu, hii ni fedheha, hii ni hujuma dhidi ya Mheshimiwa Rais.*

*Tunashukuru sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, amelishikia bango yeye mwenyewe. Hapo wapo baadhi ya mawaziri 'serious' lakini wengine ni shida. Sisi wakazi wa Dodoma tunasema, Magufuli ndiye kipenzi chetu nambari moja, hana wa mfano anazidi kutuongezea hamasa.*

*Imewasili ndege kubwa ya kisasa mno 'Dodoma-Hapa kazi tu.' Mnasemaje? Mwaka 2020 kwa kura zetu za 'Ndiyo' asilimia 98, asilimia 2 zitaenda kwa wakwepaji kulipa kodi "tunaowaona" Dodoma hii sasa. Wahujumu 'aliowakamata' Mheshimiwa Majaliwa, watupiwe jicho.*

***Ni sisi, Issa Mwenegoha Mganga Madeha***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Yanga inalea sakata la Kakolanya




**Na Adam Fungamwango**

HIVI sasa kila unapoamka na kwenda kwenye meza za magazeti, basi moja kati ya habari utakayoikuta ni sakata la golikipa Beno Kakolanya.

Kwenye mitandao ya kijamii, bado suala hili limechukua sura mbalimbali, kila mtu akilielezea kwa namna yake, wengine kishabiki na wengine wakiwa wanafuata mkumbo wala hawajui nini kilifanyika na kinachoendelea.

Kwa muda mrefu sana hili suala limekuwapo hadi limechosha kwenye masikio ya wapenzi na mashabiki wa soka.

Sakata hili linaanza kama ile hadithi ya kuku na yai nini kilianza. Ni kwamba Beno ana madai yake kwenye klabu ya Yanga, ikiwamo malimbikizo ya mishahara yake.

Kwa mujibu wake mwenyewe ni kwamba madai hayo yalikwenda mpaka ikapita miezi ambayo ipo kimkataba na baada ya hapo klabu inakuwa imevunja mkataba.

Viongozi wa Yanga nao wakaja na kudai kuwa kipa huyo ni mtovu wa nidhamu na mtoro kambini.

Kocha Mwinyi Zahera naye akadai hamhitaji kipa ambaye hana uzalendo kwani hata kama anadai malimbikizo yake, lakini asingeonyesha mgomo.

Msimamo wa kocha ni kwamba hamhitaji Kakolanya. Na Kakolanya naye ameandika barua ya kuvunja mkataba. Ukiangalia hapa, hata kama ni ndoa ya mke na mume, basi imevunjika.

Ni sawa kabisa na mume anamhitaji mke, lakini anamuogopa wazazi wake ambao hawamtaki hata kumuona. Mke naye hataki, amechoka anaomba talaka yake. Hapo ndoa hakuna.

Ni kwamba viongozi wa Yanga wanamhitaji Kakolanya, lakini hawana kauli yoyote juu ya kocha Zahera ambaye ameonekana kushika mpini. Zahera hamtaki Kakolanya na pia kipa huyo anaonekana kuchoshwa na mambo hayo, hivyo anaomba kuondoka.

Viongozi wa Yanga wamepokea barua, lakini wamedai wamepeleka kwa mwanasheria wao.

Mimi niliona kwa jinsi hali ilivyo kwa sasa, viongozi wa Yanga wala hawakuwa na haja ya kwenda kwa mwanasheria, bali kukutana na Kakolanya mwenyewe kuangalia uwezekano wa kuvunja mkataba kwa makubaliano bila upande wowote kulipa chochote, wakaachana kwa amani.

Viongozi wa Yanga hawawezi kumrudisha Kakolanya Yanga kwa lazima. Labda Zahera aondoke. Lakini je, kipa huyo naye kwa sasa yuko radhi baada ya yote yaliyotokea na lawama anazotupiwa?

Sasa viongozi wa Yanga wanavyolichelewesha sakata hili ni kwa manufaa ya nani? Au wanamkomoa Kakolanya kwa sababu wanajua hatocheza popote na pia nafasi yake Taifa Stars itakuwa finyu?

Kama hata ndoa inafika wakati haiwezi kuendelea tena, haiwezi kuwa ajabu kwenye suala hili la kimkataba.

Viongozi wa Yanga wanatakiwa kuliangalia suala hili kwa kutumia busara zaidi, ili kila upande uangalie maisha mengine. Wakiendelea kulilea na kutaka kuendelea kisheria inawezekana kukazuka mambo mengine ambayo yanaweza kuwa athari kwa mchezaji au klabu yenyewe ya Yanga.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED



# Mikataba mibovu

INATOKA UK. 2

taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini.

Kamati mbalimbali zilizoundwa na Rais John Magufuli na zile zilizoundwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuchunguza sekta za nishati na madini miaka miwili iliyopita, zilibaini kuwapo kwa changamoto ya mikataba mibovu katika sekta hizo.

Ratiba ya mkutano huo utaomalizika Ijumaa, inaonyesha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu nayo leo inawasilisha taarifa yake ya shughuli za mwaka 2018.

Taarifa ya kamati hiyo inatarajiwa kueleza hali ya miundombinu na changamoto zinazozikabili sekta za uchukuzi na ujenzi nchini.

Wiki iliyopita, kuwasilishwa taarifa za kamati nne; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

Bunge pia lilijadili na kupitisha miswada mitano ukiwamo Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2018, Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA).

Mingine ni Muswada wa Sheria za Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Namba 4) wa Mwaka 2018.

# Pinda ajitosa kumng'oa Msigwa

Na George Tarimo, IRINGA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ametaja mambo sita ambayo yamesababisha Chama Cha Mapinduzi (CCM), kupoteza Jimbo la Iringa Mjini.

Jimbo hilo linaongozwa na Mbunge wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mchungaji Peter Msigwa, huku akiwapa mbinu za kulikomboa mwaka 2020.

Alisema sababu ni makosa ya CCM wilaya na kama wanachama wenyewe wamesema 2020 watanyakuwa jimbo, lazima wafute yale yaliyosababisha awamu zilizopita wakashindwa.

Akiwa mlezi wa CCM Mkoa wa Iringa, Pinda, alisema hayo jana kwenye uzinduzi wa maadhimisho ya miaka 42 ya kuanzishwa kwa CCM.

Jambo la kwanza Pinda aliwataka kuacha makosa kwenye uteuzi wa wagombea wanakaa kwenye vikao na kujiangalia nani rafiki yao anafaa kugombea, na kwamba bila kuacha mazoea hayo yaleyale yatajirudia.

"Achaneni na kuteua na kujitizama walipo kwenye vikao, tazameni umma unaopiga kura, unasema nani watu wanamtaka safari hii. Wakati mwingine mnapuuza hili jambo mnaliona halina maana na kujifanya mnajua zaidi kuliko hawa wanaopiga kura," alisema Pinda.

Alisema kosa la pili ni viongozi wa juu kushindwa kushuka kwa wananchi na wanachama wa chini mfano viongozi wa mashina na matawi kwa lengo la kuwasikiliza na kujua matakwa yao wanayohitaji.

Waziri huyo wa zamani alisema leo atakutana na mabalozi wote wa mitaa ili kujadili namna ya kurejesha jimbo hilo kwa sababu wao wana majibu.

Tatu ni viongozi wa juu wa chama kutowapa heshima viongozi wa chini na hiyo inafanya CCM kupata tabu sana ya kupata watu wa kupiga kura siku ya uchaguzi na kwenda kujiandikisha kwa sababu mahusiano yao na wao hayapo.

"Mimi najua wana-CCM ni wengi kuliko chama chochote wanachotuhukumu

INAENDELEA UK. 26



Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya, Robert Mharamba (kulia), akizungumza wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Sheria mkoani Mbeya, katika stendi ya daladala ya Kabwe jijini humo. Katikati ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila na kushoto ni Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Joel Ngwembe. **PICHA: KENETH NGELESI**

# Kiama vigogo waliochukua mabilioni benki ya serikali

INATOKA UK. 2

binafsi na kampuni kwa lengo la ujenzi wa maghala ya kuhifadhi na kuchambulia pamba, ujenzi wa hoteli, ununuzi wa matrekta, ujenzi wa viwanda vya maji na kilimo cha mazao mbalimbali.

Alisema suala muhimu la ufuatiliaji ni kutaka kujua iwapo kweli wadaiwa hao walitekeleza malengo ya mikopo husika au ilikuwa ni dirisha la kukopa fedha kwa malengo yasiyokusudiwa.

Kaboyoka alisema kuwa, hivi karibuni Benki Kuu (BoT) imekuwa ikitekeleza wajibu wake wa kuzifunga, kuweka chini ya ufilisi na kuziunganisha baadhi ya benki nchini, ambazo uendeshaji wake umekuwa na changamoto hasa kuwa na mtaji chini, kinyume cha sheria, kunakoiweka hatarini TIB kuingia kwenye orodha hiyo.

"Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa TIB nayo pia inakabiliwa na madeni ya wadaiwa sugu wasiorejesha mikopo ya benki kwa wakati. TIB kumekuwa na 'non perfoming loans' (mikopo chechefu) hadi kufikia asilimia 33, wakati asilimia elekezi kwa mujibu wa BoT ni asilimia tano," Kaboyoka alisema.

"Ni muda mwafaka sasa kwa wadaiwa sugu kutakiwa kurejesha mikopo yao na kunusuru TIB isije kufilisika au kuwekwa chini ya usimamizi na BoT.

"Kampuni na watu binafsi wanaodaiwa wanajulikana na dhamana zao zinajulikana, hivyo ni vyema zoezi la kurejesha mikopo likafanyika haraka iwezekanavyo kwa kuzingatia sheria za nchi na mikataba husika.

"Hii ni pamoja na ukweli kuwa hali ya mikopo chechefu katika soko kwa sasa ni wastani wa asilimia 23."

Alisema hadi kufikia Septemba 30, mwaka jana, mikopo chechefu ambayo TIB ilikuwa inadai, ilifikia Sh. bilioni 251.89. Alisema mikopo hiyo ilikuwa na dhamana zenye thamani ya Sh. bilioni 550.83.

Kaboyoka alisema kamati yake imebaini mikopo chechefu iko katika makundi matatu ambayo ni mikopo isiyo safi, mikopo yenye shaka na mikopo inayohesabika hasara.

Taarifa ya ukaguzi wa mikopo chechefu ya TIB hadi kufikia Septemba 30, 2018, inaonyesha kuwa kundi la mikopo inayohesabika kama hasara linachukua karibia asilimia 69.72 ya mikopo chechefu yote (Sh. bilioni 175.35).

Alisema fedha hizo ni za umma ambazo iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa, zitapotea na kuisababishia serikali hasara.

# Repoa yashauri ukuaji uchumi

INATOKA UK. 3

Taasisi nyingine ambazo hupimwa katika ripoti hiyo kwa Tanzania ni Taasisi ya Tafiti za Kiuchumi (ESRF) na Uongozi Istitute.

Dk. Mmari alisema kinachosababisha taasisi hiyo kuwa bora Afrika ni kutokana na umahiri na ubora unaotokana na kuandaa utafiti wenye matokeo chanya katika maendeleo ya jamii.

"Sababu kubwa ni kufanya utafiti ambao unalenga maeneo makubwa ya maendeleo ya Tanzania, kufanya utafiti ambao ni 'relevant'(halisi) katika maeneo mbalimbali ya kisera na nchi imekuwa ikiuchukua na tumeona matokeo chanya katika maeneo ya maendeleo," alisema Dk. Mmari na kuongeza:

"Tulikuwa tukishirikishwa kuandaa sera mbalimbali...kwa mfano Mkukuta tangu 2004, lakini pia tukishirikishwa kuandaa mpango huu wa pili wa maendeleo. Kuna maeneo tuliyoyapendekeza yachukuliwe na serikali na kuwa sehemu ya mipango yake."

Dk. Mmari alisema Repoa imependekeza serikali kufanya uwekezaji katika miundombinu kwa lengo la kupunguza uwiano uliopo, na serikali hivi sasa inawekeza katika ujenzi wa barabara, viwanja vya ndege, viwanda, usafiri wa anga na umeme.

Aliongeza kuwa mambo yote ambayo serikali inayafanya ni muhimu katika kufanikisha ukuaji wa uchumi wa viwanda, katika sekta za kilimo na sekta nyingine za uchukuzi na mawasiliano.

Alisema pendekezo lingine ni katika suala la utawala bora na ushirikishwaji wa wananchi katika nyanja mbalimbali na kupambana na rushwa.

"Serikali ya awamu ya tano imechukua juhudi kubwa ya kupambana na rushwa na kuongeza uwajibikaji katika utendaji wa serikali na katika utoaji huduma, hili ndilo tumelishauri kwa muda mrefu na lipo kwenye mpango," Alisema Dk. Mmari.

Kuhusu ukuaji wa viwanda alisema: "Tuliainisha sehemu ambayo serikali iwekeze kwa sababu tunazo sehemu zenye rasilimali ambazo zinatupa faida...tunayo gesi, madini mengi, mbuga za wanyama na mifugo."

Alisema kuwa walipendekeza kuongezwa msukumo kuwekeza viwanda vinavyoongeza thamani ya mazao ya kilimo, madini na gesi na kupendekeza kuanzishwa viwanda vya nguo kwa sababu nchi inazalisha pamba ya kutosha pamoja na viwanda vya ngozi kwa sababu kuna mifugo mingi.

HABARI KITAIFA

## Chuo Bandari kununua mtambo wa bil. 1.5/-

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Bandari kilichopo chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), kimejipanga kupokea mitambo ya kisasa ya kufundishia ili kitoe mafunzo ya kisasa zaidi.

Kwa kuanzia, TPA imeshaingia mkataba wa kununua mtambo mkubwa wa kufundishia uendeshaji wa vyombo vyote vya kupakia na kupakua mizigo bandarini (Full Mission Crane Training Simulator).

Mwenyekiti wa Bodi ya Magavana ya chuo hicho, Deusdedit Kakoko, alisema jijini Dar es Salaam kuwa, mtambo huo unatarajiwa kugharimu takribani Sh. bilioni 1.5, wakiamini utakuwa na manufaa makubwa kwa chuo.

"Mtambo huu utafungwa ndani ya miezi sita kuanzia sasa na kuanza kutumika mwanzoni mwa mwaka ujao wa fedha," alisema.

Kakoko ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu wa TPA, alisema mamlaka itaendelea kuwekeza katika vifaa ili kukifanya chuo hicho kuwa cha kisasa zaidi.

"Chuo kimezindua tovuti pamoja na mfumo wa Tehama Students Information Management System," alisema Kakoko na kuongeza kwamba, juhudi hizo zinalenga kuimarisha na kusimamia ubora wa huduma zitolewazo na chuo.

Mkuu wa Chuo cha Bandari, Dk. Joseph Kakeneno, alisema chuo kinakusudia kutoa stashahada za juu na shahada ya kwanza ya kuongeza ujuzi wa utendaji kazi (Competence Based).

Dk. Kakeneno alisema shahada hizo wanazotarajia kuzianzisha katika kipindi cha miaka mitatu ijayo, ni katika taaluma zinazohusiana na huduma za meli, maji na menejimenti ya shughuli za bandari.

Alisema kwa sasa chuo kina karakana nne za mafunzo kwa vitendo katika fani za Mechanical, Civil, Automotive, Electrical na maabara moja ya kompyuta na maktaba moja.

# RC Gaguti aagiza mwisho vitambulisho wamachinga

**Na Mwandishi Wetu,** BUKOBA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, amegawa vitambulisho 35,000 vya awamu ya pili vya wafanyabiashara wadogo na kuwaagiza watendaji kuhakikisha vitambulisho hivyo vinagawiwa vyote ifikapo mwisho wa mwezi huu.

Mkuu huyo wa mkoa amesema katika tathmini iliyofanyika kuhusu awamu ya kwanza ya usambazaji wa vitambulisho hivyo, Mkoa wa Kagera ulishika nafasi ya sita kati ya mikoa 26 baada ya kugawa asilimia 65 ya vitambulisho 25,000.

Gaguti aliziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinakusanya takwimu za wafanyabiashara wote wakubwa, wa kati na wadogo ifikapo Februari 15, 2019.

Aliongeza kwamba takwimu hizo ziwe zimewasilishwa ofisini kwake, lengo likiwa ni kuhakikisha kila mwananchi anayetoa bidhaa yoyote na kupokea fedha anatambuliwa na kulipa kodi au tozo stahiki za serikali.

Hafla hiyo fupi iliwashirikisha Wakuu wa Wilaya saba za Mkoa wa Kagera, Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na Manispaa, Wenyeviti wa Halmashauri na Meya wa Manispaa ya Bukoba na Watendaji wa Kata.

Aliwataka watendaji hao watoe changamoto zinazowakumba katika ugawaji wa vitambulisho hivyo.

Walisema changamoto kubwa ni elimu kwa kuwa wananchi wengi na baadhi ya watendaji hawajui ni mfanyabiashara yupi anatakiwa kupata kitambulisho na yupi hastahili, hivyo wakaitaka TRA itoe elimu zaidi.

Changamoto nyingine ni suala la mfanyabiashara mdogo kuwa na namba ya utambuzi ya mlipa kodi ya TRA (TIN) wakati biashara yake ni ndogo na hastahili kupata kitambulisho cha mfanyabiashara mdogo wakati mtaji wake ni mdogo haufikii kiwango cha Shilingi milioni 4 kwa mwaka.

Meneja wa TRA Mkoa wa Kagera, Adam Ntoga, alisema mfanyabiashara mdogo anayestahili kupata kitambulisho ni yule ambaye mauzo yake kwa siku hayafikii Shilingi 11,000.

"Hata kama mfanyabiashara ana mtaji wa Shilingi 5,000, lakini anauza bidhaa zake kwa siku na kupata Shilingi 11,000 au zaidi kwa siku huyo hastahili kupata kitambulisho, kinachoangaliwa hapa si mtaji wa mfanyabiashara alionao bali ni mauzo yake," alifafanua Ntoga.

Katika hatua nyingine, Gaguti alitoa onyo kwa wafanyabiashara ambao walidanganya na kupokea vitambulisho wakiwa tayari wametambuliwa na mfumo wa ulipaji kodi wa TRA.

Aliongeza kwamba anayo majina sita na hatua kali za kisheria zitachukuliwa mara moja. Pia aliwaonya watendaji wa kata ambao wanaandika barua kuwatambulisha wafanyabiashara kuwa mtaji wao ni mdogo kuwa waache mara moja.



Ofisa Mawasiliano wa TBL, Amanda Walter, akimvisha 'reflector' jaketi mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Msewe jijini Dar es Salaam, wakati kampuni hiyo ilipokabidhi msaada wa 'reflectors' kupitia kwa Jeshi la Polisi kwa ajili ya shule za msingi 200 na kushiriki kutoa elimu ya usalama barabarani kwa wanafunzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# YARA yasambazia wakulima chokaa, elimu afya ya udongo

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya mbolea ya YARA Tanzania imehamasisha wakulima kutumia chokaa na inasambaza maarifa ya kilimo bora na hasa elimu ya afya ya udongo kwa wakulima hao katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Akizungumza jijini Dar es Salaam kufutia utilianaji saini hivi karibuni kati ya YARA, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Uyole (TARI), Bwana Shamba Mkuu wa YARA, Peter Assey, alisema makubaliano hayo yana maana kubwa kwa kampuni yake kwa kuwa yanalenga kumwinua mkulima kwa kumpa ufahamu mpana juu ya mambo mbalimbali ikiwamo upimaji wa afya ya udongo, ili kuchochea uzalishaji wa mazao anayolima.

"Hii ni hatua nyingine muhimu kwa maendeleo ya mkulima hapa nchini kwa kuwa makubaliano haya yataleta tija kubwa kwa taifa kwa kuwa yatakomboa wakulima wengi kwa kukuza kipato chao. Lakini jambo muhimu zaidi ni kufikia ya azima serikali ya kuifanya Tanzania iwe na uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025," alisema Assey.

Alisema YARA, TARI na TADB zimejipanga kutoa elimu ya udongo kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji katika kilimo na kukuza pato la wakulima.

"YARA tumekuwa tukipima udongo kabla ya kugawa mbolea, lakini tumegundua kiwango cha tindikali kipo chini sana hasa katika maeneo ya Nyanda za Juu Kusini. Hivyo kwa kushirikiana na TARI tutatoa elimu juu ya matumizi ya chokaa ambayo huongeza kiwango cha tindikali kwa kutumia wataalamu wa ndani ili kuboresha uzalishaji," alisema Assey.

Meneja Biashara wa Yara Nyanda za Juu Kusini, John Meshack, amekaribisha makubaliano ya taasisi hizo tatu na kusema anatarajia utekelezaji wake changamoto ambazo zimekuwa zikiibuliwa na utafiti wa YARA.

Meshack alisema msimu huu kampuni yao imejitahidi kusambaza chokaa ili kuongeza tindikali ardhini na wanaamini uzalishaji utaongezeka.

"Tumesambaza chokaa katika maeneo mengi ili kuboresha afya ya udongo na tunatarajia ongezeko la uzalishaji katika Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini," alisema Meshack.

HABARI KITAIFA

# TFS, NLUPC zatekeleza agizo la JPM

**Na Elizabeth Zaya**

AGIZO la Rais John Magufuli la kuzitaka mamlaka zinazoshirikiana katika masuala ya uhifadhi kuweka mipaka katika hifadhi zote nchini, limeanza kutekelezwa baada ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (NLUPC), kuanza kupima ardhi hiyo katika baadhi ya maeneo ya hifadhi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alisema kufanyika kwa kazi hiyo kutasaidia kwa kiwango kikubwa kukabiliana na changamoto ya uvamizi wa misitu katika maeneo mbalimbali ya hifadhi nchini.

Alisema upangaji huo umeshaanza katika vijiji 11 vilivyopo katika baadhi ya wilaya katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

Alisema katika kutekeleza kazi hiyo mwaka huu Sh. bilioni 1.5 zimetengwa kwa ajili ya kupanga matumizi bora ya ardhi katika vijiji 100 vinavyozunguka misitu.

Alisema kazi hiyo ya upangaji wa matumizi ya ardhi itafanyika kwa ushirikiano kati ya TFS na NLUPC na lengo ni kuhakikisha wanamaliza migogoro yote ambayo imekuwa ikiibuka katika hifadhi nyingi.

Alisema huo utawawezesha pia wananchi wanaoishi kwenye vijiji hivyo kupanga matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyao na hata kusaidia kupunguza uvamizi kwenye misitu.

"Mipango bora ya ardhi, pia itasaidia wananchi kuondokana na kilimo cha kuhama hama ambacho kwa kiasi kikubwa huchangia kupunguza maeneo ya misitu, tayari upangaji huo umeshaanza katika vijiji 11 vilivyopo kwenye baadhi ya wilaya katika mikoa ya Lindi na Mtwara," alisema Prof. Silayo.

Alisema TFS inatarajia kupandisha hadhi misitu mitano ndani ya mwaka huu kuwa hifadhi za mazingira asilia ili kulinda baionuai iliyoko katika misitu hiyo.

Mkurugenzi wa NLUPC, Dk. Stephen Nindi, alisema upangaji wa matumizi ya ardhi ni njia bora ya kuondoa migogoro kati ya wananchi na wahifadhi wa misitu.




Meneja wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Aidan Komba (kushoto), akimkabidhi Sara Saimon, mfano wa hundi ya Shilingi milioni mbili baada ya kuibuka mmoja kati ya mawakala wa Tigo Pesa aliyefanya vizuri katika promosheni inayojulikana kama Chifu wa Mawakala iliyofanyika Desemba mwaka jana. Anayeshuhudia ni Meneja wa Tigo Mkoa wa Dodoma, Gideon Moris. **PICHA: PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanajeshi mstaafu apotea mazingira tata

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAJESHI mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Ibrahim Sad (58), ambaye ni mkazi wa Kibaha Mkoa wa Pwani, anatafutwa na familia yake baada ya kutoonekana kwa wiki kadhaa.

Kwa mujibu wa familia yake, Ibrahim aliaga mara ya mwisho kwamba anaelekea Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), jijini Dar es Salaam Januari 4, mwaka huu na tangu wakati huo hakurudi nyumbani.

Mdogo wa mstaafu huyo, Sad Sad, ambaye alifika kwenye ofisi za Nipashe zilizopo Mikocheni jana, alisema mke wa Sad, alisema mume wake aliaga Januari 4, mwaka huu kuwa anakwenda Hospitali ya Muhimbili kupima macho, lakini tangu wakati huo hajarudi nyumbani na simu yake haipatikani.

Sad alisema kaka yake ambaye alistaafu Februari mwaka jana hajaonekana nyumbani kwake Kibaha hadi jana na wala simu yake haikupatikana.

"Mke wa kaka yangu alinipigia simu kuniuliza kama kaka amekuja kwangu, nilianza kumtafuta kwa ndugu jamaa na marafiki zake na nilikwenda ofisi ya kazi Lugalo alikokuwa akifanya kazi kabla ya kustaafu kujua kama alifika huko kote hayupo," alisema.

Sad alisema tayari ameshatoa taarifa kituo cha Polisi Kibaha na kupewa RB/646/2019.

Kijana huyo ameomba kwa yeyote mwenye taarifa za kaka yake apige simu 0657 850788 au 0753 555078 au azifikishe kituo chochote cha polisi.

# Kampuni yakunwa wakulima kusaidiwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Usambazaji wa Mbolea ya Petrobena East Africa Ltd, imepongeza makubaliano yaliyofanywa kati ya Kampuni ya mbolea ya YARA

Tanzania, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzinia (TADB) na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Uyole (TARI) katika kufanya utafiti wa afya ya udongo lengo likiwa kuongeza uzalishaji na kuleta mageuzi katika sekta kilimo.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Peter Kumalilwa, alisema kampuni yake imejipanga kushiriki kikamilifu katika kuchagiza mageuzi kwenye sekta ya kilimo kwa kumfikishia mkulima pembejeo kabla ya msimu wa kilimo kuanza.

"Makubaliano hayo yataleta maana zaidi kama elimu itamfikia mkulima juu ya umuhimu wa kupima afya ya udongo kabla ya msimu wa kilimo ili kutambua zao gani linafaa katika eneo lake na mbolea aina gani na kwa kiasi gani atumie shambani kwake," alisema.

Alisema kwa kufanya hivyo, mkulima atakuwa amewezeshwa kufikia malengo yake kwa kuongezeka kwa tija katika uzalishaji kutokana na kufata kanuni za kisasa za kilimo ikiwamo kupima afya ya udongo.

"Zoezi hili litarahisisha kazi kwa upande wa usambazaji mbolea kwa wakulima, kwa kuwa watakuwa wanajua ni aina gani ya mbolea zinahitajika na wakulima na hivyo kuchochea uzalishaji," alisema.

Kumalilwa pia alisema kampuni yake ilishaanza kutoa elimu kwa wakulima mkoani Morogoro juu ya matumizi bora ya pembejeo, hivyo kufuatia makubaliano yaliyofanyika yameiongezea nguvu zaidi kampuni yake kutoa mchango stahiki katika kilimo.

Alisema kampuni yake imeshasambaza mbolea mkoani Tabora na Morogoro kwa wakati na kusababisha kutokuwapo kwa malalamiko kutoka kwa wakulima juu ya mbolea na zoezi hilo litakuwa endelevu katika kipindi chote, ili kumwondolea mkulima vikwazo katika kufikia malengo yake.

Aidha, Kumalilwa aliishukuru serikali ya Rais Dk. John Magufuli, kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kuhakikisha mkulima nchini anafanya kilimo cha kisasa chenye tija.

Ofisa Mazingira na Kilimo Endelevu kutoka Kituo cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT), John

Banga, alisema makubaliano hayo ni utekelezaji kwa vitendo wa Mpango wa Awamu ya Pili wa Maendeleo ya Kilimo Tanzania(ASDP -II) hali itakayochagiza maendeleo na ukuaji wa sekta ya kilimo hapa nchini.

Alisema SAGCOT itaendelea kushirikiana na wadau wote katika sekta ya kilimo na mifugo, lengo likiwa kumwinua mkulima kutokana na kufanya kilimo cha mazoea na kufanya kilimo cha biashara na kutoa mchango katika ukuaji wa uchumi.



Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara, Tumaini Magessa, akitoa maagizo ya serikali wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# DC afafanua uvamizi maeneo ya hifadhi

**Na Mwandishi Wetu,** KITETO

MKUU wa Wilaya ya Kiteto, Mhandisi Tumaini Magessa, amewataka wakulima na wafugaji kuacha kuvamia maeneo ya hifadhi kwa kupotosha kauli ya Rais John Magufuli aliyoitoa hivi karibuni kuhusu vijiji 366 vinavyopakana na hifadhi.

Alisema hayo wakati akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo, mwishoni mwa wiki.

Alisema baadhi ya wafugaji na wakulima hawakuelewa ipasavyo taarifa hiyo, hivyo kusababisha upotoshwaji.

Alisema baada ya taarifa hiyo kutolewa baadhi ya wafugaji na wakulima walijiandaa kulima na kufugia mifugo kwenye maeneo ya hifadhi, kitendo ambacho kitasababisha migogoro upya.

"Kwenye hivyo vijiji 366 vilivyotajwa na Rais Magufuli na kunufaika na tamko hilo, sisi Kiteto tuna vitongoji viwili pekee, sasa hao wengine wasiokuwapo wasijiingize huko," alisema Mhandisi Magessa.

Alisema utaratibu ulishawekwa vizuri juu ya maeneo hayo na wao kama serikali ya wilaya hawatakubali kuona watu wachache wanawaingiza kwenye migogoro.

Diwani wa Kata ya Partimbo, Paul Tunyoni, alisema Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto linapaswa kumpongeza Rais Magufuli kwa kuwajali wafugaji na wakulima.

Alisema kauli ya Rais Magufuli ya kuwajali wanyonge na kuhakikisha jamii ya wafugaji na wakulima wanafaidi raslimali zilizoko ni jambo la kupongezwa.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Kiteto, Emmanuel Papian, alisema Pori la Akiba la Mkungunero linatambulika kisheria, hivyo baadhi ya viongozi wasipotoshe hilo.

Alisema kumekuwapo na wapotoshaji juu ya kauli ya Rais Magufuli kuhusu sehemu zenye migogoro ya hifadhi na jamii inayowazunguka.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Lairumbe Mollel, alisema wananchi wanapaswa kuwa watulivu wakati huu, ambapo serikali inaweka utaratibu vizuri.

Alisema wananchi wote wanapaswa kusubiri ili uhakiki ufanyike kwa ushirikishwaji wa uwazi kuliko kuingia sehemu zisizoruhusiwa na kuzua migogoro upya.

Januari 15 mwaka huu Rais Magufuli aliagiza vijiji 366 vilivyoainishwa kuwapo ndani ya hifadhi nchini visiondolewe katika maeneo hayo.

# Wadau walia na tathmini ya kukadiria madini

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WADAU wa madini mkoani Manyara, wameishauri serikali kuangalia upya namna ambavyo wachimbaji wanavyofanyiwa tathmini ya madini yao ambayo itaendana na thamani ya madini na siyo kuwakadiria kwa lengo la kuwaumiza.

Ushauri huo waliutoa mwishoni mwa wiki wakati wakichangia kwenye mkutano wa kujadili Rasimu ya Kanuni za Masoko ya Madini 2019, uliofanyika ofisi ya mkuu wa mkoa na kuongozwa na Mkuu wa Mkoa, Alexander Mnyeti.

Wakichangia mkutano huo, walisema wanasikitishwa na uthaminishaji wa madini yao wanaofanyiwa wakidai hauendani na thamani ya madini yao.

Walisema tathmini inafanywa kwa kukadiriwa gharama kubwa na wanapoenda kuuza wanauza kwa bei ndogo. "Suala la tathmini bado ni tatizo kwa wachimbaji, linaumiza sana, mfano mimi nilikuwa na madini yenye thamani ya Sh. 300,000, lakini nilikadiriwa Sh. milioni tatu na wengine unakuta ana madini ya Sh. milioni mbili anakadiriwa Shilingi milioni 10, akienda kuuza hazifiki, anapata hasara," alilalamika Joseph Mwanga.

Katibu wa Wachimbaji Mkoa wa Manyara, Thomas Ombede, alishauri tathmini ya bei elekezi iwe inafanyika kwa kuangalia bei ya ndani na siyo bei ya nje, kwa kuwa zinapotumika bei za madini za nje zinawaumiza wachimbaji. Alishauri pia yajengwe masoko ya madini katika maeneo ambayo yana madini ili kuwaondolea usumbufu wa kutafuta masoko wachimbaji, lakini kwa kufanya hivyo kutasaidia kuimarisha soko la madini la ndani na kuepusha utoroshaji nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Tanzanite, Money Yusuph, alipinga kipengele kilichomo kwenye kanuni kinachowataka wachimbaji kuhifadhi madini yao kwenye maghala ya umma akisema wapo wachimbaji ambao wakishayapata madini hawahitaji kuyauza kwa wakati huo, maana wengine wanasubiri bei na wengine wanaweza kuyahifadhi kwenye makumbusho yao, ili wageni wakiwa wanakuja kutoka nje waje waone na hivyo wachimbaji wanaweza kuamua iwe hivyo.

Mchimbaji mwingine Zephania Joseph, alisema katika sekta hii suala la utoaji wa vibali bado ni tatizo kubwa, hivyo aliishauri serikali kuweka utaratibu mzuri wa kuvipata vibali hivyo kwa muda usiozidi siku tatu, huku akilaumu kuwa eneo la ukadiriaji bado ni shida kwa wanakadiria kwa bei kubwa. Naye Ofisa Madini Mkoa wa Kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima, alisema sababu ya utoroshaji wa madini ni kukosa soko, hivyo alisema kwa mujibu wa rasimu hiyo, masoko ya madini yataanzishwa kwenye maeneo ambayo yana shughuli za madini.

"Mtu yeyote hataruhusiwa kwenda kuuza madini sehemu yoyote anayotaka badala yake atauza madini yake kwa njia ya mnada katika eneo husika lililopangwa na kanuni zimeweka utaratibu wa namna ya kuhifadhi madini kwenye maghala kabla ya kufanyika mnada.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, alisema wakati kanuni zinaandaliwa aliwataka wakurugenzi kuendelea kujenga vituo vya kununua na kuuzia madini, huku akiwataka wachimbaji kuwa na tabia ya kulipa kodi.

# Wiki ya Sheria yatoa elimu wakazi Longido

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

WAKAZI wa Kata ya Namanga, Orbomba na Olmolog wilayani Longido, wamejengewa uwezo kuhusu elimu ya sheria mbalimbali zikiwamo za haki za mtoto na mirathi, ikiwa ni maadhimisho ya Wiki ya Sheria.

Hakimu wa Mahakama ya Wilaya Longido, Aziza Temu, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwapa elimu wananchi namna ya kutambua haki zao na kuzisimamia.

"Wananchi wengi hawafahamu sheria na wengi wanashindwa kudai haki zao kwa sababu hawajui utaratibu upoje, wamebaki kukosa haki zao," alisema.

Alisema pamoja na wananchi wengi kutokufahamu sheria lakini pia wanakabiliwa na matatizo mengi ndani ya jamii pasipo wao kujua mahakama ipo kwa ajili ya kutatua changamoto zao.

"Kauli mbiu ya mwaka huu ni "Utoaji haki kwa wakati, wajibu wa mahakama na wadau."

Aidha, alieleza maadhimisho ya Kilele cha Siku ya Sheria ni Februari 6, ambayo yatakutanisha wadau na watu wa sheria kwa pamoja na kuendelea kupeana elimu mbalimbali juu ya sheria.

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Namanga, Shila Mkoma, alisema changamoto kubwa katika Kata ya Namanga ni ndoa zisizo rasmi pamoja na watoto kukosa matunzo kutoka pande zote mbili za wazazi wao.

Alisema amekuwa akipata malalamiko mengi ambayo ni malalamiko sugu kwa baadhi ya wanaume kukataa kuwajibika kuwatunza watoto wao, kwa sababu zisizo za msingi, lakini sheria iko wazi kabisa juu ya mzazi asiyewajibika kutunza mtoto.

Alieleza ni haki ya mtoto kupata matunzo, kupewa elimu, kupewa uhuru wa mawazo na hata kucheza, na ni wajibu wa mzazi kuhakikisha mtoto anapata mahitaji yake muhimu kwa wakati na mzazi atakayeshindwa kutekeleza hayo anaweza kupata adhabu ya kifungo au kulipa faini.

"Kama mzazi ameshindwa kutimiza jukumu lake kwa mtoto chini ya miaka 18 sheria inasema wazi kulipa faini ya Sh. milioni 5 au kwenda kutumikia kifungu miezi 6, wakati mwingine sheria inaruhusu vyote kufanyika kwa pamoja," alisema.

Alifafanua kama mtoto ana miaka zaidi ya 18, lakini yupo masomoni sheria bado inambana mzazi kutekeleza majukumu kwa mtoto huyo ikiwamo kuhakikisha anapata elimu ipasavyo pamoja na mahitaji mengine muhimu.

Akizungumzi kuwapo kwa malalamiko kwa baadhi ya wanaume kukwepa kutoa matumizi kwa watoto kwa kile kinachodaiwa wazazi hao kutengana, na kusema hata kama wazazi mmetengana ni jukumu la mwanaume kuendelea kulea mtoto.

"Kuna matunzo ya mke na mtoto endapo ndoa haijavunjwa, kama mama akiwasilisha kesi ya matunzo, ndoa ikivunjwa suala la matumizi au matunzo kwa mtoto ni haki kutoa," alidai.

Naye Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Longido, Andrew Hayuma, alisema kumekuwa na migogoro mbalimbali ndani ya jamii ikiwamo kugombania mali zilizoachwa na mzazi au wazazi na aliwataka watu wote kujenga utamaduni wa kuandika wosia na kuteua msimamizi au wasimamizi wa mali wangali bado hai kupunguza migogoro ya mirathi.

Alieleza kesi zinakuwa nyingi juu ya kurithi mali kutokana na wazazi wengi kutokutoa tamko pindi wawapo hai, juu ya warithi au msimamizi wa mirathi na kubwa zaidi wakati mwingine unakuta wosia ulioachwa ni wa mdomo (pasipo maandishi), lakini matamko hayo hayana ushahidi.

# Balozi wa China ampa tano JPM

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BALOZI wa China nchini, Wang ke, amesema serikali ya nchi yake inaridhishwa na utendaji kazi wa Rais John Magufuli, katika miradi ya maendeleo na usimamizi wa rasilimali za taifa kwa faida ya Watanzania wote,

Balozi Wang ke ,alitoa kauli hiyo baada ya kukabidhi mradi wa choo cha kisasa chenye matundu 16, manane kwa ajili ya wanaume na manane kwa ajili ya wanawake katika Shule ya Msingi ya Msinga, iliyojengwa kwa msaada wa nchi yake ambayo ilitoa Shilingi milioni 32.

Alisema Rais Magufuli kwa miaka mitatu iliyopita amefanya kazi kubwa katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ikiwamo sekta ya elimu na afya.

"Ingawa serikali yake imetekeleza miradi 25 katika mikoa 15 ukiwamo mkoa wa Kilimanjaro, lakini serikali yangu itaendelea kutafuta fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ya wananchi wa Tanzania katika kuunga mkono juhudi za Rais," alisema Balozi Ke.

Akikabidhiwa vyoo hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, alisema serikali imejipanga katika kuhakikisha miundombinu inayokabidhiwa ni endelevu na ikiharibika basi iweze kufanyiwa marekebisho kwa haraka bila kuwasubiri wafadhili.

Alisema kwa wanafunzi ni wajibu wa walimu kuwafundisha matumizi bora ya choo cha kisasa ambacho wanaweza kutumia kwa urahisi zaidi kama lengo la kudumu.

Warioba alisema halmashauri itatoa 1/5 ya mapato ya kila mwaka kwa ajili ya ujenzi wa choo cha mwalimu na kuwashukuru walimu na wakazi wa eneo hilo kusimamia ujenzi.

Naye Naibu Mkurugenzi, Idara ya Kupanga Fedha na Utawala katika Kituo cha Mambo ya Nje, Uhusiano (CFR), Balozi Innocent Shiyo, ambaye alisoma katika shule hiyo, alisema kiasi kilichobakia kitatumika kujenga choo cha mwalimu na kwamba wanafunzi waliosoma shule hiyo wataendelea kusaidia.

Maria Ernest, mwanafunzi wa darasa la sita katika shule hiyo, alisema kujengwa kwa vyoo hivyo vya kisasa kutasaidia kuleta mabadiliko katika wingo vya ufaulu wa masomo.

Mwalimu Mkuu wa Shule Msingi Msinga, Pancrasia Tesha, alimshukuru balozi huyo akiongeza kwamba shule bado inakabiliwa na changamoto ikiwa ni pamoja na ukosefu wa bwalo, veranda ya kusaidia wanafunzi mahali pa kukaa wakati wa mvua pindi wanapotoka madarasani.




Mkurugenzi wa Mikopo wa Benki ya Biashara ya DCB, Isidory Msaki (kushoto), akifungua 'champaigne', huku baadhi ya maofisa wa benki hiyo wakishangilia, katika hafla ya wafanyakazi hao kusherehekea kumaliza msimu wa uuzaji wa hisa za benki hiyo uliyoanza Novemba 12 mwaka jana na kuhitimishwa Januari 31 mwaka huu. Hafla hiyo ilifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto kwake ni Mkurugenzi Mtendaji, Godfrey Ndalahwa, Mkurugenzi wa Fedha, Zacharia Kapama na wafanyakazi wengine. **MPIGAPICHA WETU**

# Vijana waitwa kugombea mitaa 2020

**Mary Mosha na Paul William,** MOSHI

VIJANA wametakiwa kutumia fursa ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwa lengo la kutatua matatizo mbalimbali yanayowakabili.

Hayo yalisemwa na Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Taifa, kupitia vijana wa Mkoa wa Kilimanjaro, Zacharia Katikilo, ambapo alisema vijana wengi wamekuwa wakirudi nyuma katika kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Katikilo alisema serikali ya awamu ya tano imeonyesha kuwathamini vijana kwa kuwapa nafasi mbalimbali za uongozi na wameweza kuzitumikia vyema na kuwataka sasa kutojirudisha nyuma katika kugombea.

"Vijana tumekuwa tukishindwa kujiamini unapofika muda wa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya serikali, sasa yupo ambaye anatuamini vijana, hivyo hatupaswi kurudi nyuma, tunapaswa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kuanzia serikali za mitaa," alisema Katikilo.

Alisema vijana wanakabiliwa na changamoto mbalimbali likiwamo tatizo la ajira na kuwataka vijana kushika nyazifa za uongozi ili kupambana na matatizo ambayo yamekuwa sugu nchini.

Akizungumzia suala la makundi ndani ya CCM, mjumbe huyo alisema kuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa ameonyesha dhamira ya kuchukizwa na makundi ndani ya chama hicho na kuwataka wanachama kuepuka makundi ili kuwapata viongozi sahihi watakaowatumikia wananchi.

## Waiomba serikali kuziangalia mila

**Na Mary Mosha,** SIHA

WANANCHI wa Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro wameiomba serikali kuingalia kati mila na desturi zinazowakandamiza wanawake na watoto hasa ukeketaji.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya kinamama hao walisema, matatizo ya ukeketaji kwa Wilaya ya Siha bado ni kitendawili kisichoteguka kutokana na wanajamii hao kuwakeketa watoto wadogo.

Evaline Moleli, kutoka kata ya Karansi, alisema wapo baadhi ya wauguzi katika hospitali mkoani Kilimanjaro ambao wamekuwa wakipewa rushwa na kuwakeketa watoto wenye umri chini ya miaka 3.

Alisema hali hiyo inasababisha matatizo makubwa hasa wakati wa kijifungua ikiwamo uvujaji wa damu na hatimae wengine kupoteza maisha.

Safina Mhamed, alisema miongoni wa mila na desturi zinazomwathiri mwanamke katika baadhi ya makabila ni ukeketaji ambao umekuwa ukifanyika kwa njia za siri katika vituo vya afya na zahanati.

"Tunaiomba serikali ya asasi na kiraia kuungana katika kuelimisha hasa jamii za wafugaji na kuwachukulia hatua kali wale wote watakaobainika kufanya vitendo kama hivyo," alisema Safina. Msele Emanuel, alisema bado elimu ni ndogo kwa wanajamii juu ya masuala ya ukeketaji na madhara yake ili kuepukana na matatizo kwa vizazi vijavyo.

Naye mratibu wa Nafgem Tanzania, France Selasin, alikiri kuwapo kwa ukeketaji katika Wilaya Siha, hasa katika kata za Naibili, Karansi, Lekrumuni, Orkolili, Ngarinairobi na Donyomoro na kusema kuna unaofanywa kwa siri mkubwa na wanafanyiwa watoto wadogo ambao hawawezi kujieleza.

"Katika Wilaya ya Siha tatizo hili bado ni kubwa ambalo serikali inapaswa kuliangalia kwa umakini katika kuhakikisha wanaweka sheria kali zitakazowabana wahusika watakaobainika kuingia kwenye makosa mbalimbali yakiwamo ya ukatili kwa kinamama na watoto," alisema Selasini na kuongeza:

"Tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuanzisha mpango maalumu wa kuielimisha jamiii juu ya ukeketaji na kuanzisha mpango maalumu wa kutoa elimu kila mara, ili kuhakikisha wanakubali kubadilika... pia adhabu kali zitolewe juu ya wote watakaobainika kutenda vitendo hivyo."

Nipashe
# Spotika
NIPASHE JUMATATU FEBRUARI 4, 2019



**SIMBA ILIVYOJISULUBU MISRI UK.18**

## PAMBANA...




Eden Hazard akipambana kuunasa mpira dhidi ya beki wa Huddersfield Town (chini), kwenye mechi Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Stamford Bridge juzi na Chelsea kushinda kwa mabao 5-0. **HABARI UK. 30**

### ISIKUPITE

GONZALO Higuain amekuwa mchezaji wa kwanza Chelsea kufunga mara mbili katika mechi yake ya kwanza uwanja wa nyumbani [akifanya hivyo dhidi ya Huddersfield juzi] tangu Mario Stanic alipofanya hivyo dhidi ya West Ham Agosti 2000.

## MICHEZO




# SABABU TATU KWA NINI HIGUAIN HATAFANIKIWA

**LONDON,** England

MCHEZAJI Gonzalo Higuain mwenye umri wa miaka 31 ni nyota wa kimataifa wa Argentina, aliyesajiliwa kwa mkopo pale Chelsea akitokea AC Milan wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari. Ulikuwa ni uhamisho uliotarajiwa na anatazamiwa kumsaidia Maurizio Sarri kuipaisha Chelsea. Chelsea hadi sasa ina pointi 50 katika mechi 24 za Ligi Kuu ya England walizocheza.

Mshambuliaji wa Chelsea, Alvaro Morata alikuwa kwenye kiwango kibovu msimu huu na alifunga mabao 24 tu katika mechi 72 alizoichezea timu hiyo.

Olivier Giroud, mshambuliaji wao mwingine, amecheza mechi 44 kwa kipindi chote alichokaa hapo na kufunga mabao 10. Na baada ya Chelsea kuona kwamba hawana mtu wa kuwafungia mabao, wakaamua kumchukua mkongwe huyo wa Argentina.

Hata hivyo, muunganiko wa Higuain na Sarri, kocha wake wa zamani akiwa pale Napoli, unaweza usilete mafanikio makubwa zaidi kwa Chelsea. Hapa tunazichambua sababu tatu kwa nini Higuain atakuwa na wakati mgumu pale kwenye dimba la Stamford Bridge:

**1. Kuwa mpya kwenye EPL**

Higuain amezichezea klabu nyingi kubwa kama vile Real Madrid, Napoli, Juventus na AC Milan katika maisha yake ya soka, lakini hajawahi kucheza kwenye Ligi Kuu ya England. Amefunga mabao 292 katika mechi 570 ngazi ya Klabu hadi sasa, lakini atakabiliwa na ugumu wa kuzoea soka la Ligi Kuu England licha ya mwishoni mwa wiki kutupia mabao mawili katika ushindi wa 5-0 dhidi ya Huddersfield.

Higuain tayari yupo kwenye upande usio sahihi na pia amekuwa majeruhi mara kwa mara msimu huu. Zaidi ni kwamba, Ligi Kuu ya England ni moja ya Ligi Kuu yenye ushindani mkubwa zaidi duniani na hivyo itahitajika kuwa na mchezaji mwenye nguvu na uwezo mkubwa zaidi dimbani. Matarajio ya mashabiki na vyombo vya habari pia yatakuwa makubwa zaidi kwake kwenye EPL kuliko alivyokuwa kule kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, na imani ya Chelsea wameiweka kwake.

Kwa hivyo, Higuain atakabiliwa na presha kubwa zaidi wakati akicheza dimbani. Hali ya hewa ya Hispania na Italia iko tofauti, na Higuain anaweza kuwa na tatizo hilo kwa hali ya hewa ya Uingereza. Litakuwa jambo la kuvutia kumuona akiweza kukabiliana na changamoto ya Ligi Kuu ya England.

**2. Kushuka kiwango chake msimu huu**

Higuain hakuwa na mafanikio makubwa pale AC Milan msimu huu. Alifunga mabao nane katika mechi 22 na hakuwa na kiwango cha kutisha zaidi akiwa eneo la penalti la timu pinzani. Mshambuliaji mwingine wa Milan, Patrick Cutrone ameonekana kuwa na kiwango cha kuvutia zaidi kuliko yeye kwa msimu huu.

Pia alikosa penalti dhidi ya Juventus kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, na kuwafanya kushindwa kupata ushindi kwenye mchezo huo. Alikosa mechi kadhaa kutokana na kuwa majeruhi na bado ana changamoto ya kuwa fiti.

Kwa hiyo, atajikuta kwenye wakati mgumu kufunga mabao kwa kuwapita mabeki wa timu kama Liverpool, Manchester City, Manchester United na Tottenham Hotspur. Chelsea haijaweza kufunga mabao mengi dhidi ya klabu kubwa msimu huu, na haitarajiwi kama Higuain ataweza kuwasaidia.

**3. Staili yake ya uchezaji**

Higuain ni aina ya mshambuliaji wa kuvizia kwenye eneo la penalti, kitu ambacho kinamfanya kuwa na wakati mgumu zaidi kwa staili ya uchezaji wa Chelsea ambao kwa kawaida hucheza kwa mfumo wa 4-3-3 na inamhitaji mshambuliaji wao pekee mbele kuwa na jicho la goli.

Pia wamekuwa wakimtumia Eden Hazard kama mshambuliaji wao namba tisa katika mechi kadhaa, na staili yake ya uchezaji imekuwa na manufaa kwa kikosi hicho.

Zaidi ni kwamba, Chelsea haina wachezaji wengi wazuri wa kupiga pasi na kuwalisha mipira washambuliaji wao na hicho ndicho kitakuwa kigumu zaidi kwa Higuain. Staili ya uchezaji ya Chelsea si ya moja kwa moja, na Higuain anaweza kuwa kwenye wakati mgumu zaidi wa kucheza namba tisa.

Na haya kwa kiasi kikubwa yalikuwa kikwazo kikubwa kwa Morata kushindwa kupata mafanikio kwa 'Blues' hao.

**JE, WAJUA?**

NEWCASTLE imeifunga Manchester City kwenye Premier League kwa mara ya kwanza tangu Septemba 2005, na kuhitimisha ukame wa ushindi katika mechi 22 walizokutana ambapo ilitoka sare tatu na kupoteza 19 (D3, L19).

MICHEZO

## NJE YA UWANJA




### EMERY: SUAREZ HANA MADHARA KWA OZIL

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Arsenal, Unai Emery, hadhani kwamba kutua kwa Denis Suarez kutakuwa na madhara kwa Mesut Ozil.

Licha ya kuwa mmoja wa manahodha wa Arsenal, Ozil ameanza mechi 13 tu za Ligi Kuu msimu huu na haonekani kuwa katika kikosi cha kwanza anachokitaka Emery.

Suarez alijiunga na Arsenal kwa mkopo Alhamisi iliyopita akitokea Barcelona, hivyo kurejea kwa mara ya pili EPL baada ya kuitumikia Manchester City kwa miaka miwili kuanzia 2011.

Emery amemsajili mchezaji huyo, Suarez, ambaye alikichezea kikosi chake cha Sevilla msimu wa 2014-15 wakati akikinoa, hiyo ikiwa na maana kunaweza kuwapo kwa nafasi chache kwa Ozil.

"Hakutabadili kitu kwake," Emery alisema kuhusu Ozil. "[Suarez] amekuja hapa kwa sababu tuna matatizo makubwa katika winga, hatujapata mchezaji sahihi wa kucheza kulia ama kushoto - hiyo ndiyo sababu."




# YANGA ILIVYOINGIA REKODI ZA KICHUYA

**Na Adam Fungamwango**

TAARIFA ya Shiza Kichuya kutakiwa na timu ya Pharco ya Misri ilikuja ghafla tu baada ya timu ya Simba kwenda nchini huko kwa ajili ya mechi ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Al Ahly ya Misri.

Ikiwa nchini Misri zilikuja taarifa kuwa timu hiyo inahitaji huduma ya Kichuya.

Wakati Bongo kukiwa na mjadala ya Kichuya, wengine wakimuombea dili hilo litimie, hatimaye Afisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori akatangaza rasmi kuwa dili hilo limeshakamilika. Tayari sasa rasmi Kichuya ni mchezaji halali wa Pharco kwa mkataba wa miaka miwili.

Hata hivyo, siku moja tu baada ya kuuzwa, klabu hiyo nayo imemtoa kiungo huyo kwa mkopo kwa timu ya Enppi.

Kilichotokea hapa ni kwamba timu ya Daraja la Kwanza iliyomnunua Kichuya, imempeleka kwa mkopo kwenye timu ya Ligi Kuu nchini Misri.

Kichuya ambaye pia anaichezea timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, hajacheza Ligi Kuu Tanzania kwa muda mrefu sana, lakini ameacha mengi ya kukumbukwa, tuyatazame...

**1. Mabao 30 Ligi Kuu**

Mpaka anaondoka kwenye Ligi Kuu Kichuya amefunga mabao 30 akiwa na klabu mbili alizozichezea, ambazo ni Mtibwa Sugar na Simba.

Akiwa Mtibwa, amecheza msimu mmoja tu wa 2015/16 na kupachika mabao nane. Baada ya hapo alijiunga na Simba msimu wa 2016/17 na mpaka anakwenda kucheza soka la kulipwa nchini Misri ameifungia timu hiyo mabao 22 kwenye Ligi Kuu.

Kumbuka rekodi hizi ni kwa mechi za Ligi Kuu tu na si michuano mingine kama Ligi ya Mabingwa, Kombe la Mapinduzi, FA Cup na mingine.

**2. Bao la kwanza kufunga Ligi Kuu**

Kichuya aliweka rekodi ya kufunga bao la kwanza kwenye Ligi Kuu Septemba 16, mwaka 2015 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba mjini Mwanza.

Siku hiyo timu yake ya Mtibwa Sugar ilikuwa ikicheza dhidi ya Toto African ya Mwanza.

Mtibwa ilishinda mabao 2-1, Kichuya akifunga bao la kwanza dakika ya 21, lingine likifungwa na mkongwe ambaye kwa sasa amestaafu, Vicent Barnabas, huku Miraji Athumani akiifungia Toto bao la kufutia machozi. Ulikuwa ndiyo msimu wake wa kwanza kucheza Mtibwa na mechi hiyo ilikuwa ni ya pili kwenye Ligi Kuu.

**3. Bao la kwanza kuifungia Simba**

Ni msimu mmoja tu Kichuya aliocheza akiwa na Mtibwa kabla ya kujiunga na Simba, na akaifungia timu yake mpya bao la kwanza kwenye mechi ya kwanza kabisa ya ufunguzi wa Ligi Kuu msimu wa 2016/17 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam. Naye pia ilikuwa ni mechi ya kwanza kucheza dhidi ya Simba kwenye Ligi Kuu.

Alifunga bao la tatu dakika ya 79, Agosti 20, 2016, Simba ilipoichapa Ndanda mabao 3-1, mengine yakifungwa na Laudit Mavugo na Fredrick Blagnon, la kufutia machozi la Ndanda likifungwa na Omari Mponda.

**4. Mwiba mchungu kwa Yanga**

Tangu alipojiunga na Simba msimu wa 2015/16, Kichuya amekuwa mwiba mchungu kwa timu hasimu ya Yanga.

Kwa misimu minne aliyoichezea Simba, ameiwezesha timu yake kuwa mbabe mbele ya Yanga, akifunga mabao matatu na kutoa pasi moja ya bao.

Tangu Kichuya ajiunge na Simba, timu hiyo haijapoteza mechi dhidi ya Yanga kwenye Ligi Kuu hadi anaondoka.

Oktoba Mosi 2016, chupuchupu Simba ifungwe kwa bao la Amissi Tambwe dakika ya 26, lakini Kichuya akaisawazishia kwa kona iliyokwenda moja kwa moja hadi wavuni dakika ya 87.

Mechi ya mzunguko wa pili, Simba ilichapa Yanga mabao 2-1, Februari 25, Yanga ikitangulia dakika ya tano kwa bao la penalti ya Simon Msuva, lakini Laudit Mavugo akisawazisha dakika ya 66, kabla ya Kichuya kumalizia bao la pili dakika ya 81.

Msimu wa 2017/18, Simba ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Yanga Oktoba 28, 2017, Kichuya akifunga bao, lililosawazishwa na Obrey Chirwa, lakini Aprili 29, mwaka 2018, Simba ikishinda bao 1-0 lililofungwa kwa kichwa na Erasto Nyoni, baada ya faulo iliyopigwa na Kichuya.

**5. Utaalamu wa kupiga penalti**

Moja kati ya mambo ya kukumbukwa kwa kiungo mshambuliaji huyo ni umahiri wake wa kupiga mikwaju ya penalti.

Hadi anaondoka kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, amefunga penalti sita na kukosa moja tu.

Penalti hizo sita hazihusiani na za michuano mingine zaidi ya Ligi Kuu. Penalti tano amezifunga akiwa Simba na moja akiwa Mtibwa na hata aliyoikosa ilikuwa kwenye klabu ya Mtibwa.

Penalti hiyo aliikosa msimu wa 2015/16 kwenye mechi dhidi ya Toto Afrcans.

Alizofunga zilikuwa ni kati ya Mtibwa dhidi ya Majimaji, akiwa Simba alifunga dhidi ya timu za Majimaji, Kagera Sugar, Stand United, Mbeya City na Mwadui. Penalti zote za Simba zilikuwa ni msimu wa 2016/17.

**6. Bao la mwisho Ligi Kuu Bongo**

Bao lake la mwisho kabla ya kuiaga Ligi Kuu ya Tanzania, alilifunga Desemba 29, mwaka jana kwenye Uwanja wa Taifa wakati timu yake ya Simba ikiifumua Singida United mabao 3-0. Alifunga mabao mawili kwenye mechi hiyo, dakika ya 48 na bao la mwisho alilifunga dakika ya 54. Amefunga mabao matatu mpaka anaondoka nchini.

## Extra Time

# Nyota wa5 kizazi cha sasa hawajabeba ndoo UEFA

**LONDON,** England

KATIKA soka la kisasa limeshuhudia baadhi ya wachezaji wakikosa mafanikio makubwa licha ya kuwa nyota wanaotajwa zaidi duniani. Ubora wa mchezaji mmoja mmoja unakuwa na tofauti na ubora wa timu anayocheza.

Kwa miaka mingi, kumekuwa na wachezaji wakongwe ambao walishinda tuzo nyingi mno binafsi pamoja na mataji ya Ligi wakiwa na klabu zao. Hata hivyo, wamejikuta wakishindwa kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kipindi chao chote cha uchezaji.

Katika makala haya tunawaangalia washambuliaji bora wa kizazi cha sasa ambao wameshindwa kulibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Chakuelewa ni kwamba, wachezaji hawa watano wamewekwa kwenye orodha hii kutokana na viwango vyao kwa kipindi cha miaka michache iliyopita na wapo kwenye kiwango cha juu na klabu zao. Sergio Aguero, Raheem Sterling, Pierre-Emerick Aubameyang na Marco Reus wametajwa kwa heshima tu katika orodha hii...

**5. Antoine Griezmann**

Antoine Griezmann anastahili kushinda mataji mengi zaidi kuliko yale aliyonayo hadi sasa. Mfaransa huyu amekuwa na mchango mkubwa zaidi kwenye mafanikio ya Atletico Madrid tangu mwaka 2014. Alikuwa na Real Sociedad kutoka mwaka 2009 hadi msimu wa 2013-14. Hadi sasa, Griezmann amefunga mabao 128 kwenye mechi 239 alizowachezea miamba hao wanaotumia jezi ya rangi nyekundu na nyeupe.

Ana taji la Ligi ya Europa alilolishinda msimu wa 2017-18, ana taji la UEFA Super la mwaka 2018, pamoja na Supercopa ambalo alishinda mwaka 2014, haya ni mataji makubwa aliyoshinda mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 akiwa na Atletico Madrid. Mshambuliaji huyu amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi kwa kipindi chote tangu ametua hapo. Alishika nafasi ya tatu kwenye tuzo ya Ballon d'Or mwaka 2018.

Kiufundi ni mchezaji aliyebarikiwa na pia alishinda tuzo ya Kiatu cha Fedha kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018 na pia alifanikiwa kulibeba Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa. Mshamabuliaji huyu kwa sasa ana mabao 10 kwenye mechi 21 alizocheza katika ligi msimu huu.

Kwa sasa, Atletico Madrid wanashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, (kabla ya mechi za wikiendi) wakiwa na pointi 44 kwenye mechi 21 wakizidiwa tano na vinara Barcelona.

Ndio timu pekee iliyotinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu bila kushinda. Atletico Madrid watacheza na Juventus Februari 21, mwaka huu kwenye hatua ya mtoano wa timu 16-bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ni muda tu ndio utakaoongea kama wataweza kulibeba taji hilo msimu huu.

**4. Edinson Cavani**

Edinson Cavani ndiye mfungaji bora wa wakati wote wa PSG. Mkongwe huyo wa Uruguay ana mabao 190 katika mechi 268 alizoichezea PSG. Alishinda tuzo ya Kiatu cha Dhahabu mwaka 2018 na amekuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, kwa misimu miwili iliyopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ameshinda mataji manne ya Ligue 1, manne ya Coupe de France, na mataji mengine nane akiwa na PSG. Cavani huwa anacheza kama mshambuliaji wa kati na tayari amefunga mabao 16 katika mechi 14 alizowachezaji miamba hao wa Ufaransa msimu huu.

PSG watacheza na Manchester United kwenye hatua ya mtoano wa timu 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Cavani anajulikana kama mshambuliaji 'mkali' akiwa dimbani. Mzaliwa huyo wa Salto anatarajiwa kuwa na mchango mkubwa zaidi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu na yupo tayari kuisaidia PSG kulitwaa taji hilo kwa mara yake ya kwanza.

**3. Harry Kane**

Harry Kane kwa sasa anauguza majeraha ya mguu aliyoyapata kwenye mchezo dhidi ya United na anatarajiwa kuwa nje ya dimba hadi Machi mwaka huu. Mshambuliaji huyo wa kati wa Spurs tayari ameshafunga mabao 14 katika mechi 22 alizocheza kwenye Ligi Kuu msimu huu, na kumfanya kuwa kinara na mchezaji mwenzake wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 25, alitwaa Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora wa Ligi Kuu ya England msimu wa 2015-16 na 2016-17. Pia alishinda Kiatu cha Dhahabu kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018. Hata hivyo, licha ya Kane kushinda tuzo nyingi binafsi, lakini hajaweza kuisaidia timu yake kutwaa taji lolote.

Tottenham itacheza na Borussia Dortmund kwenye hatua ya mtoano wa timu 16 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Atakuwa na hamu kubwa ya kuhakikisha analitwaa taji hilo kwa mara ya kwanza kwake na kwa timu yake.

**2. Robert Lewandowski**

Robert Lewandowski amekuwa mchezaji muhimu zaidi kwa Bayern Munich tangu mwaka 2014. Ndiyo mashine ya kufunga mabao na amefunga mabao 175 katika mechi 221 alizoichezea Munich hadi sasa. Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 30 raia wa Poland kwa sasa amefunga mabao 12 katika mechi 18 kwa miamba hao wa Ujerumani msimu huu kwenye Ligi Kuu ya Bundesliga.

Kitu kinachomfanya kuwa mchezaji muhimu zaidi na mfungaji wa mabao ni uwezo wake wa kufunga kwa kutumia miguu yote miwili pamoja na kichwa. Mara kwa mara anasifiwa kutokana na kucheza kwa maadili na nidhamu. Pia yeye ni mfungaji namba sita kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wa wakati wote akiwa na jumla ya mabao 53 katika mechi 78.

Ameshinda mataji sita ya Ligi Kuu ya Ujerumani (manne akiwa na Bayern na mawili akiwa na Dortmund). Ameshinda mataji mengine tisa kwenye maisha yake ya soka. Mzaliwa huyu wa Jiji la Warsaw atakuwa na matumaini ya kupata taji la Ligi ya Mabingwa msimu huu.

Lewandowski alicheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2013, lakini timu yake ya Borussia Dortmund ilifungwa na Bayern Munich.

Bayern itacheza na Liverpool kwenye hatua ya mtoano wa timu 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

**1. Mohamed Salah**

Mohamed Salah alitengeneza rekodi ya kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja kwenye Ligi Kuu ya England akicheza mechi 38 na kufunga mabao 32. Alitwaa tuzo ya Kiatu cha Dhahabu kama mfungaji bora kwenye Ligi Kuu msimu wa 2017-18, mchezaji bora wa Afrika mwaka 2017 na 2018, mchezaji bora wa msimu wa Ligi Kuu England (2017-18).

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Misri pia alipata tuzo ya FIFA Puskas mwaka 2018 na alishika nafasi ya pili kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2017-18.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, amekuwa na msimu mzuri zaidi kwa miaka miwili iliyopita. Kwa sasa yupo kileleni kwenye orodha ya wafungaji wanaoongoza kwenye Ligi Kuu ya England akiwa na mabao 16 baada ya kucheza mechi 23.

Ana kasi, uwezo wa kumiliki mpira na kupiga chenga, Salah anaonekana kuwa juu zaidi na kama mshambuliaji aliyekamilika zaidi katika kizazi cha sasa. Nyota huyo bado hajashinda taji lolote na Liverpool.

Wekundu hao wa Anfield kwa sasa wanashika nafasi ya kwanza kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England baada ya kushinda mechi 19, sare tatu na kufungwa moja kutoka kwenye mechi 23. Pamoja na Liverpool kuwa na ukame wa mataji, pia Salah anakabiliwa na hilo. Wekundu hao wameshinda mara tano taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na la hivi karibuni zaidi walishinda msimu wa 2004-05.

Taji la mwisho kwa Salah kushinda lilikuwa ni Kombe la Ligi Kuu ya Uswisi msimu wa 2013-14. Alishinda akiwa na Basel.

Liverpool watacheza na Bayern Munich kwenye hatua ya mtoano wa timu 16-Bora Ligi ya Mabingwa Ulaya Februari 20, mwaka huu.


Mohamed Salah



Lewandowski

## NUKUU


"[Alvaro] Morata ni mchezaji muhimu kwetu, tutakuwa na mastraika wanne wakumaliza msimu huu, sambamba na wengine watatu na Griezmann, Costa na [Nikola] Kalinic. Anatupa uwezekano tofauti tangu hapo ni mshambuliaji wa kumaliza. Sifa za Costa ni kasi yake, nguvu, na uwezo wa kutumia nafasi. Na kwa kuwa na Morata tunaye mshambuliaji mmaliziaji tena," **Diego Simeone akizungumzia ujio wa Morata Atletico Madrid**



"Tumejaribu kufanya kazi na kila mmoja, [Gonzalo] Higuain ni mchezaji mpya, lakini anajua nini ambacho nini kocha anachotaka. Ni straika wa kiwango cha juu na anaweza kufunga mabao mengi. England ni tofauti na Italia na Hispania, lakini ana ubora huo. Nadhani Maurizio [Sarri] atakuwa na furaha kwa sababu alikuwa akisubiri majibu kutoka kwetu na tumempatia," **Eden Hazard baada ya Chelsea kushinda 5-0 dhidi ya Huddersfield juzi.**



"Kazi hii ni kama matairi yanavyozunguka, natakiwa kuwafanya wachezaji wacheze vizuri zaidi na kuwa kwenye ubora wao, kama naweza kuifanya timu icheze vizuri, maana yake ni kwamba wachezaji wataonyesha vipaji vyao na mwisho wa siku tutakuwa tukipata matokeo mazuri zaidi, " **Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer akizungumza kabla ya mchezo wake wa jana Jumapili dhidi ya Leicester City.**



## Michezo




Beki wa Al Ahly akimdhibiti straika wa Simba, Emmanuel Okwi (kulia), kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa iliyochezwa Jumamosi usiku nchini Misri, Simba ikikubali kipigo cha mabao 5-0.

# SIMBA ILIVYOJISULUBU MISRI

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara nyingine tena, mabingwa wa Soka Tanzania Bara, Simba wameendeleza rekodi yake mbaya kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu baada ya kuchapwa mabao 5-0 na Al Ahly wakiwa ugenini nchini Misri.

Hii ni mara ya pili mfululizo kwa Simba kufungwa idadi hiyo ya mabao kwani ilibugizwa 5-0 dhidi ya AS Vita ikiwa nchini Congo DR.

Ina maana kuwa Simba imepoteza mechi mbili za ugenini tena kwa idadi kubwa ya mabao, huku ikiwa imebakisha mechi moja ugenini dhidi ya JS Saoura ya Algeria, huku ikibakiza mechi mbili nyumbani, dhidi ya Al Ahly na AS Vita.

Kwenye mechi ya Jumamosi, makosa yaliyosababisha kufungwa idadi hiyo ya mabao hayakutofautiana sana na mechi dhidi ya AS Vita, hapa tunakuchambulia kwa uchache, twende sasa...

**1. Kukaba kwa macho**

Ukiangalia idadi kubwa ya mabao yaliyofungwa, yalitokana na mabeki wa Simba kushindwa kukaba njia za mipira na hata kukaba mtu kwa mtu na badala yake wamekuwa wakijirundika sehemu moja.

Rejea bao la kwanza ulipopigwa mpira mfupi wa adhabu, mabeki wa Simba walirundikana sehemu moja na wote wakawa wanaangalia mpira badala ya kukaba watu na mfungaji akapiga kichwa akiwa peke yake.

Mabao mengine yalionekana kufanana na hayo, kwani tatizo kubwa lilikuwa ni ukabaji, huku pia wachezaji wengi wa Simba wakishindwa vita ya kupambania mpira baina yao na wapinzani wao.

**2. Manula amechoka**

Kipa wa Simba, Aishi Manula naye pia inabidi ajitathmini. Kati ya mabao matano aliyofungwa, mawili likiwamo la kwanza kama angekuwa kwenye kiwango kizuri angeweza kuokoa.

Ni kweli kwa sasa Simba ina matatizo makubwa kwenye beki na hasa baada ya kuumia kwa Shomari Kapombe na Erasto Nyoni, lakini si kila mabeki wakipitwa basi liwe bao.

Kipa naye ana kazi yake kuhakikisha timu haifungwi, hata kama mabeki wakifanya makosa mtu wa mwisho kuamua ni yeye.

Kwa sasa mabeki wa Simba wakifanya makosa, linakuwa bao kwa asilimia kubwa kutokana na Manula kwa sasa kuonekana kuchoka baada ya kucheza mechi nyingi zikiwamo za Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa na zile za timu ya Taifa, Taifa Stars, au kiwango chake kwa sasa kimeshuka.

**3. Mkude naye 'kachomesha'**

Kiungo mkabaji Jonas Mkude kwa siku za karibuni hayuko kwenye kiwango chake cha kawaida.

Kuanzia kwenye mechi dhidi ya Bandari ya Kenya, lakini pia Jumamosi dhidi ya Al Ahly.

Alishindwa kabisa kuwasaidia mabeki kukaba kiasi kwamba akawapa kazi kubwa wenzake na kuruhusu idadi kubwa hiyo ya mabao.

Ndiyo maana Kocha Mkuu Mbelgiji Patrick Aussems, wakati wa mapumziko alimtoa na kumuingiza Mzamiru Yassin ambaye kwa kiasi kikubwa alikuja kusaidia kukaba na Al Ahly hawakupata bao lolote kipindi cha pili.

**4. Stamina kwa wachezaji ndogo**

Kwa kiasi kikubwa mazoezi ya Simba kwa siku za hivi karibuni yanachagizwa zaidi na ya viungo yakiongozwa na Mtunisia Adel Zrane.

Wachezaji wa Simba wanaonekana kila mtu akiwa na 'kirago' chake, wakifanya mazoezi ya viungo. Lakini linapokuja suala la kuyafanyia kazi mazoezi hayo ndipo wachezaji wa Simba wanapofeli.

Hata kwenye Ligi Kuu ya Tanzania Bara, wachezaji wa Simba wanaonekana hawana stamina, huko kwenye Ligi ya Mabingwa ndiyo kabisa.

Haijulikani ni kwa nini, lakini kocha huyo wa viungo inabidi naye aangalie mazoezi yake, kwani ukiangalia mechi zote mbili kati ya AS Vita na Al Ahly, moja ya vitu ambavyo Simba ilikuwa ikizidiwa ni stamina.

**5. Maneno ya Kocha wa Nkana ndiyo haya**

"Natamani kama ungekuwapo Zambia kuona namna Simba walivyocheza. Wanahitaji kujiimarisha kwenye safu ya ulinzi, wanatakiwa kuwa makini, waamke, wameingia kwenye hatua ya makundi, watakutana na timu za Waarabu, wanaweza kufungwa mabao mengi wasipojiimarisha," yalikuwa ni maneno ya Kocha Mkuu wa Nkana FC, Beston Chambeshi mara baada ya timu yake kutolewa na Simba kwa jumla ya mabao 4-3.

Na kweli kilichowapata Simba ni kile kile kilichotabiriwa na kocha huyo.

Inawezekana si viongozi wa Simba wala kocha wao waliokuwa wanajua ugumu wa michuano hiyo hatua ya makundi na kudhani kuwa kikosi chao, baada ya kuitoa Mbabane na Nkana, basi kingekuwa na uwezo wa kupambana kwenye hatua hiyo.

Ndiyo maana hakukuwa na juhudi zozote za makusudi za kuongeza wachezaji ili kuongeza nguvu na hasa eneo la ulinzi ambalo ndilo lilionekana tangu mwanzo lina matatizo.

**NAJUA WAJUA**

VICTOR Lindelof ni mchezaji wa nne raia wa Sweden kuifungia bao Manchester United kwenye EPL, ikiwa ni baada ya Jesper Blomqvist, Henrik Larsson na Zlatan Ibrahimovic.



## MAKALA



# SOLSKJAER YATAMKUTA YA ZIDANE AU DI MATEO?

**MANCHESTER,** England

HISTORIA inanionyesha ukurasa mzuri na wenye kuvutia kwenye vitabu vya hawa watu wawili ambao hawakupewa nafasi kubwa, ni Zinedine Zidane na Roberto di Mateo.

Watu hawa wametoka kwenye ardhi ambazo zina mchanga wenye damu nzuri ya mpira wa miguu. Ardhi ambazo zinaheshimika zaidi kwenye mpira wa miguu duniani.

Ardhi ambazo zimetoa nyota wengi wa mpira wa miguu. Leo hii ukimtaja beki, Paolo Maldini moja kwa moja akili yako itakupeleka nchini Italia, mabingwa mara nne wa Kombe la Dunia.

Ndivyo ilivyo kama ukitaja Michael Platin. Akili yako itakuoneyesha sura ya nchi ya Ufaransa, mabingwa wa Kombe la Dunia mara mbili.

Nchi ambayo iliwahi kujaliwa vipaji maridhawa na mpaka sasa inazidi kuzaa vipaji maridhawa kwenye dunia ya mpira wa miguu.

Unamkumbuka Thierry Henry? Mshambuliaji bora na hatari kuwahi kutokea katika uso huu wa dunia? Huyu katokea kule Ufaransa.

Wakati Ufaransa wakiwa na Claudio Makelele, Italia waliwahi kubahatika kuwa na Gattuso, viungo hawa wawili wakabaji walikuwa bora zaidi kwenye eneo la ulinzi.

Viungo ambao walikuwa wanaogopeka, wao nguvu ndizo zilikuwa sababu kuu ya wao kuendelea kuishi kwenye dunia ya mpira.

Wakati Italia ikiwa inajivunia kuwa na Gattuso ambaye alikuwa anatumia nguvu nyingi, dunia iliwapa zawadi watu wa Italia kwa kuwa na Andrea Pirlo.

Mwanadamu pekee ambaye aliwekewa 'komputa ya mpira kichwani mwake'. Kichwa chake kilikuwa na maarifa mengi ya mpira.

Kichwa chake kiliweza kukokotoa hesabu kali za mpira wa miguu ambazo zilionekana na watu wengi kuwa ni ngumu.

Kwa kifupi huu ndiyo upekee wa soka la Ufaransa na Italia. Yani soka ambalo limejaa vipaji haswaa, vipaji ambavyo vilikuja kuweka alama kubwa duniani.

Vipaji vya soka la Italia na Ufaransa halijawahi kuishia kwa kutoa wachezaji mahiri pekee tu kwenye mpira wa miguu.

Hata makocha wengi bora wametoka kwenye nchi hizi. Unamkumbuka Arrigo Sanchi? Mwanamapinduzi mkubwa wa soka la Italia?

Kwa sasa unaweza kuwatazama kina Carlo Ancelotti, Maurizio Sarri, Antonio Conte kama makocha ambao wanafanya vizuri pia.

Hii inatosha kuonyesha kuwa soka la Italia huwa linatoa makocha bora kabisa, lakini kuna makocha ambao waliwahi kupewa timu kwa mashaka na wakoondoka kwa fedheha.

Chelsea imekuwa timu ambayo ina damu nzuri ya makocha kutoka Italia ambao hufanya vizuri zaidi. Makocha wengi waliofanya vizuri Chelsea wametoka Italia.

Di Matteo anaweza kukumbukwa Chelsea kwa kuipa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kocha huyu alikuwa hapewi nafasi kubwa.

Aliichukua timu kama kocha wa muda, lakini alifanikiwa kuifikisha katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kubeba kombe hili.

Lakini katika hali ya kushangaza, akatupiwa virago mwishoni mwa msimu licha ya kuipa mafanikio makubwa timu hiyo.

Hadithi kama hii iliwahi kutokea kwa Real Madrid, baada ya Zinedine Zidane kukabidhiwa timu kama kocha wa muda baadaye akawa kocha mkuu kama ambavyo ilikuwa kwa Di Matteo.

Zinedine Zidane aliipa mafanikio makubwa Real Madrid, alichukua makombe tisa ndani ya miaka miwili na nusu, ikiwamo kuchukua Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu.

Lakini tofauti ya hawa makocha wawili ni moja tu. Wanafanana jinsi walivyoingia, walitumia mlango wa aina moja kuingia.

Hata hivyo, walivyotoka, Di Matteo alitolewa kwa fedheha ya kufukuzwa na Zinedine Zidane alijiuzulu kwa heshima.

Hapa ndipo ninapoanza kuwaza, Ole Gunnar anaweza akachukua sura ya nani kati ya hawa watu wawili ambao anafanana nao namna ambavyo ameingia kwenye timu.

Tangu ameingia amekuwa na mafanikio makubwa ya kutoshindwa mchezo wowote hadi sasa, lakini mwisho wa msimu ataweza kudumu na timu hiyo?

Hili ndilo jambo ambalo unaweza ukajiuliza, je, atatoka kama Di Mateo kwa kufukuzwa au atatoka kwa heshima kama Zidane. Uzuri ni kwamba Ole Gunnar amepewa nafasi hiyo kwa muda hadi mwishoni mwa msimu huu.

Yote kwa yote ni kwamba, kama atafikiriwa kupewa nafasi hiyo baada ya kuwa na mafanikio ya angalau kuipa taji moja Man United msimu huu ni suala la kusubiri na kuona.

**NDANI YA 18**

WASHAMBULIAJI wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang na Alexandre Lacazette kila mmoja amefunga mabao matano dhidi ya timu zilizopanda Ligi Kuu England msimu huu, idadi ambayo ni kubwa zaidi kuliko mchezaji mwingine yeyote katika ligi hiyo kwa sasa.




NDANI YA 18



KATIKA soka la kisasa limeshuhudia baadhi ya wachezaji wakikosa mafanikio makubwa licha ya kuwa nyota wanaotajwa zaidi duniani. Ubora wa mchezaji mmoja mmoja unakuwa na tofauti na ubora wa timu anayocheza.

Uk. 16-17



XXX

# WANASOKA WA4 BABA ZAO MAWAKALA ZAO

**LONDON,** England

MAWAKALA ni watu muhimu mno katika maisha ya wacheza soka. Kuanzia kwenye kufanya makubaliano katika mikataba yao, kuwasimamia kwenye maisha yako nje ya uwanja, mawakala wana mchango mkubwa mno kwenye maisha ya wanasoka wengi duniani.

Hivyo, ni muhimu kuwa na wakala mzuri kwa mwanasoka ili kuweza kuwa na ubora wako dimbani na nje ya dimba na maisha binafsi.

Mawakala wamekuwa nguzo muhimu zaidi kwenye soka la kisasa, kwani usajili unatokea kwa ajili yao.

Kiukweli fedha nyingi zinalipwa kwao kwa ajili ya kuwafanya wateja wao waende kwenye klabu husika. Tumeona mawakala wenye majina makubwa duniani kama Mino Raiola na Jorge Mendes ambao wamekuwa na mahusiano na klabu kadhaa na kwenye usajili wachezaji wao wamekuwa wanakwenda kwenye klabu hizo tu.

Kuhusisha mmoja wa wanafamilia kwenye michezo ya kulipwa huwa kuna wakati inaleta athari. Hata hivyo, kumekuwa na matukio kadhaa ya mmoja wa wanafamilia kuwa wakala wa mwanamichezo fulani na kwa miaka ya sasa inatokea zaidi. Kwa sasa haiepukiki tena, kwani kuna wachezaji wengi ambao wameamua kuwafanya baba zao wazazi kuwa mawakala wao.

Katika makala haya tunakuchambulia wachezaji soka wanne ambao baba zao wazazi ndio mawakala wao, na ndio wenye maamuzi ya mwisho kwenye maisha yao ya soka...

**1. Neymar - Neymar Santos Sr.**

Mmoja wa wachezaji ambaye ameamua kumfanya baba yake mzazi kuwa wakala wake ni Neymar. Baba yake Neymar Sr. ndiye alikuwa stelingi wa kuhakikisha Neymar anatoka Brazil na kutua pale Barcelona, na pia ndiye aliyesisimamia mwanawe aweke rekodi ya dunia ya usajili wakati anatoka Barcelona na kujiunga na PSG mwaka 2017.

Neymar Sr. ndiye amekuwa chachu ya mafanikio ya Neymar kwenye soka. Neymar Santos pia amekuwa akimsaidia mwanawe kumaliza kesi zake za mahakama pia.

Kiukweli Neymar Sr. pia alikuwa mchezaji wa kulipwa, lakini hakupata mafanikio makubwa. Neymar Santos Sr. alikuwa anamalizia kipindi chake cha uchezaji kwenye klabu ya Mogi Das Cruzes inayomilikiwa na kiwanda kimoja cha jijini Sao Paulo wakati Neymar anazaliwa.

Awali Wagner Ribeiro alitumika kama wakala wa Neymar kabla ya baba yake kuchukua majukumu hayo, kwa sasa amekuwa maarufu baada ya kuweza kuhakikisha maisha binafsi ya Neymar nje ya uwanja hayapewi kipaumbele.

**2. Lionel Messi - Jorge Messi**

Lionel Messi ni mmoja wa wachezaji maarufu zaidi duniani kwa sasa. Mchezaji huyu wa kimataifa wa Argentina ameshinda karibia kila kitu kwenye ngazi ya klabu na bado kwa hivi sasa yupo kwenye msimu mzuri kwa kipaji chake.

Lionel Messi amekuwa na miamba wa soka la Hispania, Barcelona tangu alipotoka Argentina. Ingawa alihusishwa na klabu kadhaa kwenye maisha yake ya soka, lakini Messi hajawahi kuondoka kwenye klabu yake hiyo ya utotoni. Na sababu kubwa ni wakala ambaye ni baba yake mzazi, Jorge Messi.

Jorge amekuwa wakala wa Lionel Messi, na amekuwa akihusika kwenye kusaini mkataba mpya kwa wanawe. Messi alikuwa na matatizo kadhaa kwenye masuala ya ulipaji wa kodi na Jorge alisimama naye imara.

Ingawa haionesi kama Messi anaweza kuondoka Barca, lakini uhamisho wowote utamhusisha Jorge.

**3. Juan Mata - Juan Manuel Mata Sr.**

Juan Mata amekuwa mmoja wa wachezaji wachache ambao hawapewi thamani yao kwenye soka. Mhispania huyu ana akili zaidi anapocheza kwenye safu ya kiungo mshambuliaji na amekuwa akitengeneza nafasi nyingi kwa washambuliaji kufunga, na pia amekua mfungaji mzuri.

Mambo yote ya Juan Mata nje na ndani ya dimba yanasimamiwa na baba yake mzazi, Mata Sr.

Alihusika kwenye uhamisho mkubwa kutoka Valencia kwenda Chelsea mwanzoni mwa kipindi chake cha uchezaji na baadaye kutua pale Manchester United. Wengi hawajui, lakini Mata alishawahi kuichezea Real Madrid kabla ya kukaa pale Valencia.

Juan Manuel Mata Rodríguez pia alikuwa mwanasoka akicheza nafasi ya ushambuliaji ambaye alicheza kati ya mwaka 1980 na 1990 na alikuwa akiichezea timu ya mtaani kwao ya Burgos CF. Alianza kuwa wakala wa mchezaji wake tangu akianza kucheza soka la kulipwa.

Mata anatarajia kusaini mkataba mpya na Manchester United, na Mata Sr. atakuwa ndiye mwenye kauli ya mwisho.

**4. Eden Hazard - Thierry Hazard**

Thierry Hazard amekuwa akipamba vyombo vya habari katika siku za hivi karibuni akizungumzia majaliwa ya mwanawe wapi atakakokwenda. Hazard kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua kule Real Madrid, na baba yake mzazi ndiye amekuwa katikati ya uvumi huo.

Eden Hazard hakuwa na wakala kabla ya baba yake kuamua kuichukua nafasi hiyo. Carine na Thierry Hazard, ni wazazi wa Eden Hazard, na wana historia ya soka huko nyuma.

Wakati Thierry alikuwa mchezaji wa soka katika klabu ndogo ya La Louviere, iliyopo kwenye mji ambao Thorgan na Eden walizaliwa na mama yao alikuwa mshambuliaji wa timu ya wanawake akicheza kwa miaka sita. Baadaye wanandoa hao waliamua kuwa walimu wa viungo.

Chelsea inapigania kumbakiza Hazard, hivyo Thierry Hazard atakuwa na kazi kubwa kwenye mkataba mpya au kumuondosha mwanawe siku sijazo.

**USILOLIJUA**

CHELSEA imepata ushindi wa mabao matano kwa mara ya kwanza tangu Desemba 2017, wakati ilipoichapa Stoke 5-0 kwenye Uwanja wa Stamford Bridge. Juzi Chelsea ilipata ushindi kama huo dhidi ya mabao ikiwa nyumbani.



## HABARI MBEYA

### Madiwani washauriwa utekelezaji wa miradi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, limeshauriwa kuanza kutekeleza miradi ya kimkakati ili kuongeza ukusanyaji wa mapato badala ya kuendelea na miradi ya kawaida.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya, Hassan Mkwawa, baada ya kubaini kuwa halmashauri hiyo imefikia malengo ya ukusanyaji wa mapato katika robo mbili za mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Aliitaka halmashauri hiyo kuanzisha miradi mikubwa kama zilivyofanya halmashauri zingine nchini ikiwamo Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ambayo imejenga kituo kikubwa cha mabasi cha Msamvu.

Alisema halmashauri hiyo ilikadiria kukusanya Shilingi bilioni mbili katika mwaka huu wa fedha, lakini mpaka sasa imekusanya zaidi ya Shilingi bilioni 1.3 na kwamba kuna uwezekano katika robo mbili zilizobakia wakamalizia kiasi kilichobakia.

"Halmashauri hii inaenda vizuri sana kwenye ukusanyaji wa mapato, hivyo wanaweza wakahama kutoka kwenye miradi ya kawaida na kuanza kutekeleza miradi ya kimkakati, ili kuongeza ukusanyaji zaidi wa mapato," alisema Mkwawa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Mwalingo Kisemba, alisema baraza lake linapokea ushauri huo kwa madai kuwa utaleta tija kwenye ukusanyaji wa mapato na hatimaye kuwa na uhakika wa kuwahudumia wananchi.

Hata hivyo alisema miradi ya kimkakati iko kwenye mipango ya halmashauri hiyo na kwamba kilichobaki ni utekelezaji ambao unaweza ukaanza wakati wowote kama bajeti itaruhusu.

Alisema wataalamu wa halmashauri hiyo wanaendelea na uandaaji wa maandiko mbalimbali kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi hiyo na kwamba baadhi ya miradi hiyo tayari imeshaainishwa. "Sisi tupo kwenye barabara kuu na tunapakana na Jiji kila mahali, sasa kwenye hii barabara kuu tumeona fursa ya kuwa na stendi ya mabasi na maegesho ya malori ambayo wataalamu wanaendelea kuandaa andiko la kupeleka hazina ili tupewe fedha," alisema Mwalingo.

Naye Diwani wa Viti Maalumu, Aida Haule, alisema miradi hiyo itaiongezea halmashauri mapato kutokana na baadhi ya vyanzo kuondolewa.

Alisema baadhi ya vyanzo vimechukuliwa na taasisi zingine ikiwamo miradi ya barabara ambayo imepelekwa kwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) pamoja na ushuru ambao umepungua kutokana na wajasiriamali kuanza kupewa vitambulisho.

# Mahakama yatoa neno kwa wadau kikokotoo cha mafao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, imewashauri watumishi wa umma, wastaafu na wadau mbalimbali kuyatumia maadhimisho ya Wiki ya Sheria kushughulikia suala la kikokotoo cha mafao ya wastaafu na kulipatia ufumbuzi suala hilo mapema.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, Robert Mharamba, wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki ya Sheria, ambapo alisema suala hilo linatakiwa kupatiwa ufumbuzi mapema ili kuepusha maswali baadaye.

Alisema watu wote ambao wanaona kuwa kikokotoo hicho kinaweza kuwaathiri baada ya mwaka 2023 ambao ni muda uliowekwa kwa huruma ya Rais kwa ajili ya maandalizi kuisha na kwamba wanatakiwa wapatiwe ufafanuzi namna itakavyokuwa.

Jaji Mharamba alisema kwa mujibu wa sheria za nchi, hakuna mtu ambaye yupo juu ya sheria, hivyo jamii ikibaini kuna jambo la kisheria linalokinzana na matakwa ya jamii uko utaratibu wa kulishughulikia na chombo pekee chenye mamlaka ya kutoa haki ni mahakama.

"Hata sisi mahakama tunaweza tukashtakiwa na tutaenda kumuomba mwanasheria wa sherikali akatutetee, hivyo tunawashauri watu waje wapate ufafanuzi maana hata sisi mahakama na waajiriwa wote ni wadau wake," alisema.

Aidha, alisema Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, inakabiriwa na uhaba mkubwa wa majaji hali inayosababisha kuelemewa na wingi wa mashauri yaliyopo.

Alisema mahakama hiyo ina majaji wawili pekee, huku ikiwa na mashauri 1,600 ambayo yanatakiwa kushughulikiwa, hivyo akaeleza kuwa wanaomba miongoni mwa majaji walioteuliwa hivi karibuni baadhi wapelekwe mkoani humo kupunguza pengo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye alikuwa mgeni rasmi, aliitaka Mahakama ya Tanzania kuendelea kuwa chombo kikuu cha kutafsiri sheria.

Vilevile, aliitaka mahakama hiyo kuendelea kutoa haki kwa maslahi mapana ya umma wa Watanzania huku watumishi wake wakizingatia maadili ya kazi yao.

Alisema kuna baadhi ya matukio ambayo huwa yanatokea na ukweli unaeleweka, lakini mahakama zinapotoa uamuzi inaonyesha kuwa matukio hayo hayakutokea hivyo akaitaka mahakama kuendelea kutoa tafsiri sahihi ya haki.

"Kule Kyela ilitokea tukio la mtoto wa miaka nane kubakwa, Jeshi la Polisi likasema amebakwa, madaktari wakathibitisha kuwa alibakwa lakini mahakama ikasema hakubakwa, Chunya hivyo hivyo, sasa nashindwa kuelewa ushusiano uliopo," alisema Chalamila.

Kwa upande wake Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Joel Ngwembe, alisema mahakama na wadau wake wamejiandaa kikamilifu katika mwaka mpya wa sheria kusikiliza kesi zinazofikishwa mahakamani.

Pia alisema wamejipanga kuhakikisha wanatoa haki kwa wakati kadri itakavyowezekana na kwamba haijalishi watakuwa wachache kiasi gani, lakini watafanya kazi.



Ofisa Uhamiaji wa Mkoa wa Mbeya, Shaaban Hatib (wa kwanza kushoto) na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, wakiwakagua watuhumiwa wa uhamiaji haramu raia wa Ethiopia waliokuwa wakisafirishwa kupitia Malawi kuelekea Afrika Kusini. **PICHA: KENETH NGELESI**

# Watendaji wa ardhi waonywa uzembe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewawashia moto watendaji wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji wa Jiji la Mbeya kutokana na uzembe unaosababisha mpangilio mbovu wa makazi ya wananchi na uvamizi wa maeneo ya wazi.

Amewapa watendaji hao siku 14 kuainisha maeneo yote ya wazi kwa mujibu wa ramani ya jiji hilo, ambapo alisema ikibainika kuwa kuna eneo la wazi limevamiwa na kujengwa nyumba atazibomoa.

Chalamila alisema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa anazungumza na wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri zote na maofisa biashara wakati alipokuwa anakabidhi vitambulisho 80,000 vya wajasiriamali awamu ya pili.

Ilikuwa ni siku chache baada ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wiliam Lukuvi, kutoridhishwa na mpangilio wa makazi katika jiji hilo, ambapo aliwalaumu maofisa hao kwa uwajibikaji wao mdogo.

Alisema amebaini kuwa kuna baadhi ya maeneo yalitengwa kuwa ya wazi, lakini maofisa ardhi wa Jiji wamepima viwanja na kuwauzia baadhi ya mabwenyenye ambao wamejenga nyumba za kuishi na za biashara.

Vilevile Chalamila alisema kuna hata baadhi ya maeneo maofisa hao wameuza viwanja vya kuchezea mpira watoto na hivyo akahimiza zoezi hilo lifanyike haraka, ili hatua zichukuliwe ikiwamo kuvunja miundombinu hiyo na maeneo hayo yaendelee kuwa ya wazi.

"Waziri Lukuvi juzi juzi alipokuwa hapa alisema Jiji letu limepangwa ovyo, sasa changamoto hiyo imesababishwa na maofisa ardhi wetu ambao hawatimizi majukumu yao ipasavyo, sasa mimi naanza nao," alisema Chalamila.


Katika hatua nyingine Chalamila alisema anashangazwa na baadhi ya maofisa ardhi wa Jiji hilo kupima viwanja vya makazi kwenye eneo la hifadhi ya Uwanja wa Ndege wa zamani wa Mbeya.

Alimwagiza Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa huo, Jeremia Minja, kufuatilia na kumpelekea taarifa kwa maandishi sababu za maofisa hao kupima eneo hilo.

Mwanzoni mwa wiki iliyopita, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alifanya ziara ya kushtukiza katika Jiji la Mbeya na kuzungumza na watumishi wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji, ambapo mbali na mambo mengine aliwataka wataalamu hao kutekeleza majukumu yao kwa weledi.

Alisema makazi ya wananchi katika Jiji hilo yamepangwa ovyo kutokana na maofisa ardhi na mipango miji kutotekeleza majukumu yao ya upimaji na utoaji wa hati miliki za ardhi kwa wananchi.

Alisema wananchi wanayapanga wenyewe makazi yao na hivyo kuwa miongoni mwa miji inayomkera kwenye masuala ya ardhi pamoja na ukusanyaji wa mapato.+





# Lugola ajitosa kupambana na mauaji ya vikongwe

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imevitaka vyombo vya ulinzi na usalama kupambana na mauaji ya vikongwe yanayofanyika katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na kwingineko ili kuyatokomeza hadi ifikapo 2020.

Mbali na hilo, serikali imelitaka Jeshi la Polisi kuendelea na mapambano ya mauaji ya watoto yanayofanyika katika Mkoa wa Njombe kuhakikisha yanatokomezwa. Akizungumza katika mkutano wa ufunguzi wa wadau wa kutetea haki za wazee na kupambana na mauaji dhidi yao Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola, alisema Jeshi la Polisi lina kila sababu ya kupambana na mauaji hayo ili wazee wakae sana kama ilivyo kwa watu wengine.

Alisema Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ishirikiane na wizara yake kuhakikisha wanayatokomeza mauaji hayo. "Hakuna muuaji ambaye atabaki salama kwa Jeshi la Polisi kila mmoja atafikiwa na zoezi hilo la kuwasaka," alisema Lugola.

Alisema lengo lao ni kuona kila mtu anaishi kwa amani iwe mzee, kijana na watoto, pia hakuna mtu mwenye mamlaka ya kumuua mzee akiuhisi kuwa ni mchawi kwa sababu suala hilo halikubaliki.

Alisema lengo lao kama wizara ni kuhakikisha mauaji ya vikongwe yanatokomezwa na kukomeshwa kabisa na kuongeza kuwa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imeainisha kutokomeza mauaji ya wazee kama moja ya lengo la kufikia katika kipindi cha miaka mitano. Alioshukuru Wizara ya Afya ambayo imepata mkakati ulioandaliwa na utakaratibiwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na serikali na idara nyingine.

"Tutafikia lengo tulilojiwekea katika mkakati wetu, tunahitaji kutokomeza mauaji yote," alisema Lugola. Alifafanua zaidi kuwa nchi inatakiwa kuwa salama na kila mmoja anatakiwa kuishi bila woga.

Naye mzee Hilda Jonas, alisema wazee nao wanahitaji mikopo ambayo wanapewa vijana wanawake na wao wanahitaji kuingizwa katika makundi hayo kwa sababu wana uhitaji.

Alisema wanahitaji nao kuingia bungeni ili waweze kutoa changamoto zao ambazo zinawakabili huko mitaani.



Wananchi katika Kijiji cha Igando, Kata ya Bwera, wilayani Chato, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (hayupo pichani), wakati alipofika kijijini hapo kuzindua huduma ya umeme. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yamrushia Lissu kombora

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amewataka wanasiasa kuacha tabia ya kulichafua taifa nje ya nchi kwa kuvikejeli vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na serikali kwa ujumla.

Dk. Bashiru aliyasema hayo juzi katika kijiji cha Nzali wilayani Chamwino mkoani Dodoma, wakati wa ufunguzi wa maadhimisho ya miaka 42 ya kuzaliwa kwa CCM.

Alisema hivi sasa ameibuka mwanasiasa mmoja ambaye anafanya siasa za kulichafuta taifa nje ya nchi kwa kueneza mambo ya uongo dhidi ya vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na serikali.

"Mwanasiasa huyu amekuwa akifanya fitina ya kulichafua taifa nje ya nchi na kudai serikali yetu inahusika katika kushambuliwa kwake," alisema bila kumtaja na kuongeza kuwa:

"Kuna watu wangapi walipata ajali tu wakapoteza maisha, lakini yeye kanusurika, Mungu kamnusuru anatakiwa kushukuru na siyo kuendeleza hiki anachokifanya, anataka kulichafua taifa na kuvifanya vyombo vyetu visiaminike kule ambako vilikuwa vimejijengea heshima."

Pamoja na kutokumtaja, mwanasiasa pekee ambaye yupo nje ya nchi na amekuwa akitoa kauli kadhaa hivi karibuni ni Mbunge wa Singida Mashariki, ambaye pia ni mwanasheria mkuu wa Chadema, Tundu Lissu.

Aidha, alisema kuwa wanasiasa wanatakiwa kuacha kutumia matamshi yao kama sehemu ya kujitafutia 'kiki' na kama wamechoka kukaa katika vyama ambavyo havina itikadi, wajiunge na CCM.

"Aje huku tumfundishe namna ambavyo wanasiasa anatakiwa kuwa sio kufanya siasa za kuchafuana kama ambavyo anafanya hivi sasa huko nje ya nchi... haiwezekani mtu anayetaka kuwa Rais wetu anakuwa na matamshi ambayo hayana tahadhari," alisema Dk. Bashiru.

Aliongeza kuwa serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na CCM haitakuwa tayari kumvumilia mtu ambaye anatumia nafasi yake vibaya kuvizalilisha vyombo vya ulinzi na usalama.

Akizungumza kuhusu uchaguzi mkuu mwakani, alisema kuwa chama hicho hakitawavumilia wabunge pamoja na madiwani mizigo.

"Tunatafuta wabunge bora na sio bora wabunge, mtu ambaye atakuwa hana uwezo siwezi kabisa mbeba katika chama changu tutaweka watu wenye uwezo ambao wataweza kuwatumikia wananchi," alisema.

## Sababu za wazee kuishi zaidi hizi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema umri wa kuishi kwa wazee umeongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na jitihada zinazofanywa na mashirika mbalimbali kwa kushirikiana nao.

Akizungunza jana, katika mkutano wa wadau wa kutetea mauaji ya vikongwe Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Faustine Ndugulile, alisema hali hiyo bado itaendelea kuongezeka kutokana na jitihada za serikali kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali kuwatunza.

"Tutaendelea kuwalinda hawa wazee kuhakikisha wanapata stahiki zote," alisema Ndugulile.

Alifafanua zaidi ya kuwa lengo ni kuona wazee hao wanaishi kama watu wengine.

Akizungumzia suala la matibabu, alisema wanajitahidi kuhakikisha wote wanapata bima za afya ili kuweza kupata matibabu.

Alisema wanajitahidi kuhakikisha sera ya afya ya 2003 ya wazee inaboreshwa ikiwamo haki ya wazee kupatikana.

Alisema suala hilo lazima watalifanyia kazi kwa ufasaha ili kila mzee anapata haki yake ya msingi.

Alisema kila mkoa utahitajika kuwa na Baraza la Wazee ambalo litasaidia kutetea na kusikiliza matatizo ya wazee.

Naye Mkurugenzi wa Helpage, Smart Daniel, alisema kwa sasa wana mafanikio makubwa hususan upande wa matibabu kila hospitali unazoenda wazee wanapewa kipaumbele.

Alisema hilo linawapa moyo kwa sababu inaonyesha jinsi gani kazi yao inaonekana.

Daniel alisema lengo lao ni kuona wazee malalamiko yao yanakwisha na mauaji yamepungua kwa sasa.

HABARI KITAIFA



Wana CCM wakifanya usafi kwenye maeneo ya jengo la Ofisi ya CCM Mkoa wa Mjini Magharibi Amani jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Operesheni kulinda misitu, hifadhi yatangazwa Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, amevitaka vyombo vya ulinzi na usalama mkoani humo kusimamia maelekezo yaliyotolewa na kamati yake kuimarisha amani na usalama mkoani humo.

Akizindua operesheni maalum ya kupambana na uhalifu mwishoni mwa wiki, Mahmoud alisema operesheni hiyo inakusudia kuzuia aina zote za uhalifu ikiwamo uhujumu wa misitu ya hifadhi.

Alisema kuwa katika operesheni hiyo, vikosi hivyo vitafuatilia na kutekeleza maelekezo na maagizo mbalimbali yaliyotolewa na kamati yake hivi karibuni, ikiwa na pamoja na mapambano dhidi ya biashara ya dada na kaka poa pamoja na usafiri wa pikipiki (bodaboda) katikati ya mji. Mkuu huyo wa mkoa alisema operesheni hiyo pia itayafikia maeneo mbalimbali yanayotumika au kushukiwa kuwa ni maficho ya wahalifu.

Aliwataka askari polisi na wa ulinzi shirikishi kufanya kazi hiyo bila uoga na kwa kushirikiana ili kukomesha vitendo viovu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Thobias Sedoyeka, alisema jeshi hilo limejipanga vyema kutekeleza operesheni hiyo, huku akiwataka viongozi na wananchi kujenga tabia ya kutii sheria bila kushurutishwa.

Alisema jeshi hilo lina taarifa za kuwapo kwa baadhi ya viongozi wa serikali na madereva wao wanaotumia magari yao kinyume cha utaratibu uliowekwa.

Alisema jeshi litatumia vipimo vya ulevi ili kubaini madereva wanaoendesha magari wakiwa wamelewa.

Kamanda Sedoyeka alibainisha kuwa, licha ya uhalifu kupungua mkoani humo katika kipindi cha robo ya mwisho wa mwaka jana, operesheni hiyo itatumika kufanyia kazi taarifa za kuwapo kwa viashiria vya uhalifu ndani ya mkoa huo.

Aliwataka wananchi wa maeneo ya mkoa huo kutoshtuka watakapoona makundi ya askari yakipita katika maeneo yao, badala yake watoe ushirikiano ili kufanikisha kuwanasa wahalifu.

# Ataka uwazi miradi ya Ukimwi, TB

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Abdallah Hassan Mitawi, amewataka wasimamizi wa miradi ya kudhibiti kifua kikuu (TB), Ukimwi na malaria, kutumia vyombo vya habari kutangaza mafanikio yaliyopatikana, ili kuongeza imani ya wananchi na wafadhili wa miradi hiyo.

Akifungua kikao cha tathmini ya utekelezaji wa miradi hiyo kilichowakutanisha wadau mbalimbali kwenye Ukumbi wa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale mwishoni mwa wiki, Mitawi alisema kufanya hivyo, kutongeza uelewa wa jamii juu ya maradhi hayo.

Alisema kufanikiwa kwa utekelezaji wa miradi hiyo kumeongeza umaarufu wa Zanzibar katika nchi zingine ambazo wataalamu wake wamekuwa wakitembelea Zanzibar kujifunza.

Alisema kwa kipindi kirefu, Zanzibar imeendelea kuwa na kasi ndogo ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), mafanikio ambayo yanapaswa kulindwa kwa kutumia mbinu na mikakati shirikishi miongoni mwa wadau wanaohusika na masuala ya huduma na udhibiti wa maradhi. Alisema kuwa kwa upande wa malaria, kuna mafanikio makubwa yaliyofikiwa, akibainisha kuwa, hadi sasa Zanzibar imefanikiwa kudhibiti kwa kiwango kikubwa maradhi hayo na kuitaka jamii kuendelea kushirikiana na mamlaka husika ili kuondoa kabisa maradhi hayo.

Alisema utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali ya kudhibiti maradhi hayo, ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2020, Mkuza awamu ya tatu na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, hivyo kutangazwa kwa mafanikio hayo, kutasaidia kuimarisha nguvu za wadau na wananchi.

Mitawi pia aliwashukuru washirika mbalimbali wa maendeleo wakiwamo Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia watoto (Unicef) na Mfuko wa Fedha (Global Fund) kwa kufadhili shughuli za taasisi hizo na kusaidia kupatikana kwa mafanikio hayo.

Awali, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi wa kudhibiti TB na Ukimwi, Dk. Farhat Jowhar, alisema shughuli mbalimbali zilitekelezwa kwa lengo la kudhibiti kasi ya maambukizi ya maradhi hayo, kutoa huduma bora kwa watu wanaoishi na VVU na kuondoa mitazamo hasi ya jamii kuhusu maradhi hayo.

Aliyataja mafanikio yaliyopatikana katika udhibiti wa TB kuwa ni pamoja na kupatia vifaa vya uchunguzi na udhibiti wa maradhi hayo vituo vya afya vya taasisi za kiraia na binafsi, kuwapatia tiba asilimia 99.3 ya wagonjwa na kuongeza idadi ya watumiaji wa dawa kutoka asilimia 95 mwaka 2017 na kufikia asilimia 96 mwaka jana.

Hata hivyo, Dk. Farhat, alisema kuwa licha ya mafanikio hayo, bado kuna changamoto kadhaa zinazopunguza ufanisi ikiwamo ya unyanyapaa dhidi ya watu wanaoishi na VVU pamoja na kutoendelea na matibabu kwa baadhi ya watu waliogundulika kuwa na maambukizo.

# 'Viongozi, wanachama CCM someni kanuni na miongozo'

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Zanzibar, Tunu, amewataka kina mama wa umoja huo kuendeleza utamaduni wa kusoma kanuni, miongozo na machapisho mbalimbali ya UWT na CCM ili wajue kwa upana majukumu yao, hasa kusimamia na kutekeleza kazi zao za kila siku.

Rai hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki katika ziara yake ya kujitambulisha kwa wajumbe wa Mabaraza ya UWT Wilaya za Mjini na Amani za Mkoa kwenye Ukumbi wa CCM uliopo Amani kisiwani hapa.

Alisema umoja huo una miongozo na kanuni zake zinazotakiwa kusomwa na viongozi na wanachama ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi.

Alisema kila kiongozi ndani ya umoja huo akijua ipasavyo muundo sahihi wa majukumu yake, mipaka na wajibu, itasaidia kutatua changamoto ya migongano na kutegeana kimajukumu na kuongeza ari kiutendaji.

Tunu alisema umoja huo umeweka utaratibu maalum na wa kudumu kwa viongozi na watendaji wa taasisi hiyo kufanya ziara za mara kwa mara katika maeneo mbalimbali ya kinamama kwa nia ya kubaini changamoto zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi kwa wakati.

Aliwataka wajumbe wa umoja huo kuepuka kujiingiza katika makundi yasiyofaa yanayoweza kuhatarisha umoja huo na kusababisha migogoro kwa UWT na CCM kwa ujumla.

Alisema wanawake wa UWT ndiyo jeshi kubwa la kisiasa la CCM, hivyo wajipange kisaikolojia kila mmoja kwa nafasi yake kuhakikisha chama kinashinda kwa kishindo katika uchaguzi mkuu wa mwakani.

Alisema ibara ya tano ya Katiba ya CCM ya mwaka 1977 imewaelekeza viongozi na wanachama kuhakikisha CCM inashinda kwa kila uchaguzi wa serikali za mitaa pamoja na uchaguzi mkuu wa serikali, na UWT inatakiwa kuwa mstari wa mbele kutekeleza matakwa hayo ya kikatiba.

Tunu pia alimpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, pamoja na Rais Dk. John Magufuli kwa juhudi zao za kusimamia vizuri utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2015/2020 na kulinda tunu za taifa.

Alisema juhudi za viongozi hao zinatakiwa kuthaminiwa kwa kuwa hivi karibuni kupitia Baraza la Mawaziri, waliamua kusamehe deni la umeme kwa Zanzibar iliyokuwa ikidaiwa Sh. bilioni 22 za tozo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Awali, akisoma risala ya umoja huo, Katibu wa UWT Mkoa wa Mjini, Stahamili Omar, alisema wamejipanga vizuri kutekeleza shughuli mbalimbali za kitaasisi sambamba na kubuni miradi ya ujasiriamali itakayoweza kukuza uchumi wa jumuiya na chama kwa ujumla.

Alisema miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuwainua kiuchumi kina mama kwa kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali ili wajikimu kimaisha.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 04 Feb**

| | |
|---|---|
| 06:00 | Al jazera |
| 08:00 | CNN International News |
| 09:00 | Al Jazeera |
| 10:00 | Kumekucha |
| 10:30 | Kumekucha Michezo |
| 11:30 | Kumekucha Kishindo |
| 12:00 | Turning the spotlight rpt: |
| 12:30 | Drive it rpt |
| 13:00 | Series rpt : Grapes of justice |
| 13:45 | Series rpt: Ode To Joy |
| 14:30 | Usafiri wako rpt |
| 15:00 | Cookery rpt: Culinary Delight |
| 15:30 | Toyota world of wildlife rpt |
| 16:00 | CNN International |
| 17:00 | Eco@Africa rpt |
| 17:30 | Meza huru |
| 19:00 | The Décor rpt |
| 19:30 | Business edition |
| 20:00 | Series: Grapes of Justice |
| 20:45 | The Monday Agenda |
| 21:30 | Capital Prime News |
| 22:00 | Kipima Joto |
| 00:00 | Al Jazeera |

**Tues 05 Feb**

| | |
|---|---|
| 06:00 | Al Jazeera |
| 08:00 | CNN International News |
| 09:00 | Al Jazeera |
| 10:00 | Kumekucha |
| 10:30 | Kumekucha Michezo |
| 11:30 | Kumekucha Kishindo |
| 12:00 | The Decor rpt |
| 12:30 | Mizengwe rpt |
| 12:45 | Aibu Yako |
| 13:00 | Series rpt: Grapes of justice |
| 13:45 | Series rpt: Ode To Joy |
| 14:15 | Local pgm rpt: Business Edition |
| 15:00 | Bundesliga kick off |
| 15:30 | Out and About rpt |
| 16:00 | Capchat rpt |
| 17:00 | Ripoti Maalum rpt |
| 17:30 | Meza huru |
| 19:00 | Innovation |
| 19:30 | Ripoti Maalum |
| 20:00 | Series: Grapes of Justice |
| 20:45 | Series: Ode To Joy |
| 21:30 | Capital Prime |
| 22:00 | Turning the Spotlight rpt |
| 22:30 | Iron Chef rpt |
| 23:30 | Al Jazeera |

**Wed 06 Feb**

| | |
|---|---|
| 06:00 | Al jazeera |
| 08:00 | CNN International News |
| 06:00 | Al Jazeera |
| 08:00 | CNN International News |
| 09:00 | Al Jazeera |
| 10:00 | Kumekucha |
| 10:30 | Kumekucha Michezo |
| 11:30 | Kumekucha Kishindo |
| 12:00 | Turning the Spotlight rpt |
| 12:30 | Culinary delight rpt |
| 13:00 | Series rpt: Grapes of Justice |
| 13:45 | Series rpt: Ode To Joy |
| 14:30 | Local Pgm: The Monday Agenda Rpt |
| 15:15 | Capchat rpt |
| 16:15 | CNN International |
| 17:00 | Innovation rpt |
| 17:30 | Meza Huru |
| 19:00 | Sports Gazette |
| 19:30 | Business edition rpt |
| 20:00 | Series: Grapes of Justice |
| 20:45 | Series: Ode To Joy |
| 21:30 | Capital Prime News |
| 22:00 | Dakika 45: |
| 22:45 | The Décor |
| 23:15 | Al Jazeera |

**Thurs 08 Feb**

| | |
|---|---|
| 06:00 | Al Jazeera |
| 08:00 | CNN International News |
| 09:00 | Al Jazeera |
| 10:00 | Kumekucha |
| 10:30 | Kumekucha Michezo |
| 11:30 | Kumekucha Kishindo |
| 12:00 | Sports Gazette |
| 12:30 | Out n' about rpt: |
| 13:00 | Series rpt: Grapes of Justice |
| 13:45 | Series rpt: Ode To Joy |
| 14:30 | Business Edition rpt |
| 15:00 | Korean Drama rpt: Emperor of the sea |
| 16:00 | Dakika 45 rpt |
| 17:00 | In good shape |
| 17:30 | Meza Huru |
| 19:00 | Turning the spotlight |
| 19;30 | Usafiri wako |
| 20:00 | Series: Grapes of Justice |
| 20:45 | Series: Ode To Joy |
| 21:30 | Capital Prime News |
| 22:00 | Capchat rpt |
| 23:00 | Al Jazeera |

**Frid 09 Feb**

| | |
|---|---|
| 06:00 | Al Jazeera |
| 08:00 | CNN International News |
| 09:00 | Al Jazeera |
| 10:00 | Kumekucha |
| 10:30 | Kumekucha Michezo |
| 11:30 | Kumekucha Kishindo |
| 12:00 | Innovation rpt |
| 12:30 | The Decor rpt |
| 13:00 | Series rpt: Grapes of Justice |
| 13:45 | Series rpt: Ode To Joy |
| 14:30 | Ripoti Maalum rpt |
| 15:00 | Korean Dram rpt: Emperor of the sea |
| 16:00 | CNN International |
| 16:30 | The Monday Agenda rpt |
| 17:30 | Meza Huru |
| 19:00 | Drive it |
| 19:30 | Eco@Africa |
| 20:00 | Aibu yako |
| 20:15 | Local Pgm: Business Edition |
| 20:45 | Series: Ode To Joy |
| 21:30 | Capital Prime News |
| 22:00 | Malumbano ya hoja rpt |
| 00:00 | Al Jazeera |

**Sat 10 Feb**

| | |
|---|---|
| 08:00 | CNN International |
| 09:00 | Drive It rpt |
| 09:30 | Turning the Spotlight rpt |
| 10:00 | Culinary delight rpt |
| 10:30 | Innovation rpt |
| 11:00 | Out n'about rpt |
| 11:30 | Sports Gazette rpt |
| 12:00 | Usafiri wako rpt |
| 12:30 | Eco@Africa rpt |
| 13:00 | Business edition rpt |
| 13:30 | Korean Drama rpt: Emperor of the sea |
| 14:30 | Telenovela rpt: Ode To Joy |
| 17:15 | Ripoti Maaalum rpt |
| 17:45 | Bundesliga kick off |
| 18:15 | Capchat rpt |
| 19:15 | Mizengwe |
| 19:30 | The Decor |
| 20:00 | Iron Chef. |
| 21:00 | Out n' about |
| 21:30 | Movie: Fangs |
| 23:00 | The other side rpt |
| 01:00 | Al Jazeera |

**Sun 03 Jan**

| | |
|---|---|
| 08:00 | CNN International |
| 09:00 | In good shape |
| 10:00 | Capchat rpt |
| 11:00 | Sports Gazette rpt |
| 11:30 | Iron chef rpt |
| 12:00 | Out n about rpt |
| 12:30 | Bundesligga Kick Off rpt |
| 13:00 | Ripoti Maalum |
| 13:30 | Series rpt: Grapes of Justice Inkulo |
| 15:15 | Aibu yako |
| 15:30 | Drive it rpt |
| 16:00 | Dakika 45 rpt |
| 16:45 | Mizengwe rpt |
| 17:00 | The Decor rpt |
| 17:30 | Meza huru |
| 19:00 | Turning the Spotlight rpt |
| 19:30 | Cookery pgm:Culinary Delights |
| 20:00 | Korean Drama rpt: Emperor of the sea |
| 21:00 | Shift |
| 21:15 | Capchat live |
| 22:15 | Telenovela: Ode To Joy |
| 00:00 | Al Jazeera |

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 04 Feb**

| | |
|---|---|
| 05:30 | Uwanja wa Mazoezi |
| 06:00 | Habari |
| 06:40 | Kumekucha |
| 07:30 | HABARI |
| 08:00 | Kumekucha Michezo |
| 08:55 | Habari za saa |
| 09:00 | Kumekucha Kishindo |
| 09:30 | Isidingo |
| 09:55 | Habari za saa |
| 10:00 | Watoto wetu |
| 10:30 | Igizo: Hatua |
| 10:55 | Habari za saa |
| 11:00 | Kimya Milele |
| 11:55 | Habari za saa |
| 12:00 | Al Jazeera |
| 12:30 | Jungu kuu rpt |
| 12:55 | Habari za saa |
| 13:00 | Mjue Zaidi |
| 13:55 | Habari za saa |
| 14:00 | Telenovela: Destiny (Destino) |
| 14:55 | Habari za saa |
| 15:00 | Meza Huru |
| 16:30 | Watoto Wetu |
| 17:00 | The Base |
| 18:00 | Jiji Letu |
| 18:10 | Aibu yako rpt |
| 18:15 | Huduma ya kwanza |
| 18:30 | Shamba shape up |
| 19:00 | Afya ya Jamii |
| 19:30 | Isidingo |
| 20:00 | Habari |
| 21:05 | Dakika 45 |
| 21:50 | Kipindi Maalum: St Patrick School |
| 22:00 | Telenovela: Destiny (Destino) |
| 23:00 | Habari |
| 23:30 | The Base |
| 00:30 | Al Jazeera |
| 02:00 | CNN International |

**TUESDAY 05 Feb**

| | |
|---|---|
| 05:30 | Uwanja wa Mazoezi |
| 06:00 | Habari |
| 06:40 | Kumekucha |
| 07:30 | HABARI |
| 08:00 | Kumekucha Michezo |
| 08:55 | Habari za saa |
| 09:00 | Kumekucha Kishindo |
| 09:30 | Isidingo |
| 09:55 | Habari za saa |
| 10:00 | Watoto wetu |
| 10:30 | Hawavumi lakini wamo |
| 10:55 | Habari za saa |
| 11:00 | Hawavumi lakini wamo |
| 11:15 | Igizo: Mtego |
| 11:55 | Habari za saa |
| 12:00 | Al Jazeera |
| 12:30 | Afya ya jamii rpt |
| 12:55 | Habari za saa |
| 13:00 | Uchumi na biashara |
| 13:30 | Kipindi Maalum rpt : TFDA |
| 13:55 | Habari za saa |
| 14:00 | Huduma ya kwanza |
| 14:15 | Telenovela: Destiny (Destino) rpt: |
| 14:55 | Habari za saa |
| 15:00 | Meza Huru |
| 16:30 | Watoto wetu |
| 17:00 | The Base |
| 18:00 | Jiji Letu |
| 18:15 | Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk |
| 19:00 | Jarida la wanawake |
| 19:30 | Isidingo |
| 20:00 | Habari |
| 21:00 | Kipindi maalum: |
| 22:15 | Telenovela: Destiny (Destino) |
| 23:00 | Habari |
| 23:30 | The Base |
| 00:30 | CNN International |

**WEDNESDAY 06 Feb**

| | |
|---|---|
| 05:30 | Uwanja wa Mazoezi |
| 06:00 | HABARI |
| 06:40 | Kumekucha |
| 07:30 | HABARI |
| 08:00 | Kumekucha Michezo |
| 08:55 | Habari za saa |
| 09:00 | Kumekucha Kishindo |
| 09:30 | Isidingo |
| 09:55 | Habari za saa |
| 10:00 | Watoto wetu |
| 10:30 | Shamba shape up |
| 10:55 | Habari za saa |
| 11:00 | Korean: The Great Queen Seonduk |
| 11:55 | Habari za saa |
| 12:00 | Al Jazeera |
| 12:30 | Jarida la wanawake rpt |
| 12:55 | Habari za saa |
| 13:00 | Dakika 45 |
| 13:55 | Habari za saa |
| 14:00 | Telenovela rpt: Destiny (Destino): |
| 14:55 | Habari za saa |
| 15:00 | Meza Huru |
| 16:30 | Watoto Wetu |
| 17:00 | The Base |
| 18:00 | Jiji Letu |
| 18:15 | Mapishi rpt |
| 18:30 | Ijue Sheria |
| 19:00 | Kipindi Maalum: TFDA |
| 19:30 | Isidingo |
| 20:00 | Habari |
| 21:00 | Aibu Yako! Hata wewe? |
| 21:10 | Kipindi Maalum : Uongozi |
| 21:40 | Kipindi Maalum: Tanesco |
| 22:15 | Telenovela: Destiny (Destino) |
| 23:00 | Habari |
| 23:30 | The Base |
| 00:30 | Al Jazeera |
| 02:00 | CNN International |

**THURSDAY 07 Feb**

| | |
|---|---|
| 05:30 | Uwanja wa Mazoezi |
| 06:00 | HABARI |
| 06:40 | Kumekucha |
| 07:30 | HABARI |
| 08:00 | Kumekucha Michezo |
| 08:55 | Habari za saa |
| 09:00 | Kumekucha Kishindo |
| 09:30 | Isidingo |
| 09:55 | Habari za saa |
| 10:00 | Watoto wetu |
| 10:30 | Igizo: Hatua |
| 10:55 | Habari za saa |
| 11:00 | Igizo: Hatua |
| 11:15 | Usafiri wako |
| 11:55 | Habari za saa |
| 12:00 | Al jazeera |
| 12:30 | Ijue Sheria |
| 12:55 | Habari za saa |
| 13:00 | Kipindi Maalum rpt |
| 13:30 | Jungu Kuu |
| 13:55 | Habari za saa |
| 14:00 | Telenovela rpt: Destiny (Destino) |
| 14:55 | Habari za saa |
| 15:00 | Meza Huru |
| 16:30 | Watoto Wetu |
| 17:00 | The Base |
| 18:00 | Jiji Letu |
| 18:15 | Huduma ya kwanza rpt |
| 18:30 | Kipindi Maalum: Ewura |
| 19:00 | Usafiri wako |
| 19:30 | Isidingo |
| 20:00 | Habari |
| 21:00 | Malumbano ya hoja |
| 23:00 | Habari |
| 23:30 | The Base |
| 00:30 | CNN International |

**FRIDAY 08 Feb**

| | |
|---|---|
| 05:30 | Uwanja wa Mazoezi |
| 06:00 | HABARI |
| 06:40 | Kumekucha |
| 07:30 | HABARI |
| 08:00 | Kumekucha Michezo |
| 08:55 | Habari za saa |
| 09:00 | Kumekucha Kishindo |
| 09:30 | Isidingo |
| 09:55 | Habari za saa |
| 10:00 | Watoto wetu |
| 10:30 | Hawavumi lakini wamo |
| 10:55 | Habari za saa |
| 11:00 | Hawavumi lakini wamo |
| 11:20 | Usafiri wako |
| 11:55 | Habari za saa |
| 12:00 | Al Jazeera |
| 12:30 | Kipindi Maalum rpt: TCRA |
| 12:55 | Habari za saa |
| 13:00 | Kipindi maalum: Tanesco |
| 13:30 | Kipindi Maalum rpt - Uongozi |
| 13:55 | Habari za saa |
| 14:00 | Mapishi |
| 14:15 | Telenovela rpt: Destiny (Destino) |
| 14:55 | Habari za saa |
| 15:00 | Meza huru |
| 16:30 | Watoto wetu |
| 17:00 | The Base |
| 17:30 | Ibada ya kiislamu |
| 18:00 | Jiji Letu |
| 18:15 | Igizo: Mizengwe |
| 18:30 | Uchumi na biashara |
| 19:00 | Kipindi maalum: TCRA |
| 19:30 | Isidingo |
| 20:00 | Habari |
| 21:05 | Kipima joto |
| 23:00 | Habari |
| 23:30 | The Base |
| 00:30 | CNN International |

**SATURDAY 09 Feb**

| | |
|---|---|
| 05:30 | Uwanja wa Mazoezi |
| 06:00 | HABARI |
| 06:40 | Kumekucha |
| 07:00 | Habari |
| 08:00 | Al Jazeera |
| 09:00 | Watoto wetu |
| 10:00 | Mjue Zaidi rpt |
| 11:00 | Jungu kuu rpt |
| 11:30 | Usafiri wako |
| 12:00 | Shamba Shape up |
| 12:30 | Telenovela rpt: Destiny (Destino) |
| 14:45 | Igizo rpt: Riziki |
| 15:15 | Igizo rpt: Hatua |
| 15:45 | Igizo rpt: Mizengwe |
| 16:00 | Igizo rpt: Kimya Milele |
| 16:30 | Igizo: Mtego rpt |
| 17:00 | Shamsham za Pwani |
| 18:00 | Jiji Letu |
| 18:15 | Mapishi |
| 18:30 | Igizo: Riziki |
| 19:00 | Sanaa na wasanii |
| 19:30 | Jungu Kuu |
| 20:00 | Habari |
| 21:00 | Igizo: Kimya Milele |
| 21:30 | Hawavumi lakini wamo |
| 22:30 | Isidingo rpt |
| 01:00 | CNN International |

**SUNDAY 10 Feb**

| | |
|---|---|
| 05:30 | Uwanja wa Mazoezi |
| 06:00 | HABARI |
| 06:40 | Kumekucha |
| 07:00 | Habari |
| 08:00 | Al jazeera |
| 09:00 | Watoto Wetu |
| 10:00 | Isidingo |
| 11:45 | Aibu Yako |
| 11:50 | Hawavumi lakini wamo rpt |
| 12:50 | Bongo Movie rpt: Fundi Rama 2 |
| 14:00 | Tamasha la Michezo |
| 15:00 | Mwangaza |
| 16:00 | Korean drama: The great queen Seonduk |
| 16:45 | Mjue zaidi |
| 17:30 | Kipindi cha kikristo |
| 18:00 | Jiji Letu |
| 18:15 | Mapishi |
| 18:30 | Mizengwe rpt |
| 18:45 | Matukio ya wiki |
| 19:30 | Igizo: Mtego |
| 20:00 | Habari |
| 21:05 | Mizengwe |
| 21:00 | Bongo Movie: Green light |
| 22:00 | Telenovela rpt: Destiny (Destino) |


EATV



UJENZI

LEO USIKU SAA 3:00



JUMATATU

11:00 DADAZ (live)
15:00 FUNGUKA
16:00 UTAKE
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 KURASA
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 UJENZI
21:30 5SPORTS LIVE
22:30 BONGO HITS

*Ujenzi Fahamu mambo mbalimbali kuhusu ujenzi, mapambo ya nyumba nje na ndani, mitindo na teknolojia tofauti zitumikazo kwenye ujenzi.*

eastafrica RADIO

05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise

88.1FM DAR ES SALAAM


## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

| TIME | MONDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

| TIME | TUESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | WEDNESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | THURSDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | FRIDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | SATURDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

| TIME | SUNDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

## HABARI KIMATAIFA

# Gavana atakiwa kujiuzulu kisa ubaguzi

**WASHINGTON, Marekani**

GAVANA wa Jimbo la Virginia, Ralph Northam ametakiwa kujiuzulu baada ya kudhihirika kuwa aliweka picha ya ubaguzi wa rangi katika kitabu chake cha picha za kumbukumbu cha chuo cha udaktari zaidi ya miaka 30 iliyopita.

Hata hivyo, Northam ameomba msamaha kwa kueleza kuwa ubaguzi na matusi hayo katika mavazi ambayo yaliwekwa ndani ya kitabu hicho.

Katika tamko alilolitoa kupitia picha ya video Northam alisema picha hiyo haiendani na yeye alivyo hivi leo.

"Siwezi kubadilisha maamuzi niliyofanya, wala kurekebisha madhara yaliyoletwa na tabia yangu ya wakati huo na hivi leo," alisema na kuongeza.

"Lakini nakubali kuwajibika kwa vitendo vyangu vilivyopita, na niko tayari kufanya bidii kurejesha imani yenu kwangu."

Kurasa ya kitabu hicho kinapicha ya mtu mwenye uso mweusi na mwengine amevaa mavazi ya kikundi cha ubaguzi wa rangi kilichokuwa na mavazi ya kutisha na kuficha utambulisho wao maarufu kama Ku Klux Klan garb.

Gavana ameeleza kuwa yeye ni moja wao katika hiyo picha lakini hajajitambulisha ni yupi kati yao.

Kikundi cha wabunge Wamarekani weusi na cha Baraza la wawakilishi weusi la Virginia vimemtaka mara moja ajiuzulu.

"Ralph Northam alikuwa na karne tatu za kujitambua zaidi lakini ni hivi sasa anakiri kitendo hiki cha ubaguzi wa rangi, kuomba msamaha hivi sasa haitoshi. Ni lazima ajiuzulu," Kikundi cha wabunge weusi walituma ujumbe huo kwenye ukurasa wa twitter.

***VOA***

# Kaburi lenye miili 50 lapatikana Misri

**CAIRO, Misri**

MIILI 50 iliokuwa imehifadhiwa na inayodaiwa kutoka katika enzi za Ptolemaic (miaka ya 305-30BC) imepatikana na mwanakiolojia, kulingana na wizara ya vitu vya zamani.

Miili hiyo ambayo 12 kati yao walikuwa ni watoto ilipatikana katika makaburi manne yenye kina cha urefu wa mita tisa katika eneo la Tuna El-gebel huko Minya kusini mwa mji mkuu wa Cairo.

Baadhi ya miili hiyo ilikuwa imefungwa ndani ya kitambaa huku mingine ikiwa ndani ya majeneza ya mawe na ya mbao.

Taaifa zaidi zinaeleza kuwa miili ya watu hao bado haijatambulika ni ya akina nani lakini maafisa wa polisi wanasema huenda walishikilia nyadhifa za juu.

***BBC***

# Fayulu akataa wito wa maridhiano wa Tshisekedi

**Congo, Kinshasa**

KIONGOZI wa upinzani katika Jamhuri ya Kidemokrasia Congo Martin Fayulu amekataa wito wa Rais mpya wa nchi hiyo Felix Tshisekedi za kutaka maridhiano.

Wito huo wa maridhiano umetolewa na Rais, Tshisekedi lakini Fayulu alisema "Pale unapopewa mkono ambao ni mchafu, hupaswi kuupokea".

Kwenye hotuba yake rasmi ya kwanza tangu kushindwa kwenye uchaguzi wa rais, Fayulu aliwaambia mamia ya wafuasi wake waliokusanyika mjini Kinshasa kuwa wasifanye fujo wakati anapoendelea kupinga uchaguzi anaodai ulikumbwa na udanganyifu.

Kiongozi huyo wa upinzani ameuhimiza Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU) kutopokea maagizo kutoka kwa mtu anayedai kuwa Wakongo hawakumchagua.

Tshisekedi aliapishwa kuwa rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo Januari 24, mwaka huu katika makabidhiano ya kwanza ya madaraka kwa njia ya amani katika taifa hilo tangu lipate uhuru karibu miaka 60 iliyopita.

Baada ya matokeo kutangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi nchini Congo (CENI), Fayulu aliyaita matokeo hayo kuwa ni mapinduzi ya uchaguzi.

Tshisekedi alitangazwa mshindi katika uchaguzi huo uliofanyika mwezi Desemba mwaka jana kwa kupata asimilia 38.57 ya kura dhidi ya asilimia 34.8 za Fayulu. CENI ilimtangaza mgombea aliyekuwa akiungwa mkono na Rais Joseph Kabila kushika nafasi ya tatu akiwa na asilimia 23.8.

***DW***



Papa Francis akibadilishana zawadi na Sheikh Ahmed Mohamed el-Tayeb, kushoto, Imam wa Chuo Kikuu cha al-Azhar huko Vatican. **PICHA REUTERS**

# Maelfu washiriki maandamano Venezuela

**CARACAS, Venezuela**

KIONGOZI wa upinzani nchini Venezuela, Juan Guaido awaambia wafuasi wake anatarajia kufanya mabadiliko ya haraka wakati mikutano ya hadhara ikivutia watu 100,000 nchini humo.

Guaido ambaye alijitangaza kuwa rais wa mpito nchini humo alitoa wito wa maonyesho ya amani dhidi ya serikali ya Rais Nicolas Maduro.

Vuguvugu la upinzani la Guaido limeshaandaa maandamano 333 ya kuipinga serikali nchini Venezuela, huku tukio kubwa zaidi likifanyika katika mji mkuu Caracas na kuhudhuriwa na watu zaidi ya 100,000.

Waandamaaji hao walitoa wito wa kuondolewa kwa Maduro. Rais huyo wa Venezuela alianza muhula mpya wa miaka sita mwezi Januari, baada ya kushinda uchaguzi wa rais uliozingatiwa na baadhi ya mataifa na jumuiya za kimataifa kukosa uhalali wa kisheria.

Takribani ni muda wa wiki mbili imepita baada ya kujitangaza kuwa kaimu mkuu wa serikali, Guaido aliwaambia wafuasi wake kwamba "mabadiliko yako njiani Venezuela." "Maduro hamlindi yeyote, katiba ndiyo inafanya hivyo,".

Guaido aliitisha maandamano mengine Februari 12, kabla ya kuzungumzia masahibu ya wale walioathirika na mgogoro wa kiuchumi wa taifa hilo.

"Kuna Wavenezuela kati ya 250,000 na 300,000 walioko katika hatari ya kufa, Leo tunatangaza muungano wa kimataifa wa msaada wa kibinadamu na uhuru nchini Venezuela," Guaido aliuambia mkutano.

Gauido alisema upinzani utaanza haraka kusambaza msaada kutoka Colombia na Brazil, huku akiwahimiza wanajeshi kuruhusu ugavi wa mahitaji muhimu kuingia nchini, ambao Maduro ameuzuia kwa sasa. Kilomita kadhaa kutoka hapo, Chama cha Maduro cha Kisoshalisti kiliadhimisha miaka 20 tangu hayati Hugo Chavez, mlezi wa kisiasa na mtangulizi wa Maduro alipoingia madarakani.

Maelfu ya wafanyakazi wa serikali na wafuasi wa Maduro, wakiwamo wanachama wa kundi la wanamgambo wanaoiunga mkono serikali, walikusanyika katika mtaa wa Bolivar katikati mwa Caracas.

Mbele ya wafuasi wake, Maduro kwa mara nyingine alipendekeza kuitisha uchaguzi wa mapema wa bunge mwaka huu. Pendekezo hilo linaonekana kama jaribio la kuwapiku wapinzani, wanaodhibiti bunge la taifa.

***DW***

# Wafanyabiashara D'Salaam walalamikia huduma choo

**Na Margreth Emily,**

**TUDARCo**

=WAFANYABIASHARA wa soko la Shekilango, Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, wanalalamikia huduma mbovu za choo cha soko ambacho hakitoshelezi mahitaji na kujaa kila baada ya muda fupi.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wafanya biashara walisema ukosefu wa huduma ya choo katika soko hilo ni kero kubwa na hatari kwa afya zao.

=Aidha, walisema uondoshaji wa takataka nalo ni tatizo kubwa na kusababisha nyingi kubaki sokoni humo licha ya kutoa ushuru kila siku.

Betty Daniel, alisema shimo la choo cha soko hilo ni fupi hivyo hujaa mara kwa mara na kuna uwezekano mkubwa ya kuwa chanzo cha magonjwa mbalimbali ya kuambukiza.

="Choo ni kichafu sana na hakuna huduma ya maji na kina shimo dogo lisiloweza kuhilimili uwingi wa uchafu wa watu wote hivyo hujaa kila baada ya siku mbili au tatu ukizingatia kipo mbele ya soko kwahiyo harufu kali hutoka, kwa kweli hadhi ya soko na choo kilichopo ni tofauti kabisa, tunaugua magonjwa ya njia ya mkojo yaani UTI," alisema.

=Naye, Sam Ngudunga, alisema lipo tatizo la muda mrefu la uondoshaji wa takataka kwenye soko ambazo hukaa muda mrefu na kutoa harufu na wadudu kama nzi na wengine na hivyo kutuweka katika hatari ya kupata magonjwa.

="Hapa sokoni hali si ya kuridhisha kuna harufu ya takataka zilizooza, choo kina jaa mara kwa mara, gari la takataka linatakiwa kuja kila baada ya siku mbili lakini inafika hata wiki hazijatolewa na soko linakuwa linanuka sana,"alisema.

=Aidha, alisema ni vyema Manispaa hiyo ikawajibika kuzoa takataka hizo kama inavyowajibika kukusanya fedha za ushuru kila siku, ambao unapaswa kuhusika kwenye kusafisha soko hilo.

=Mwenyekiti wa soko hilo, David Mrisho, alithibitisha kuwapo kwa changamoto ya choo na uzoaji wa takataka kwa kuwa hakuna gari na miundombinu ya choo ni chakavu.

="Choo cha Manispaa ni kidogo na hakiwezi kukidhi mahitaji ya watumiaji, hapa kuna wafanyabiashara zaidi ya 1,000 na matundu ni matano tu yatumike kwa huduma za choo na kuoga hii ni changamoto magonjwa ni mengi kwa hali hii kunaweza kutokea mlipuko wa magojwa,"alisema.

=Alisema choo hicho kinasimamiwa na Manispaa toka mwaka jana baada ya kamati ya soko kunyang'anywa na kuwapa halmashauri.

="Choo kinapokuwa kimejaa utoaji wa maji taka unachukuwa muda mrefu tofauti na kamati ilivyokuwa inasimamia, kinaweza kukaa hata wiki nzima kimefungwa kwa wingi wa wafanyabiashara na Manispaa ndiyo inayowajibika," alisema.

=Aidha, alisema kwa sasa wanategemea choo cha mwekezaji ambacho kimeweza kukidhi mahitaji yao.

=Kuhusu gari la takataka, alisema ucheleweshwaji wa kuondoa takataka husababisha uharibifu wa hali ya hewa katika soko hilo.

="Kwa kawaida gari la taka linatakiwa kupita mara mbili kwa wiki, lakini linapita mara moja na takataka nyingi za hapa ni za manyoa ya kuku na maji maji hivyo huoza na kuharibu hali ya hewa. Hawatupi jibu la kueleweka kwanini wanashindwa kuzoa takataka licha ya sisi kulipa ushuru kila siku," alihoji.



Waombolezaji wakiulaza mwili wa aliyekuwa mvumbuzi wa madini ya tanzanite, Mzee Jumanne Ngoma, katika Kijiji cha Makanya, Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: MARY MOSHI**

# Bil. 1.5/- kujenga hospitali ya wilaya

**Na Friday Simbaya, MUFINDI**

SERIKALI imetenga zaidi ya Sh. bilioni 1.5 kwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya kisasa ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Festo Mgina, wakati wa kikao cha baraza la madiwani.

Baraza hilo ambalo lilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za kamati zake wakati wa uchangiaji, madiwani wameishukuru serikali kwa kuwapatia fedha takribani Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali mpya ya kisasa ya Halmashauri hiyo katika Kata ya Igowole.

Mgina alimtaka mkandarasi aliyepata fursa ya ujenzi wa hospitali hiyo kutekeleza mradi huo kwa wakati na kufanya kazi kwa weledi wa hali ya juu ili kuleta ufanisi na ubora unaotakiwa kwa muda mwafaka.

Aidha, aliwatahadharisha watumishi watakaojaribu kukwapua au kuhujumu fedha za ujenzi huo, na kwamba baraza lake halitawafumbia macho bali litawashugulikia ipasavyo kuhakikisha fedha zilizotolewa na serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI zinatumika kwa matumizi yaliyopangiwa ya kuboresha afya za Watanzania.

Hafla ya utiaji saini wa kandarasi hiyo ulifanyika katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ambapo majengo saba muhimu yatajengwa kwa awamu ya kwanza ambayo ni la utawala, la wagonjwa wa nje, la kuhifadhi dawa, la kufulia, mionzi, la wazazi sanjari na la maabara ambapo yanatarajiwa kukamilika kwa miezi 8.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Agape Fue, alihakikishia baraza hilo kuwa yeye na wataalamu wenzake watafanya kazi kwa bidii kuhakikisha ujenzi huo unakamilika kwa wakati na ubora wa hali ya juu, kwa kuwa wameshaunda kamati ya ufuatialiaji kwa kila hatua.

Kwa upande wake mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa wa Iringa, Sifael Kivamba, amewataka watumishi wa wilaya hiyo kushirikiana na madiwani kuhakikisha wanasimamaia ipasavyo kukamilika kwa hospitali hiyo na kujengwa katika ubora.

# Pinda ajitosa kumng'oa Msigwa

INATOKA UK 8

nacho ni kwamba hatujawathamini, sasa tusahihishe hili kosa na kulisahihisha naomba mimi nianze na hili zoezi kesho kukutana na mabalozi," alisema Pinda.

Alisema kosa la nne ni kwamba hakuna kiongozi yoyote ambaye kwa asilimia 100 ni malaika atakuwa na upungufu wake kama mwanachama mmoja mmoja alivyo.

"Tatizo kubwa wana-Iringa hawajui kusameheana, ndugu zangu hakuna mwanadamu aliyekamilika kwenye siasa hizi na mimi kama mlezi lazima tuvumiliane, kusameheana kwa lengo la kwenda mbele kwa sababu wananuniana hadi wanaathiri shughuli za chama," alisema Pinda na kuongeza:

"Na matatizo huwa yanatokea kwa viongozi wawili katibu na mwenyekiti wake ikifika wakati wa uchaguzi kila mtu anakuwa na mtu wake na kukigawa chama, ifike mahala tumalize haya makundi, tusemane ili tujenge chama."

Kosa lingine ambalo aliomba wasilifanye ni la udini na ukabila, na kwamba Iringa inasemwa sana kwa kuwa na udini pamoja na ukabila na kuongeza watakapokutana uso kwa uso anataka kila mmoja aseme ukweli tatizo hilo ni kitu gani kwa sababu wasipokubaliana wataenda hadi uchaguzi.

Kosa la sita waziri huyo alisema ni shetani anayeitwa fedha. Alisema tatizo la fedha lipo pande zote na kwamba inapofika kipindi cha uchaguzi watu wanadhani ni kipindi cha mavuno na kuwatahadharisha kwamba wakiingia kwenye ugonjwa huo wajue wameumia na anayefanya hivyo siku zote hajiamini kwa kuwa ana upungufu mbalimbali.



# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

## ELIMU/MAFUNZO

**NAFASI ZA MASOMO:** Tanzania research and Career development institute. Reg pwf/041.Certificate na diploma za kilimo,mifugo, na maendeleo ya jamii.Mawasiliano:0767574701/0758753063.www.tracdi.ac.tz

## NAFASI ZA KAZI

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 – 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA

YAKO KWA BEI NAFUU

## NYUMBA INAUZWA

Nyumba inauzwa ipo maeneo ya tabata chan'gombe.

Ina vyumba vya kulala vitatu, kimoja ni master. Ina store, Jiko, Sebule, dining na Parking ya kutosha.

**Bei ni nafuu sana.**

**Mawasiliano: 0786058343/ 0622 096682 /0654 969280**

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO? Nipashe

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

*Uza,*

*Chenye Thamani Kubwa*

*Kwa Kutangaza Nasi*

*Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0767 223311*

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Gattuso kumbakisha Bakayoko AC Milan

**MILAN, Italia**

KOCHA wa AC Milan, Gennaro Gattuso, anata kumsajili kwa mkataba wa kudumu Tiemoue Bakayoko ambaye anacheza hapo kwa mkopo akitokea Chelsea na anaamini kwamba kiungo huyo anaweza kuwa muhimu zaidi kwa miaka mingi hapo katika dimba la San Siro.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, mchezaji wa zamani wa Monaco hakuwa na msimu nzuri kwenye Ligi Kuu ya England msimu uliopita na hivyo kupelekwa kwenye Serie A.

Lakini alipotua Italia alionekana kuwa kwenye kiwango kizuri na Gattuso anaamini kwamba Bakayoko atakuwa na msaada mkubwa kwa timu hiyo kwa miaka mingi ijayo.

Mapema wiki hii, Bakayoko aliliambia Gazeti la Corriere dello Sport kwamba ndoto yake ni kubakia na Rossoneri hao na Gattuso ameonyesha nia ya kumuunga mkopo.

"Kwa wakati huu hatuwezi kumuacha, anatakiwa kubakia Milan," alisema akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wake wa jana dhidi ya Roma.

"Ana uwezo mkubwa dimbani. Unajua kwamba amekuja hapa kucheza kwa mkopo, lakini anaonekana kuwa muhimu zaidi kwetu," aliema Gattuso.

"Anaweza kuja kuwa mchezaji muhimu zaidi kwa klabu hii kwa miaka mingi."

Mchezaji mwingine ambaye Gattuso amemsajili ni Krzysztof Piatek, akifurahia kuanza kuichezea timu hiyo baada ya kufunga mabao mawili kwenye mchezo wake wa kwanza kuichezea timu hiyo, wakati ikiibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Napoli.







# Messi, Ronaldo vita bado ngumu Ulaya

**BARCELONA, Hispania**

WASHAMBULIAJI Lionel Messi wa Klabu ya Barcelona na Cristiano Ronaldo wa Juventus, bado ushindani wao barani Ulaya unaendelea kuwa mgumu baada ya wawili hao usiku wa kuamkia juzi kila mmoja kufunga mabao mawili.

Pamoja na wote kuzifungia timu zao mabao mawili, lakini hazikuondoka na ushindi, kwa kuwa zilitoka sare.

Messi alifunga mara mbili kuiwezesha Barcelona kupata sare ya 2-2 na Valencia kwenye Uwanja wa Nou Camp ukiwa ni mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania juzi Jumamosi.

Huku Ronaldo naye alifunga mabao mawili na kuifanya Juventus kutoka sare ya 3-3 na Parma kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia Serie A.

Hadi sasa Messi amefunga mabao 21 kwenye Ligi Kuu ya La Liga, huku Ronaldo akifunga mabao 17.

Wachezaji hao wawili kwa usiku huo walifanikiwa kuziokoa timu zao kutoka kwenye kipigo.

Ndani ya msimu huu wa 2018/19, Messi tayari ametupia mabao 29 kwenye michezo yote ya kimashindano aliyoichezea Barcelona, huku Ronaldo akitupia mara 19 ndani ya Juventus.

# KLOPP HANA WOGA MBIO ZA UBINGWA

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesisitiza kwamba hana woga wakati kikosi chake kikiendelea na mbio zake za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ya hapa England.

Vijana hao wa Klopp leo Jumatatu watakuwa ugenini kucheza na West Ham, siku moja baada ya wapinzani wao kwenye mbio hizo Manchester City kucheza na Arsenal.

Mshindi huyo mara mbili wa Kombe la Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, akiwa na Borussia Dortmund, Klopp amesema hajawahi kuwa na woga kuhusu timu yake kwa kuwa akili yake ni kuhakikisha wanashinda kila mchezo.

"Mimi si mtu wa kuogopa na hivyo sijawahi kuwa muoga kabla ya kushinda taji langu la kwanza nikiwa na Dortmund. Na sasa bado niko hivyo hivyo," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Uzoefu umenionyesha mimi kuwa kile



nilichokifanya huko nyuma, hakijabadilika. Kitu pekee ninachokijua ni kwamba kuhakikisha nakuwa makini na kazi yangu na kujiamini kwa kile ninachokifanya.


"Halafu kama upo fiti, itatokea tu kuwa na matokeo mazuri. Kama hauko vizuri hutaweza kupata matokeo mazuri. Hiyo ndio njia rahisi. Kitu cha kubadilisha hali zetu ni soka. Hicho ndicho kitu pekee tunaweza kukifanya."

Uwezo wa Klopp aliouonyesha msimu uliopita wakati Liverpool ikitinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ni uzoefu tosha kwake, kwa kuwa aliweza kukabiliana na presha kubwa.

Lakini wakati Liverpool ikiwa haijashinda taji la Ligi Kuu tangu mwaka 1990, Klopp anaelewa kwamba mashabiki wana hamu kubwa ya kupata mafanikio hayo.

"Kutakuwa na hofu? Ndio. Lakini usiwafanye wao kuwa wakubwa kuliko walivyo kwa sababu kulikuwa na hali ya woga mwaka jana, miaka miwili iliyopita, au miaka mitatu," aliongeza.

## HABARI MICHEZO



# RONALDO
## ALAUMU MAKOSA YA JUVE

**TURIN, Italia**

NYOTA wa Juventus, Cristiano Ronaldo hakuwa na furaha wakati timu yake ilipotoka sare ya mabao 3-3 na Parma kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, juzi Jumamosi.

Ronaldo alifunga mabao mawili na kuifanya Juve kuongoza kwa 3-1, kabla ya Gervinho kufunga mawili yaliyoiwezesha Parma kupata sare hiyo kwenye Uwanja wa Allianz.

Wakati Mreno huyo alianza kuwa na furaha kwa kuwapo kwenye orodha ya wafungaji, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 hakupendezwa na matokeo hayo.

"Nina furaha kuhusu mabao yale, lakini sio matokeo. Huu ni mchezo wa soka," alisema Ronaldo akiiambia DAZN.

"Tulipoteana dakika za mwisho na Parma walitumia makosa yetu.

"Sidhani kama matokeo haya ni kutokana na kuwa na ratiba ngumu. Tulitulia na kuonekana kutokuhofia.

"Tunajiamini kwa uwezo wa timu hii na kiufundi pamoja na benchi la ufundi tuko imara."

Juve kwa sasa hawajashinda mechi mbili zilizopita, wakiwa wametolewa kwenye Kombe la Coppa Italia na Atalanta Jumatano.

Licha ya sare hiyo, Juve bado wapo kileleni kwa msimamo na wamecheza mechi 22 bila kufungwa msimu huu.

## Solskjaer na mbeleko ya wachezaji ajira United

**MANCHESTER, England**

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer anafikiri kwamba nafasi ya kuteuliwa kuwa kocha wa kudumu wa Manchester United itategemeana na wachezaji wake.

Solskjaer alitangazwa kuchukua nafasi ya Jose Mourinho kwa muda, Desemba mwaka jana baada ya mreno huyo kufukuzwa.

Si tu kwamba wameshinda mechi nane tangu achukue mikoba, lakini pia soka wanalolicheza kwa sasa ni tofauti na zama za Mourinho.

Marcus Rashford, Anthony Martial na Paul Pogba walikuwa ni wachezaji ambao hawakuelewana na Mourinho, lakini sasa wameonekana kuwa kwenye kiwango cha juu zaidi.

Kuanza vizuri kwa Solskjaer kumeonekana kwa baadhi ya wachambuzi wa soka kwamba kunaweza kumfanya apewe mikoba hiyo moja kwa moja.

"Kazi hii ni kama matairi yanavyozunguka," alisema akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wake wa jana Jumapili dhidi ya Leicester City.

"Natakiwa kuwafanya wachezaji wacheze vizuri zaidi na kuwa kwenye ubora wao.

"Kama naweza kuifanya timu icheze vizuri, maana yake ni kwamba wachezaji wataonyesha vipaji vyao na mwisho wa siku tutakuwa tukipata matokeo mazuri zaidi."



## Valverde ahofia Messi kuikosa Real Madrid

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA Ernesto Valverde amethibitisha kwamba Lionel Messi atafanyiwa uchunguzi wa kina na timu ya madaktari wa Barcelona baada ya kuumia kwenye mchezo wa sare juzi Jumamosi dhidi ya Valencia.

Barca walikuwa nyuma kwa mabao ya Kevin Gameiro na Daniel Parejo hadi Messi alipofunga mara mbili kuwaepusha na kipigo kwenye mchezo huo.

Lakini Messi alionekana kuumia misuli ya nyama za paja katika kipindi cha pili na alipata matibabu kabla ya kurudi tena uwanjani kuendelea kucheza.

Huku Barca ikikabiliwa na mchezo wa Kombe la Mfalme ('Copa del Rey') dhidi ya Real Madrid Jumatano, Valverde anasubiri kupata majibu ya uhakika baada ya Messi kufanyiwa vipimo vya afya.

"(Messi) alikuwa na tatizo dogo," alisema Valverde. "Siwezi kusema kwa sasa ni kwa kiasi gani ameumia.

"Tunasubiri taarifa rasmi kutoka kwa timu ya madaktari. Kama yupo kwenye hali nzuri atacheza mchezo wa Jumatano."

Wakati huo huo, kiungo Ivan Rakitic amefurahishwa na namna Barca ilivyoweza kupigana na kusawazisha mabao hayo na kuweza kupata pointi moja kwenye mechi hiyo.

"Tulionyesha morali ya hali ya juu," alisema Rakitic. "Katika kipindi cha pili tulikuwa fiti zaidi. Ilikuwa ni kama tunacheza mpira wa mikono. Tulikuwa tunakosa goli."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# HIGUAIN, HAZARD WAANZA KUMKUNA SARRI CHELSEA

**LONDON,** England

MAURIZIO Sarri anategemea kupata ubora wa kutosha kutoka kwa Gonzalo Higuain na Eden Hazard baada ya wawili hao kila mmoja kutupia mabao mawili wakati Chelsea ikishinda 5-0 dhidi ya Huddersfield Town Jumamosi.

Baada ya kucheza mechi yake ya kwanza kwenye Ligi Kuu wakati Chelsea ikichezea kichapo cha aibu cha mabao 4-0 dhidi ya Bournemouth Jumatano, Higuain alifurahia upepo mzuri Stamford Bridge Jumamosi wakati wakiibuka na ushindi mnono wa mabao 5-0.

Higuain alifungua akaunti yake ya mabao Chelsea katika dakika ya 16, akiitendea haki pasi ya N'Golo Kante, na kisha Hazard akibadili matokeo na kusomeka 2-0 kabla ya kuelekea mapumziko.

Hazard alifunga bao lake la pili katika mchezo huo dakika ya 66 wakati alipomzunguka kipa Jonas Lossl, na kisha Higuain akarejea kimiani dakika tatu baadaye huku David Luiz akikamilisha hesabu dakika ya 86.

Sasa inabaki kuona endapo Higuain atathibitisha kuweza kufanikiwa katika klabu hiyo kuliko kama ilivyokuwa kwa Alvaro Morata na Olivier Giroud, lakini Sarri bado anaamini katika ushirikiano wa straika huyo na Hazard.

Wakati alipoulizwa kama Higuain anaweza kuwa kanyanga kama wengine waliokuwapo Chelsea, Sarri aliwaambia wanahabari: "Sijui. Ninajua vizuri sana kwamba, wakati alipotua, hakuwa katika ubora wake wa juu kimwili.

"Kwa sasa anajizatiti. Ukweli ni mwenye furaha sana kwa sababu, mbali ya mabao, hisia zangu anafaa kucheza karibu sana na Eden.

"Nadhani hilo, uwanjani, ukweli ni wazuri kucheza mmoja karibu na mwingine. Kwetu sisi, haya ni matumizi mazuri kwa Higuain kwa sababu atakuwa tayari kufunga mabao mengi, lakini pia kwa Eden."

Ingawa Chelsea iliweza kuweka kando kipigo dhidi ya Bournemouth, Sarri hawezi kujihakikishia 'Blues' hawataweza kukutana tena na dhahama ya matokeo kama hayo.

"Sina uhakika, lakini ninatumai [kupoteza kwa Bournemouth ni kitu cha mara moja]," alisema. "Kama nilivyosema hapo kabla, tunahitaji kujizatiti kiakili, tunapaswa kwenda katika kila mechi tukiwa na uamuzi na hamasa ya kiwango kile kile, na hatutaki kupoteza mechi ili kuwa na hamasa sahihi.

"Hivyo, tunahitaji kujizatiti. Tutajaribu, bila shaka kujizatiti. Tunahitaji kutambua kuwa, kwa mbeleni, hatukupaswa kupoteza mechi ili kuongeza hamasa."

## KWA UFUPI

### CHELSEA, UTD KWA POCHETTINO
CHELSEA inaweza kutoa upinzani kwa Manchester United kwa kumuajiri kocha wa Tottenham, Mauricio Pochettino katika dirisha la majira ya kiangazi. **(Sunday Express)**

### RAMSEY, POGBA PAMOJA JUVE
JUVENTUS inataka kumsajili kwa mara nyingine kiungo wa Manchester United, Paul Pogba, 25, na kumuunganisha Mfaransa huyo na nyota wa kimataifa wa Wales, Aaron Ramsey. Miamba hiyo ya Italia inatarajia kumsajili Ramsey akiwa huru wakati mkataba wake utakapomalizika Arsenal majira ya joto. **(iBancoNero, via Sunday Mirror)**

### PEP KWA BISSAKA, CHILWELL
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anataka kumsajili beki wa Leicester na England, Ben Chilwell, 22, pamoja na beki wa kulia wa Crystal Palace anayeichezea England U-21, Aaron Wan-Bissaka, 21, katika majira ya kiangazi. **(Sun on Sunday)**

### SOLSKJAER AMSHUKIA DE GEA
KOCHA wa muda wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amemtaka kipa Mhispania David de Gea, 28, kufuata nyayo za mshambuliaji Mfaransa Anthony Martial, 23, kwa kusaini mkataba mpya. **(Evening Standard)**

### HUDSON-ODOI LULU BAYERN
BAYERN Munich tayari imetenga ofa mpya kiasi cha pauni milioni 45 kwa ajili ya kumsajili kiungo wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, 18. **(Sun on Sunday)**

### BATSHUAYI HAKURUHUSIWA SPURS
TOTTENHAM ilikuwa tayari kufika dau la pauni milioni nane zilizohitajika Chelsea ili kumwachia kwa mkopo straika Mbelgiji Michy Batshuayi, 25, lakini 'Blues' haikuwa tayari kuwaimarisha wapinzani wao hao wa karibu, mshambuliaji huyo kuruhusiwa kujiunga na Crystal Palace. **(DH, via Sun on Sunday)**

### RABIOT AVIZIWA ARSENAL
ARSENAL inaamini itapewa nafasi ya kumsajili kiungo wa Paris St-Germain, Mfaransa Adrien Rabiot, 23, ambaye atakuwa huru katika dirisha la majira ya kiangazi. **(Sunday Mirror)**

### BROOKS AANDALIWA DAU SPURS
TOTTENHAM inaandaa pauni milioni 50 kwa ajili ya kutoa ofa kwa kiungo wa Bournemouth na Wales, David Brooks, 21, katika majira ya joto, wakati Manchester United ikiwa miongoni mwa klabu zinazovutiwa naye. **(Sunday Mirror)**

### COURTOIS AMTAKA HAZARD REAL
KIPA wa Real Madrid, Thibaut Courtois angependelea klabu hiyo kumsajili mshambuliaji Mbelgiji Eden Hazard, 28, kutoka klabu yake ya zamani Chelsea badala ya Mbrazil wa Paris St-Germain, Neymar, 26. **(Het Nieuwsblad, via Sun on Sunday)**

### KLOPP ATABIRIA MAKUBWA KEITA
kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp anaamini kuna nafasi kubwa ya kujizatiti kwa kiungo raia wa Guinea, Naby Keita, ambaye alimsajili kwa pauni milioni 53 kutoka RB Leipzig majira ya joto yaliyopita. **(Independent on Sunday)**

### VERRATTI KUIWAHI UNITED KESHO
KIUNGO wa PSG, Marco Verratti anaweza kuwa fiti kwa ajili ya mechi ya kwanza ya mtoano ya hatua ya 16-bora dhidi ya Manchester United Jumanne Februari 12, mwaka huu. **(Mail on Sunday)**

### SMITH-ROWE KUCHELEWA RB LEIPZIG
KIUNGO wa Arsenal, Emile Smith-Rowe, 18, amejiunga na RB Leipzig kwa mkopo katika dirisha la Januari, lakini hatakuwa tayari kuanza mazoezi na klabu hiyo ya Ujerumani hadi baada ya wiki tatu kutokana na majeraha ya nyonga. **(Independent on Sunday)**

### NEWCASTLE 'KUMFUNGA' BENITEZ
MMILIKI wa Newcastle United, Mike Ashley anatarajia kocha Rafael Benitez, ambaye mkataba wake utamalizika majira ya joto, atasaini mkataba mpya kufuatia kusajiliwa kwa kiungo Mparaguay Miguel Almiron, 24. **(Sunday Mirror)**

## HABARI MICHEZO

# TFF YANG'ATWA SIKIO SOKA LA WANAWAKE

**Na Somoe Ng'itu, ARUSHA**

WAKATI timu ya soka ya Taifa (Taifa Stars), ikihitaji ushindi wa aina yoyote dhidi ya Uganda ili iweze kukata tiketi ya kushiriki Fainali zijazo za Kombe la Afrika (AFCON 2019), Shirikisho la mchezo huo Tanzania (TFF), limetakiwa kuongeza nguvu kwa upande wa wanawake.

Taifa Stars itaikaribisha Uganda baadaye Machi mwaka huu katika mechi ya mwisho ya Kundi L.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mjumbe wa Baraza la Wadhamini la TFF, Abdallah Bulembo, alisema umefika wakati viongozi wa shirikisho hilo wakabadilisha vipaumbele kwa kuangalia uhalisia wa soka la wanawake kuwa na nafasi kubwa ya kuitangaza nchi.

Bulembo amemtaka Rais wa TFF, Wallace Karia na wadau wote wa soka kuungana kuelekeza nguvu katika soka la wanawake ambalo njia yake ya kufikia mafanikio ni fupi ukilinganisha na upande wa wanaume.

"Mimi soka la wanawake ndio kilio changu, nilisema bungeni Dodoma, ninasema hapa (Arusha) na nitaendelea kulipigania, najua uwekezaji wake hata ukichukuliwa asilimia 10 ya kile kinachowekezwa kwa wanaume, ninahakika tutacheza Kombe la Dunia," alisema Bulembo. Aliwataka viongozi wa soka wa mikoa kuendesha ligi kwa weledi katika ngazi za mikoa yao kwa sababu inasaidia kutoa nyota wapya wa Timu ya Taifa ( Twiga Stars) kwa kuwa hatuna wachezaji wanaotoka nje kuja kuitumikia timu hiyo.

Ushauri huo wa Bulembo umetokana na hotuba ya Rais Karia aliyoitoa kwa wajumbe wa mkutano mkuu hapo juzi kuwa soka la wanawake limefanya vema katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo iliyopita. Karia alisema mwaka 2016, timu ya wanawake ya Tanzania Bara maarufu Kilimanjaro Queens ilitwaa ubingwa wa Kombe la Chalenji na mwaka jana wakafanikiwa kulitetea huku pia ikitwaa Kombe la Jumuiya ya Afrika Mashariki katika michuano iliyofanyika kwa mara ya kwanza mwaka jana huko Burundi.

**UMETISHA...**



Mbwana Samatta (katikati), akipongezwa na wenzake baada ya kuifungia bao la kwanza Genk, katika ushindi wa mabao 2-1 walioupata dhidi ya Waasland-Beveren kwenye mechi ya Ligi ya Daraja la Kwanza A, Ubelgiji iliyopigwa Uwanja wa Freethielstadion mjini Beveren. **PICHA: BIN ZUBEIRY**

# Mchangani yapania Kombe la FA Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa timu ya Mchangani United Abdul Salehe, amejipanga kuhakikisha ananyakua ubingwa wa Kombe la FA mwaka huu licha ya michuano hiyo kuwa na ushindani mkubwa.

Akizungumza na Nipashe mara baada ya timu yake kufanikiwa kusonga mbele katika michuano hiyo inayoratibiwa na Chama cha Soka Zanzibar (ZFA), kwa mikwaju ya penati 5-4 dhidi ya Gulioni FC, alisema atakitumia Kikosi B katika michuano hiyo ambacho pia kina uwezo mkubwa wa kupambana.

Alisema lengo la kunyakuwa ubingwa wa michuano hiyo lipo pale pale na atajitahidi kupambana ili kuhakikisha linatimia na kuwaandaa wachezaji wake vizuri ili kukabiliana na timu yoyote watakayokutana nayo.

Aidha, alisema michuano hiyo itawapa nafasi ya kuwapima wachezaji wao wapya waliowasajili katika msimu huu wa dirisha dogo ili waweze kuwatumia katika kikosi kikubwa kwenye Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja.

"Tunapambana mwanzo hadi mwisho, nitawaandaa wachezaji wangu ili kuona sehemu ambayo kuna mapungufu na kuyarekebisha ikiwamo safu ya ulinzi na nina hakika tutasonga mbele zaidi katika michuano hii,"alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa Gulioni FC, Kaptani Juma Sinapo, licha ya kutoizungumzia sana mechi hiyo iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa Amaan juzi ndani ya dakika 90 na kisha changamoto ya mikwaju ya penalti kuchukua nafasi yake, alisema wachezaji wake wamejitahidi kujituma dakika zote za mchezo licha ya timu yake kutolewa kwa matuta.

"Haikuwa bahati yetu kusonga mbele katika michuano hiyo na kama tunavyojua Penalti hazina ufundi sana, sehemu ambayo tumeona mapungufu tutafanyia kazi ili wachezaji wajipange na Ligi Daraja la Pili Taifa," alisema.

## Usajili Kili Marathon wasogezwa mbele

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

TAREHE ya mwisho ya usajili kwa ajili ya mbio za kimataifa za Kilimanjaro Premium Lager Marathon (Kili Marathon) kwa mwaka wa 2019, zimesogezwa mbele hadi Februari 16, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa mbio hizo jana, John Addison, imeeleza kuwa uamuzi huo umetolewa na wandaaji wa mbio hizo kutokana na maombi ya washiriki wengi kutoka ndani na nje ya nchi.

"Tumepokea maombi mengi ya kusogezwa kwa tarehe ya mwisho ya usajili, kutokana na maombi hayo, sisi waandaaji tumeyaridhia kwa lengo la kuhakikisha wote wanaotaka kushiriki mbio hizi wanafanya hivyo", alisema na kuongeza:

**"Tunapenda kuweka wazi kuwa nafasi zikishajaa kabla ya tarehe hii mpya, tutafunga zoezi hili na hakutakuwa na nafasi za ziada; kuna nafasi 750 kwa Kilo meta 42 za Kiliman jaro Premium Lager; nafasi 5,500 kwa ajili ya kilometa 21 za Tigo na nafasi 5,000 kilometa tano za Grand Malt."**

Alitoa rai kwa wanaotarajia kushiriki kujisajili mapema ili kuepuka kukosa namba za ushiriki kama ilivyokuwa kwenye mbio zilizopita.

Addison alichukua fursa hiyo pia kuwapongeza wadhamini wenza wa mbio hizo ambao alisema ni pamoja na KK Security, Keys Hotel, wadhamini wa meza za maji Kilimanjaro Water, TPC Sugar, Simba Cement, AAR, Kibo Palace, Barclays Bank, Precision Air na CMC Automobiles, ambao alisema udhamini wao umechangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa mbio hizo, mwaka hadi mwaka.

Mbio za Kimataifa za Kilimanjaro Premium Lager Marathon, kwa mwaka huu zinatarajiwa kufanyika Machi 3, katika Uwanja wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, ulioko Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Michezo

Jumatatu Februari 4, 2019

Nipashe

Simba ilivyojisulubu Misri



HABARI UK. 18

PENYEZA...



Mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo, akipenyeza mpira dhidi ya beki wa Parma, Simone Iacoponi (kulia), kwenye mechi ya Serie A iliyopigwa Turin juzi na timu hizo kutoka sare ya mabao 3-3. **HABARI UK. 29**

# FIFA YALETA NEEMA SIMBA, YANGA SC

## Rais TFF atangaza zitakavyonufaika na kufafanua kuwa ni pamoja na...

**Na Somoe Ng'itu,** ARUSHA

KLABU zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara zikiwamo Simba na Yanga zote za jijini Dar es Salaam huenda zikapata mgawo wa fedha kutoka Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa) endapo zitatimiza vigezo vya kupata fungu hilo, imeelezwa.

Kauli hiyo ilitolewa baada ya Fifa kutangaza itaanza kuipa Tanzania fedha za maendeleo ambazo kwa muda wa miaka mitatu ilisitisha kutoa kutokana na Shirikisho la Soka nchini (TFF), kutokuwa na ripoti safi ya ukaguzi wa mapato na matumizi.

Akizungumza na gazeti hili jijini hapa, Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema fedha hizo zitaelekezwa katika programu za vijana na itazipatia klabu ambazo utekelezaji wake utaonekana wazi baada ya kujiridhisha.

Karia alisema maendeleo ya soka ya vijana ni moja ya vipaumbele vyake 11 alivyovitangaza wakati anawania nafasi hiyo na sasa vimebadilishwa na kuwa mpango mkakati.

Rais huyo alisema bila ya kuwekeza katika soka la vijana nchi haitaweza kupiga hatua kwa sababu wachezaji waliopo sasa watakosa nyota watakaorithi mikoba yao pale uwezo wao wa kucheza utakapopungua.

Alisema katika kuhakikisha malengo hayo yanatimia, TFF inajipanga kuwajengea uwezo wanachama wake na vile vile itaanza kupeleka ruzuku mikoani kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo.

"Fedha hizi za Fifa hatutazigawa kama sadaka, zitapelekwa moja kwa moja katika shughuli za maendeleo," alisisitiza Karia, ambaye aliwahi kuwa Makamu wa Rais wa TFF, chini ya Jamal Malinzi.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema serikali inaahidi kuendelea kushirikiana na TFF katika kuinua kiwango cha soka hapa nchini.

Mwakyembe ambaye alikuja kufunga mkutano huo mkuu wa mwaka, alisema kwa sasa inajipanga kuhakikisha inaandaa katika kiwango cha juu michuano ya vijana ya Afrika (Afcon U-17) ili kuifungulia njia Tanzania ambayo ina kiu ya kushiriki fainali za Afrika.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, aliwapongeza viongozi wa TFF kwa kusimamia vema mipango yake na kujiendesha kwa uadilifu kama serikali ya Rais John Magufuli inavyoelekeza.

## Kaseke ainusuru Yanga kufia Tanga

**Na Faustine Feliciane**

BAO la kipindi cha pili la mtokea benchi, Deus Kaseka (pichani chini), jana liliinusuru Yanga kuepuka kipigo kutoka kwa Coastal Union kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliomalizika kwa bao 1-1 katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Mchezo huo wa 21 kwa Yanga, ulikuwa na upinzani mkubwa na Coastal Union walikuwa wa kwanza kupachika bao dakika ya 29 kupitia kwa Haji Ugando kwa kichwa akiunganisha krosi safi kutoka upande wa kulia wa uwanja.

Yanga iliuanza mchezo kwa nguvu huku ikionekana kusaka ushindi, lakini Coastal Union walizidhibiti nyota wa timu hiyo.

Mabadiliko ya kipindi cha pili yaliyofanywa na kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera ya kumtoa Ibrahim Ajibu na kumuingiza Kaseke yaliiwezeha Yanga kufafanya mashanbulizi mfululizo.

Ajibu jana alibanwa vilivyo na mabeki wa Coastal na kusababisha kutolewa na kuingia Kaseke ambaye aliipatia Yanga bao kupitia krosi safi ya Gadiel Michael.

Coastal jana walijitahidi na kufanikiwa kuwadhibiti washambuliaji wa Yanga akiwemo kinara wa mabao, Heritier Makambo ambaye licha ya kupata nafasi alishindwa kupachika mpira wavuni.

Baada ya mchezo huo wa jana, Yanga sasa itaelekea Singida kucheza na Singida United kabla ya kurejea tena Tanga kucheza na JKT Tanzania.

Kwa matokeo hayo, yanaifanya Yanga kufikisha pointing 54 baada ya michezo 21 huku ikiiacha Simba kwa pointi 21 iliyocheza mechi 14.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >